# Nipashe

Jumanne Septemba 20, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581074

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



JACKPOT BABA LAO!

TZS. 346,249,820

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Mkurugenzi** mwingine wa PSSSF matatani matumizi milioni 200/-

UKURASA 3



**ZUCHU ATAKA LIGI NA WANAUME**

UKURASA 27

# Moto wawashwa kwa Panya Road

• **Mikakati** saba kuwakabili yasukwa... *Endelea ukurasa 2*



Marais kutoka nchi mbalimbali duniani waliohudhuria mazishi ya Malkia Elizabeth II wakiwa kwenye gari la pamoja kuelekea katika maziko Westminster Abbey, London jana. **PICHA: MTANDAO**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

MSHTUKO SENSA

**AOMBA KUHESABU WATU KWA DOLA MIL.5**

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2022, Anne Makinda, amesema wakati wa sensa...

UKURASA WA 7

**KESI YA KUPINGA TOZO KUNGURUMA MAHAKAMA KUU**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Masjala Kuu ya Dar es Salaam inatarajia leo kusikiliza shauri la...

UKURASA WA 8

**SABABU MTIHANI LA VII KUFANYIKA SEPTEMBA**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imelieleza Bunge sababu za mtihani wa taifa wa darasa la...

## Samia ashiriki maziko Malkia Elizabeth

UKURASA 25



## Kuku sasa waadimika sokoni

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA: HESABU ZETU KWA DE AGOSTO UK.32

**KABWELA** UK.7



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiagana na viongozi wa Jumuiya ya Watanzania waishio New York Marekani, baada ya mazungumzo yaliofanyika ukumbi wa ubalozi wa Tanzania nchini humo jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Mikakati saba ya kukabili 'panya road'

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ametaja mikakati saba ya kupambana na kundi la vijana wanaohusika na matukio ya uhalifu mitaani, maarufu panya road.

Moja ya mikakati hiyo ni kwa vituo vyote vya polisi kufanya kazi saa 24 kuanzia sasa.

Mkakati mwingine ni kuanza kwa operesheni maalumu ya kuwasaka na kuwakamata wanunuzi wa vifaa vya wizi, baada ya kubainika wanawatuma vijana hao kwenda kuvunja na kuiba majumbani.

Makalla alitaja mikakati hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa kuanzia sasa askari polisi hawatalala, watafanya kazi na vikundi vya ulinzi shirikishi.

Alitaja mkakati mwingine ni kuanza kuwafuatilia watu waliotoka gerezani ambao walihukumiwa kwa matukio ya uhalifu kujua wako wapi na wanafanya nini.

Hatua hiyo alisema imetokana na kugundua asilimia kubwa ya wahalifu waliokamatwa wengi wao wametoka kutumikia vifungo.

"Kuanzia sasa tunataka kufanya ufuatiliaji kila aliyetoka gerezani ambaye alihukumiwa kwa matukio ya kihalifu, tutamfuatilia tujue yuko wapi na anafanya nini, na hii ni kwasababu tumejiridhisha asilimia kubwa ya wahalifu tuliowakamata wengi wametoka kwenye vifungo," alisema Makalla.

Alisema serikali ya mkoa inaendelea kuweka mipango ya kudhibiti matukio ya uhalifu, huku akisisitiza wamejipanga kuhakikisha kunakuwa na hali ya usalama endelevu katika mkoa huo.

Katika operesheni iliyoanza zaidi ya watuhumiwa 135, vifaa mbalimbali vya wizi na wanunuzi wakubwa watano wa vifaa hivyo ikiwamo televisheni, simu na redio wamekamatwa na hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa dhidi yao.

Alisema asilimia kubwa ya watuhumiwa waliokamatwa walikutwa na dawa za kulevya ikiwamo bangi, akibainisha dawa hizo ni moja ya chanzo na kichocheo cha kufanya uhalifu.

Makalla alisema wataendelea na operesheni ya kuwatafuta na kuwakamata wote wanaojihusisha na biashara ya dawa hizo. Vijana wameulizwa kwanini wanajeruhi watu wanasema 'katika akili ya kawaida huwezi kumkata mtu panga mpaka uvute bangi na sisi kabla ya kwenda kufanya uhalifu lazima tuivute kwanza'.

"Kwa maana hiyo kuna haja ya kushughulika na vituo vyote vinavyouza bangi, vijiwe vipo mitaani vinajulikana nani na nani wanauza na wapi utapata bangi, watu wanakaa kwenye mapagala wanavuta, wengi wanaeleza wanao bodaboda wao wanawatumia katika uhalifu."

Kadhalika, Makalla alisema wamepata magari 102, kila kata itakuwa na gari kusaidia vituo vya polisi na ulinzi shirikishi kufanya doria.

Pia wamekubaliana kuweka mkutano maalumu kila wiki ya kwanza ya mwisho wa mwezi ambao utahudhuriwa na viogozi wa jeshi, Mkuu wa wilaya, Katibu Tarafa na wananchi, likiwa ni kufanya tathmini ya ulinzi katika maeneo husika.

Alitoa angalizo kwa wafanyabiashara wanaouza vifaa vya umeme na magari kujiepusha na ununuzi wa mali za wizi, akieleza kuwa yeyote atakayekutwa na mali za wizi hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Alisema watapambana na 'panyaroad' na mwisho wa siku watatokomea.

Kamanda wa Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema watatimiza wajibu wao wa kuhakikisha wananchi wa mkoa huo wanakuwa salama pamoja na mali zao.

Alimhakikishia Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ushirikiano na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kutekeleza kazi hiyo usiku na mchana.

"Wahalifu wakae chonjo tutafanya kazi kubwa na ya ziada kwa kuzingatia sheria kuhakikisha wananchi wa Dar es Salaam wanakuwa salama, tunaomba wananchi waendelee kutupa ushirikiano tutatunza siri za watoa taarifa, lengo la vyombo vya dola ni kuzuia na sio kupambana na uhalifu."

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa wilaya wa Mkoa wa Dar es Salaam. Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ludigija Ngwilabuzu alisema: "Sisi wakuu wa wilaya wote tunaunga mkono kauli ya Jeshi la Polisi na ya Mkuu wa Mkoa wa kuimarisha ulinzi na usalama katika wilaya zetu."

Alisema wamepokea maelekezo yote na wamejipanga kwa kufanya vikao na wenyeviti wa serikali za mitaa, kudhibiti magenge ya uhalifu.

***Imeandaliwa na Maulid Mbaga, Saumu Hassan, Evance Evarist (DSJ), Golden Kisapile (TUDARCo)**

# Kuku waadimika sokoni, watu walalamika

**Na Halfani Chusi**

BAADHI ya wafanyabiashara wa kuku wa kisasa na walaji wamelalamikia kuadimika kwa kitowewo hicho, huku wengine wakiuza ambavyo havijakomaa.

Nipashe ilibaini kuwapo kwa uhaba huo baada ya kutembelea masoko mbalimbali ambayo wafanyabiashara walikuwa wanauza kuku wadogo wanaokadiriwa kuwa chini ya miezi sita.

Katika soko la Shekilango, walionekana wafanyabiashara wengi wakisubiri magari yanayoleta kuku bila mafanikio. Hata waliobahatika, walipata kuku wadogo.

Aidha, Nipashe iliwaona wafanyabiashara wa chipsi na mama lishe katika masoko ya Mwananyamala na Shekilango wakiondoka sokoni bila kitoweo hicho.

Jabiri Omari, mfanyabiashara wa chipsi alisema amefikisha siku tatu hajapata kuku sokoni hivyo imemlazimu kuuza chips tu.

"Sokoni siku hizi kuku hawashikiki kabisa. Kila wanaokuja kwenye matenga tayari wana oda kwa hiyo unakaa unasubiri. Hata ukiwapata bei inakuwa kubwa tofauti na awali maana tulikuwa tunanunua Sh. 5,500 lakini sasa ni Sh. 8,000 kuku mmoja na mdogo," alisema.

Irene Mfyate, anayejishughulisha na mama lishe, naye alisema: "Kwa kweli kuku hawashikiki kabisa na hali hii imeanza kama wiki tatu hivi, sijui shida nini? Mimi nauza wali na nilikuwa nauza wali kuku, lakini kuku sina na siuzi wali kuku tena mpaka pale watakapoanza kupatikana kwa wingi,"alisema.

Mmoja wa wauzaji wa kitowewo hicho katika soko la Mwananyamala, Stephano Balama, alisema uhaba wa bidhaa hiyo unatokana na uzalishaji mdogo tofauti na ilivyokuwa awali.

"Sisi tunanunua kwa bei ya juu kutoka kwa walanguzi, hivyo lazima tutawauzia wateja bei kubwa. Hii yote kwa sababu serikali imepiga marufuku vifaranga kutoka nje bila kujua uwezo wa kuzalisha hapa kwetu ni mdogo, kuku wetu pia ni wadogo sio kama wale wa kutoka nje ya nchi,"alisema.

"Wafugaji wanalalamika bei za vyakula vya kuku ziko juu kwa hiyo hata gharama za utunzaji wake tofauti na awali, hivyo lazima bei itapanda kuanzia kwa mteja mdogo hadi mkubwa," aliongeza.

Kutokana na hali hiyo, mfanyabiashara wa kuku, Amiri Ali, alisema anafikiria kuachana na biashara hiyo kwa kuwa anapata faida ndogo na malighafi haipatikani.

"Hawapatikani hata ukiwapata unawapata wadogo halafu kwa bei kubwa kwa hiyo inakulazimu na wewe uuze kwa bei kubwa ukiwauza kwa bei ndogo faida hupati,"alisema.

Nipashe pia ilishuhudia kuku wadogo tena wachache wakiwa katika matenga tayari kwa kuwauziwa wateja waliokuwa wamefurika maeneo hayo.

Simoni Tarimo, ambaye ni mbobezi katika biashara akijihusisha na kununua kwa wafugaji na kuwauza sokoni anasimulia hali ilivyo alisema: "Unaenda kwa mfugaji kufuata kuku unakuta naye hana kwa sababu vifaranga havipatikani kwa urahisi kutoka kwa wazalishaji. Kingine, bei ya vyakula vya kuku iko juu kiasi kwamba mfugaji anaona hapati faida kutokana gharama za matunzo."

Mfugaji wa kuku maeneo ya Tandale, Fred Amidu, alisema kukosekana kwa vifaranga kutoka kwa wazalishaji ndio sababu ya kushindwa kuwafuga pamoja na wimbi la utapeli lililopo katika kupatikana kwa mbegu nzuri ya vifaranga.

"Licha ya serikali kuzuia vifaranga kutoka nje ya nchi, bado kuna shida ya kupata mbegu nzuri ya kuku. Mbegu inayopatikana hapa vifaranga havikui, unakuta mwezi unaisha bado kuku mdogo yupo kwenye rika la kifaranga

"Vile vifaranga vya kutoka nje ya nchi yaani wiki mbili tu tokea ulipoanza kuvihudumia vinakuwa tayari unapata kuku mkubwa na anakuwa na nyama nyingi. Sasa hivi tunawalisha wahitaji vifaranga na si kuku kama ilivyokuwa awali. Kitaalamu kuku hao wasipotimiza muda wake huwa wanakuwa na madhara makubwa kwa afya,"alisema.

## WAZALISHAJI WANENA

Mmoja wa wazalishaji wa vifaranga hivyo, Jeremia Jumanne, alisema: "Wakati wa kuzalisha vifaranga tunapata changamoto sana. Mbegu ya kuku wa ndani ni tofauti na wale kuku wa nje. Vifaranga vinakufa sana wakati wa kuzalisha katika vifaranga 100 lazima 30 vitapotea, havina uwezo wa kustahimili hali ya hewa sasa ukizingatia msimu huu kuna baridi kidogo.

"Hata huko tunakochukua mayai kwa ajili ya kuyatotolesha nako yanapatikana machache kimsingi mayai yanayokuja hayakidhi mahitaji ya kuzalisha kuku wengi."

Mtaalamu wa Lishe Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala, Bertha Shekalaghe, aliyataja madhara kwa mtu anapokula nyama ya kuku ambaye hajatimiza muda wake.

"Mtu anapokula nyama ya kuku wa kisasa ambaye bado hajafikisha siku 30 anajiweka katika hatari ya kupata magonjwa mengi sana ikiwamo presha ya damu, maradhi ya moyo, kuongeza sumu mwilini, pamoja na kuongezeka uzito bila mpangilio, upungufu wa nguvu za kiume," alisema.

## KAULI YA SERIKALI

Ofisa Mifugo Mkoa wa Dar es Salaam, Odetha Mchunguzi, alithibitisha kukosekana kwa kuku ambayo inachangiwa na kupanda kwa bei ya vyakula vya kuku na zuio la vifaranga kutoka nje.

"Ni kweli kuna uhaba wa kuku kwa sababu gharama za uzalishaji zimekuwa kubwa sana, lakini uzalishaji huu unatokana na zuio la kuchukua vifaranga kutoka nje ya nchi, kama serikali itaruhusu tena vifaranga kutoka nje ya nchi basi uhaba utapungua kama ilivyokuwa awali," alisema.

Alisema bei ya chakula cha kuku imeongezeka kutoka Sh. 50,000 hadi 80,000 kwa mfuko wa kilo 50, hali ambayo inakwamisha wafugaji wengi kuachana na biashara hiyo.

Kwa mujibu wa Mchunguzi, vifaranga vinavyozalishwa hapa ndani ya nchi vinaathiriwa na hali ya hewa ya kipindi hiki cha baridi kidogo vifaranga vinakufa sana hiyo nayo inapunguza uzalishaji kwa kiasi kikubwa.

Julai 22, mwaka huu, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akiwa jijini Dodoma alipiga marufuku uingizaji vifaranga kutoka nje ya nchi kwa lengo la kudhibiti ugonjwa wa mafua ya ndege na kulinda soko la ndani.

# Mkurugenzi mwingine PSSSF matatani kwa matumizi ya mil. 200/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI wa Mifumo ya TEHAMA wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Gilbert Chawe, amefikishwa kwenye Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma kwa tuhuma za ukiukwaji wa maadili na kukopa Sh. milioni 200.7 kinyume cha utaratibu wa mfuko.

Akisoma mashtaka hayo mbele ya baraza hilo mwishoni mwa wiki, Wakili wa Serikali, Hassan Mayunga, alidai mkurugenzi huyo alitumia fedha za umma za mfuko wa PSSSF Sh. milioni 135.6 bila kufuata utaratibu kwa kuzikopa na kununua gari binafsi, ilhali akijua fedha hizo hazikutengwa kwenye bajeti ya mwaka 2020/21.

"Katika shtaka la pili, mlalamikiwa, akitekeleza majukumu yake ya kikazi kati ya mwaka 2020 na 2021, alipokea na kutumia bila kufuata utaratibu fedha za umma kutoka PSSSF Sh. milioni 65.13 kwa ajili ya kulipia kodi ya ununuzi wa gari binafsi bila kufuata utaratibu," alidai.

Wakili huyo alidai kitendo hiko ni kinyume cha kifungu cha 6(1)(a), (b) na (f) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya Mwaka 1995, kikisomwa pamoja na Kanuni ya 3(2)(a) na (e) ya Kanuni za Udhibiti wa Mgongano wa Maslahi na Kanuni 7(d) na (e) ya Kanuni za Ahadi ya Uadilifu.

"Shtaka la tatu ni kupokea fedha Sh. milioni 65. 13 kutoka PSSSF kwa ajili ya kulipia kodi ya ununuzi wa gari binafsi,

lakini kiasi hicho kilitumika kinyume cha utaratibu pia hakikutumika kama ilivyokusudiwa," alidai.

Wakili Mayunga, alidai mlalamikiwa huyo alipata mkopo huo kinyume cha Sera ya Mikopo ya PSSSF na haukupita kwenye kamati ya mikopo ya taasisi.

Upande wa mlalamikaji ulidai mbele ya baraza hilo kuwa kipengele cha 4(2)(b) cha Sera ya Mikopo ya PSSSF ya tarehe 1/11/2018 kinasema mfuko utalipa asilimia 100 ya kodi kwa mkurugenzi mkuu na wakurugenzi wengine kwa gari jipya, lakini gari alilonunua mlalamikiwa halikuwa jipya, bali gari chakavu.

Upande wa mlalamikaji pia uliwasilisha vielelezo mbalimbali ikiwamo mkataba wa mkopo uliotiwa saini Aprili 24, 2021, orodha ya wanufaika wa mkopo na hati ya malipo ya Aprili 29, 2021.

Vilevile, ushahidi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) unaonyesha kuwa, gari alilonunua Chawe lenye namba za usajili T 607 DTQ, lilisajiliwa kwa mara ya kwanza na mamlaka hiyo Juni 12, 2020 na mmiliki wake wa kwanza ni Kipenka Musa.

Mnamo Mei 4, 2021, umiliki wa gari hilo ulihamia kwa Chawe kutoka kwa Salim Cars wa Dar es Salaam ambapo Salim Cars alilinunua kutoka kwa Jaji Musa wakati gari hilo lilishalipiwa kodi na serikali na ililinunua gari hilo na kumpa Jaji Musa kama stahiki yake alipostaafu.

Mlalamikiwa huyo alikana mashtaka hayo yote lakini akakiri mbele ya baraza kuwa mmiliki wa kwanza wa gari hilo ni Jaji Musa.

"Ni kweli gari hilo alipewa Jaji Musa kama stahiki yake, lakini aliliacha Toyota kwa lengo la kutafuta mnunuzi mwingine," alisema Chawe.

Alipoulizwa kama Salim Cars anayedaiwa kulinunua kutoka kwa Jaji Musa, alimwonyesha hati za malipo ya kodi, mlalamikiwa alishindwa kulithibitishia baraza.

"Mfuko wa PSSSF ulimlipa fedha za kodi Salim Cars, siyo mimi, malipo haya yalilipwa baada ya kujiridhisha na kiasi cha kodi kilichotakiwa kulipwa," alidai.

Mlalamikiwa alipoulizwa mbele ya baraza kama Sh. milioni 13.6 ambayo ni asilimia 10 ya Sh. milioni 135 iliyotakiwa kulipwa TRA kama gharama ya uhamisho wa umiliki wa gari

ililipwa, alishindwa kulithibitishia baraza malipo hayo.

# ...Baraza la Maadili lahoji vigogo wengine

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Maadili ya Viongozi wa Umma chini ya Mwenyekiti wake Jaji Mstaafu Ibrahim Mipawa, limehitimisha vikao vyake vya uchunguzi na kusikiliza malalamiko tisa dhidi ya 'vigogo' mbalimbali, wakiwamo wa mashirika ya umma.

Vikao vya baraza hilo vilianza Septemba 6, mwaka huu na vilihitimishwa mwishoni mwa wiki baada ya kusikiliza malalamiko hayo ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Baraza hilo linatekeleza majukumu hayo kwa matakwa ya Ibara ya 132 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kuhusu kusimamia tabia na mwenendo wa viongozi wa umma waliotajwa katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Waliofikishwa mbele ya baraza ni pamoja na aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Geofrey Chibulunje, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hoseah Kashimba, Mkurugenzi wa Fedha wa PSSSF, Beatrice Lupi, Mkurugenzi wa Ugavi na Ununuzi wa PSSSF, Ernest Khisombi, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Peter Sulle.

Wengine ni Mkurugenzi wa Sheria wa EWURA, Kapwete John, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Dk. Ayoub Rioba, Mkurugenzi wa Tathmini na Ufuatiliaji wa TACAIDS na Dk. Jerome Kamwela.

Katika malalamiko hayo, Mwenyekiti wa Halmashauri Mji wa Mbulu, pekee ndiye alikubali mashtaka hayo huku wengine wakikana tuhuma za ukiukwaji wa sheria ya maadili.

Baada ya kuhitimisha kusikiliza malalamiko hayo, baraza hilo litakaa kutoa uamuzi ambao utawasilishwa kwenye ngazi zingine za uamuzi.


World Health Organization

## Terms of Reference for Technical assistance to conduct induction training of DHMT members in Zanzibar

**Purpose of the technical assistance contract**
Under the supervision of the UHC cluster lead, the team of technical assistants will develop and implement a curriculum for induction training of the District Health management team in Zanzibar.

**Background**
The objectives of the UHC-LC are to assist the Member States to plan and implement relevant policies and strategies for the achievement of Universal Health Coverage and Health-related Sustainable Development Goal. The Universal Health Coverage Life Course (UHC-LC) team provides technical assistance and strategic support to improve access to quality people-centered health services along the life course, to improve access to medicines and medical devices, and to ensure financial access to health services for all including the most vulnerable.

In Zanzibar, the Minister of Health has appointed new members of District health teams. Most of the newly appointed District medical officers, district administrators, and district public health nurse officers were freshly graduated from training institutions with completion of a one-year internship course, but no previous experience in health administration and health service management. The honorable minister has requested technical assistance for induction training of the newly appointed DHMT members. The training will focus on improving the functionality and performance of Districts in Zanzibar to foster the implementation of the Health Sector Strategic Plan IV, based on the results of the ongoing assessment of District functionality in Zanzibar.

**Objectives of the consultancy**
The team of consultants will develop and deliver short courses to improve the capacities of newly appointed District Health Team members in strategic and operational planning, district services management, and result-based monitoring and evaluation.

**Deliverables**
1. Inception report
2. Short courses curriculum based on WHO resources for the following modules:
   a. Strategic planning and operational planning at the District level: improving the coverage of essential health services in Zanzibar
   b. Management and leadership in Primary health care Services: teamwork, multisectoral collaboration, resource mobilization, integration of disease control program, etc.
   c. Designing and implementing quality of care initiatives at the District level
   d. Emergency preparedness and response at the District level
   e. Improving the performance of support function at the District level:
      i. HR resources management,
      ii. Supply chain management for improved access to medicine and medical products at the District level,
      iii. Maintenance of infrastructures and equipment at the District level,
      iv. Managing finances and accounts
   f. Organizing community participation at the District level
   g. Conducting operational research and health system research at the District level.
3. Workshops reports for each module.
4. Final activity report

The titles and content of the modules may be adapted to new requirements of the Ministry of Health during the assignment.

**Requirements and planning**
- The contract will be granted for a maximum of 20 men*days per module.

**Selection criteria**
1. The selection will be based on the quality of technical proposals, and the education and experience of consultants.
2. The proposal should include all the modules with the proposed timeline for delivery.
3. The proposal must clearly provide the names and qualifications of consultants who will provide each module and the name of the lead consultant who will ensure the coordination of the activity. The proposal must also describe the teaching method.

**Characteristic of the provider**
- Only universities or public health training institutions may apply.

**Profile of consultants**

**Education:**
- Advanced University degree in Medicine or health-related field
- Master's in public health, business administration, public administration, or equivalent, with a concentration in a health service organization or hospital management.
- Holding a DrPH or Ph.D. will be an asset
- Qualification in adult learning and capacity development
- Postgraduate qualification in result-based planning, monitoring, and evaluation will be an asset.

**Experience:**
- At least 7 years of relevant experience in capacity building of Health workers and Health Service managers
- At least 5 years of working experience at the District and regional level
- Relevant experience in the management of primary health services and/or clinical units
- Relevant experience in designing and delivering short courses in Public Health including by coaching and mentoring.
- Experience in performance management and knowledge management.

**Remuneration**
- The remuneration will be based on UN consultancy rates for the United Republic of Tanzania.

**Application procedures**
- Interested institutions should send their technical and financial proposals and the resume of the consultants to the WHO Country Representative via the following email addresses: afwcotzremit@who.int clearly mark your email subject as ***Technical assistance to conduct induction training of DHMT members in Zanzibar***
- WHO has a smoke-free environment and does not accept the candidacy of smokers or users of any form of tobacco
- **Deadline for submission of applications is Monday 30th September 2022, 16:00 HRS**

2170524t02

# NEMC yataka uwajibikaji katika serikali za mitaa

Na Joram Gervas,TUDARCo

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewashushia mzigo wa kudhibiti kelele sehemu za starehe na ibada wenyeviti na wajumbe, kusimamia vyema na kutoa taarifa kwa wanaokaidi.

Akizungumza na Nipashe kwa simu, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Samuel Gwamaka, alisema usimamizi wa kudhibiti kelele ni jukumu la viongozi hao huku baraza likiwajibika kusimamia utekelezaji wa sheria ya mazingira.

"Tumeshazungumza sana kuwa sio jukumu letu sisi kama baraza kudhibiti kelele hizo sisi jukumu letu ni kusimamia sheria tu na kuingia kwenye changamoto kubwa zinazojitokeza, hivyo hizo kelele zinazo jitokeza katika mitaa ni jukumu la wenyeviti na wajumbe kusimamia," alisisitiza Gwamaka.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mara kadhaa anatafutwa kuulizwa kuhusiana na usimamizi na udhibiti wa kelele zinazotokea usiku kwenye nyumba za starehe na ibada, jambo ambalo kimsingi ni la viongozi hao.

Mei 30, mwaka huu, akizungumza na waandishi wa habari, mkurugenzi huyo alisema sheria inakataza kumbi za starehe na nyumba za ibada kujengwa karibu na makazi ya watu. "Kwa sasa kumekuwa na ongezeko kubwa la nyumba za ibada na kumbi za starehe za watu kwenda kustarehe na hivyo kuwepo kwa vyanzo vingi vya kelele, sheria iko wazi kuanzia muda fulani kiwango kinapaswa kupungua, watakaokiuka serikali itawachukulia hatua kali,"alisema.

Aidha, alisema kuna mikesha na ufungaji vipaza sauti nje inafanyika ambayo haina kibali maalum na kuwataka wananchi kuzingatia sheria na viongozi kuwajibika kwenye usimamizi.



Mchuuzi wa utumbo katika machinjio ya Vingunguti akiupanga kusubiri wateja, fungu liliuzwa kwa Sh. 3,000.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mbaroni madai utapeli wa milioni 190/-

Na Francis Godwin, IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa, linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kujipatia zaidi ya Sh. milioni 190 kutoka kwa wakazi wa mkoani hapo, akiwamo mmoja kwa ahadi ya kuwaagizia gari aina ya HOWO.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi, alimtaja mmoja wa watuhumiwa hao kuwa ni Michael Mbata (34) mkazi wa Dar es Salaam ambaye anayedaiwa kuwatapeli Sh. milioni 100 Abdalah Huel na Sh. milioni 50 Isaya Edward kwa ahadi ya kuwaagizia magari kutoka Japan na Uingereza kupitia kampuni ya FOA Motors ambayo yeye ni mkurugenzi mtendaji.

Bukumbi alisema mtuhumiwa huyo baada ya kujipatia fedha hizo, alikuwa akipoteza mawasiliano ya wateja wake hao na Agosti 20, mwaka huu, alikamatwa eneo la Chanika, jijini Dar es Salaam.

Alisema baada ya upekuzi wa polisi, Mbata alikutwa na magari mawili ambayo ni Nissan Dualis likiwa na namba za usajili T104 DZL leye thamani ya Sh. milioni 24 na Subaru Impreza T328 DZR lenye thamani ya Sh. milioni 18.

Kamanda Bukumbi alisema upelelezi wa tukio hilo umekamilika na kwamba mtuhumiwa atafikishwa mahakamani wakati wowote kuanzia sasa.

Bukumbi pia aliasema jeshi hilo linamshikilia Castor Mapunda (42) mkulima na mkazi wa Songea mkoani Ruvuma kwa tuhuma za wizi wa kuaminiwa baada ya kupokea Sh. milioni 41 kupitia akaunti yake namba 012424700 ya benki ya CRDB.

Alisema Mapunda alipokea fedha hizo kutoka kwa Sadiki Kikoti (45) mfanyabiashara wa Kibwabwa, Iringa ili amnunulie mahindi tani 60 na kutoweka nazo.

Kamanda Bukumi alisema baada ya kukamatwa, polisi walimpekua na kumkuta na gari jipya aina ya Toyota Premio lenye namba T029 EAC na baada ya kuhojiwa alikiri kutumia sehemu ya fedha hizo kununua gari hilo kwa gharama ya Sh. milioni 18.

MSHTUKO SENSA

# Aomba kuhesabu watu wote kwa Dola milioni 5

Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2022, Anne Makinda, amesema wakati wa sensa katika hali ya kushangaza kuna mtu aliomba zabuni akitaka apewe kazi ya kuhesabu Watanzania wote kwa malipo ya Dola za Marekani milioni tano.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Sensa ya Mkoa wa Singida na kupewa taarifa jinsi mkoa ulivyofanikiwa kwa asilimia 123 katika kazi hiyo iliyoanza nchi nzima Agosti 23, mwaka huu.

Anne alisema mtu huyo ambaye hakumtaja jina, alisema kama atapewa zabuni hiyo angewatumia wafanyakazi wa Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) ambao angewaliwapa posho ya Sh. 200,000 kwa siku na yeye angejilipa Sh. 300,000 kwa siku.

"Umaskini kitu kibaya, sababu mipango yote tuliifanya ilipokuja kwenye visentisenti, kuna watu walifikiri sensa hii kuna mamilioni ya fedha za ovyo, sababu tulivyoanza tu kuna mtu aliomba tenda ya kuhesabu watu, anasema mnilipe Dola za Marekani milioni tano, yaani mpaka tulitamani tumwone huyo mtu kwa sura," alisema.

Anne alisema lilikuwa jambo la kushangaza kumwachia mtu mmoja ahesabu watu Tanzania nzima, akisisitiza kuwa waliona ni utani.

Alisema wanashukuru kazi imekamilika kwa mafanikio makubwa na wananchi walionyesha ushirikiano mkubwa, hivyo uzalendo unaweza kuondoa kila kitu kinachoweza kuwa mgogoro.

Aliongeza kuwa takwimu za idadi ya watu zitakazopatikana, itabidi zifanyiwe kazi kuanzia mwaka huu, hivyo kila mkoa ujipange ili kuleta mabadiliko katika nchi.

Anne alisema kumalizika kwa sensa hii kuwe mwanzo wa maandalizi ya sensa nyingine itakayofanyika 2032, hivyo matatizo ya mipaka yakiyojitokeza katika sensa ya mwaka huu serikali ichukue hatua kuyatafutia ufumbuzi.

Awali Mratibu wa Sensa ya Watu na Makazi Mkoa wa Singida, Naing'oya Kipuyo, alisema mkoa umefanikiwa kuhesabu kaya kwa asilimia 123 na idadi ya majengo kwa asilimia 121.

Alisema makisio ya idadi ya kaya ambazo zingehesabiwa katika halmashauri zote saba za Mkoa wa Singida ambazo ni Iramba, Manyoni, Itigi, Ikungi, Mkalama, Singida Vijijini na Singida Manispaa yalikuwa ni 319,816 lakini hadi kazi inakamilika, kaya zilizohojiwa ni 394,171, sawa na asilimia 123.

Kipuyo alisema baadhi ya vikwazo vilivyojitokeza wakati wa kazi hiyo ni baadhi ya watu kutoelewa sensa ya majengo, hivyo kutoa ushirikiano kwa tabu, na ramani za maeneo ya kuhesabu watu kutofautiana na mipaka ya kiutawala.

Vikwazo vingine ni baadhi ya viongozi kukataa kutoa ushirikiano mpaka wapewe fedha, kuwapo wanyama wakali kwenye baadhi ya maeneo, baadhi ya watu kwenye kaya za mjini kutopatikana kwa wakati, ajali za bodaboda kwa makarani na kusababisha kuharibika kwa vishikwambi na migogoro ya mipaka ya kiutawala kati ya vitongoji.

## Serikali kuboresha mifumo ufuatiliaji mazao ya uvuvi

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali imejipanga kuboresha mifumo ya ufuatiliaji wa mazao ya uvuvi ikiwamo samaki pweza, ili kuhakikisha usalama wa mazao hayo na kuyaongezea thamani.

Aidha, imesema maboresho hayo yana lenga kuboresha maisha ya wavuvi na wadau wa zao hilo nchini.

Waziri Ndaki alisema pia imeweka mazingira mazuri kwa wawekezaji wa uchakataji wa zao hilo na ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kuna viwanda sita vya uchakataji wa zao la pweza na wawekezaji wawili wameonyesha nia ya kuwekeza katika mazao ya bahari ili kuongeza thamani ya zao hilo.

Waziri Ndaki aliyasema hayo jana, katika kongamano la kukusanya maoni ya kuboresha mkakati wa kufunga mfumo kielektroniki wa ufuatiliaji wa uvuvi wa pweza katika Wilaya ya Kilwa, jana jijini Dar es Salaam, ulioandaliwa na Shirika la Aqual Farm (AFO) kwa kushirikiana na Umoja wa Ufuatiliaji na Uhalalisho wa Mazao ya Bahari (SALT).

"Kwa hiyo napenda kuwahakikishia walaji wa mazao ya uvuvi kwamba mazao haya ni salama na kuwa serikali chini ya mifumo yake iliyowekwa inafuatilia kwa karibu sana mazao yote kabla hayajafika kwa walaji, wananchi waendelee kutumia mazao hayo kama chakula na biashara," alisema.

Kuhusu mfumo wa ufuatiliaji utakaotumika Kilwa, Waziri Ndaki alisema ni utaratibu nzuri wa kufuatilia ubora wa samaki huyo tangu anapovuliwa mpaka anapofika sokoni, hali itakayopandisha thamani ya chakula hicho na kuleta manufaa endelevu katika nchi.

"Tunawashukuru sana wadau wetu kwa kutusaidia kiasi cha fedha kuweza kuutengeneza mfumo huu, ili kufuatilie tangu uzalishaji wa pweza mpaka kwenye kuuza na itakapokamilika tunaamini kwamba tutapandisha thamani ya zao la pweza hapa nchini na kuwasaidia wavuvi wetu kujipatia kipato," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilwa, Eston Ngilangwa, alisema, mradi huo ni sahihi kuanzia katika halmashauri hiyo kwa sababu inajulikana kuwa hazina ya uchumi wa bahari nchini, na kuwakaribisha wadau wengine kuwekeza katika sekta ya uvuvi.

# Masauni asema kuna tishio kuenea itikadi kali

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limeridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi, huku serikali ikieleza kuwapo viashiria vya matishio ya kigaidi nchini vinavyotokana na kuenea kwa itikadi za msimamo mkali.

Itikadi hizo zinatajwa kusababisha watu kuhamasika na kujiunga na vikundi vya kigaidi na vikundi vyenye misimamo mkali nje ya nchi.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuph Masauni, wakati anawasilisha azimio la Bunge la kuridhia itifaki hiyo jana, alisema hali hiyo inadhihirishwa na matukio ya kukamatwa kwa baadhi ya watuhumiwa waliokimbia baada ya kufanya vitendo vyenye viashiria vya ugaidi katika nchi jirani.

Alisema kumekuwa na matukio yenye viashiria vya ugaidi wa ndani ya nchi (Domestic Terrorism), ambayo yamejitokeza katika baadhi ya mikoa ya Arusha, Geita, Mwanza, Pwani na Tanga.

Baada ya kuridhiwa kwa itifaki hiyo na Bunge, Tanzania sasa itawezesha kubadilishana wahalifu wa kigaidi kupitia makubaliano au mikataba maalum.

"Hivi karibuni kumeanza kuonekana dalili za baadhi ya wafuasi wa vikundi hivyo kuanza kuvuka mipaka na kuingia nchini kwa nia ya kuendeleza vitendo vyao vya kihalifu na kueneza itikadi za msimamo mkali za kuwashawishi watu kujiunga na makundi ya kigaidi.

"Hali hii inaifanya nchi yetu kuwa katika hatari ya kuathiriwa na harakati za vikundi vya kigaidi vinavyotuzunguka," alisema.

Kwa mara ya kwanza, Bunge la Tanzania lilitunga Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya Mwaka 2002, Sura ya 19, ambayo ilifuatiwa na kutungwa kwa Kanuni za Kuzuia Ugaidi za Mwaka 2014.

Kupitia itifaki hiyo, Tanzania itapata taarifa na takwimu za wahusika wa vitendo vya kigaidi ndani na nje ya nchi, chini ya Kituo cha Taifa cha Kuratibu Mapambano dhidi ya Ugaidi (NCTC).

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa, alisema kwa kuzingatia maudhui ya itifaki hiyo, kamati yake ilijiridhisha kuwa itifaki hiyo ina tija kwa nchi kwa kuwa tumekuwa na matishio ya viashiria vya ugaidi ndani ya nchi.

"Manufaa ambayo nchi yetu itapata baada ya kuridhia itifaki hiyo ni kubadilishana utaalamu na misaada ya kiufundi na kutumia kanzidata ya Kituo cha Afrika cha Masuala ya Ugaidi kilichoko Algiers, Algeria.

"Pia kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijensia zinazohusu ugaidi kupitia ushirikiano na nchi wanachama," alisema.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watu wasibweteke kupungua maambukizi mapya VVU

**TAARIFA** ya Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), aliyoitoa wiki iliyopita kuhusu kupungua kwa maambukizi mapya vya Virusi Vya UKIMWI nchini, zinatia matumaini kuwa sasa watu wamekuwa na uelewa na kuchukua hatua za kudhibiti maambukizi hayo.

Takwimu zilizotolewa zinaonyesha kuwa kutoka maambukizi 81,000 sasa yameshuka hadi 51,000 kwa mwaka.

Taarifa hizi ni njema kwa sababu wakati ugonjwa wa Corona ulipoingia nchini mwaka juzi watu wengi walisahau magonjwa mengine ya kuambukiza na nguvu kubwa ilienda katika kudhibiti virusi hivyo.

Nguvu iliyowekwa kudhibiti virusi vya Corona ilikuwa kubwa na kila mwananchi aliguswa kutokana na kasi ya maambukizi yake kusambaa kwa kiwango kikubwa na idadi ya watu waliopoteza maisha kutokana na ugonjwa huo kuwa mkubwa na kuitikisa dunia.

Tofauti ya maambukizi ya Corona na Virusi vya UKIMWI ni dalili za ugonjwa wa Corona kuonekana mara moja.

Wakati ugonjwa huo ukiingia nchini kuna waliosahau kama Virusi vya UKIMWI vinaendelea kushambulia watu kimya kimya.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi wa TACAIDS, mwaka 2017, walipofanya utafiti waliona kiwango cha maambukizi kilifikia watu 81,000 kwa mwaka, lakini hadi kufikia mwaka 2021 wanakadiria kuwa watu 54,000 wanapata maambukizi mapya.

Kadhalika, katika utafiti unaofanyika kila baada ya miaka minne hadi mitano, pia imebainika hata vifo vimepungua kutoka watu 32,000 waliokuwa wanakufa kwa mwaka na kufikia watu 29,000.

Taarifa hiyo ya TACAIDS, inasema kiwango cha unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU kimepungua kutoka asilimia 28 mwaka 2013 hadi kufikia asilimia tano.

Lengo la TACAIDS, ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 kiwango cha maambukizi mapya ya VVU, vifo na unyanyapaa inakuwa ni asilimia sifuri kwa kuwa Tanzania bila UKIMWI inawezekana.


Takwimu hizi zilizotolewa na TACAIDS zinaonesha kuwa pamoja na nchi yetu kuwa katika janga la ugonjwa wa Corona, lakini watu wamekuwa na tahadhari ya kujilinda na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI ili kuliepusha taifa kuwa na watu wenye magonjwa hali inayoisababishia kutumia gharama kubwa ya kuagiza dawa.

Fedha hizo zinazotumika kuagiza dawa kutoka nje ya nchi zitumike kwa ajili ya mambo mengine ya maendeleo ambayo yatainua wananchi wa Tanzania kiuchumi na pia kulifanya taifa kuwa na rasilimali watu wenye nguvu ya kufanya kazi badala ya kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa. Nguvu hiyo iliyotumika kupunguza idadi ya VVU, kupungua, iendelee kuhamasishwa maeneo mbalimbali nchini ili kila mmoja apate elimu ya kudhibiti ugonjwa huo.

UKIMWI unaua taratibu na mtu anapopata virusi hutumia gharama kubwa kuanzia kwenye dawa hadi lishe ili kuufanya mwili kuwa na nguvu. Dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI, zinahitaji mtu ale lishe bora itakayomwezesha kuhimili nguvu ya dawa hizo.

Kwa pamoja tukiendelea kutoa elimu ya kudhibiti ugonjwa huo tunaweza, na kama kaulimbiu ya TACAIDS inavyosema Tanzania bila UKIMWI inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** adverties@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.eippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kusimama hadharani kunaongeza ushindani

**LICHA** ya ajenda ya 50/50 au kuwa na uwiano wa kiusawa baina ya wanawake na wanaume kwenye masuala yanayohusu maendeleo ya taifa hata yasiyokuwa ya kisiasa kama udahili unaolingana wa wanafunzi wasichana kwa wavulana na idadi sawa ya wajumbe wa kamati mbalimbali za kimaendeleo.

Juhudi za kuwa na idadi ya wanawake katika ngazi za maamuzi likiwamo bunge bado ni tatizo muda wote likibakia kuhusishwa na mfumo dume unaokandamiza wanawake na kuwanyima fursa za kujitutumua na kuonyesha uwezo wao.

Lakini, wakati mwingine shida si mfumo dume pengine hata kuwa na maarifa au ujasiri wa kusimama jukwaani na kujenga hoja. Haya ni mambo ya kujifunza pia, hivyo watu wasidhani kuwa ya kujifunza ni hesabu pekee hata kuongea, kutembea hadharani ni kuweka ajenda zinazoeleweka hadharani.

Kwa mfano, inaelezwa kuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wabunge wa kuchaguliwa katika majimbo walikuwa 264 wanawake wakiwa ni 26 pekee, anasema Seleman Bishagazi, Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti Jamii Kipunguni Dar es Salaam, kinachofanyakazi pamoja na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), akihimiza kuwa ni vyema kinamama wakafahamu namna ya kujieleza na kuomba kura majukwaani. Si kwenye siasa lakini katika masuala yanayohusu maisha ya kila siku.

Anazungumza katika mafunzo kwa vitendo ya kuwajengea uwezo wanawake, ili wajiandae kuwania uongozi kwenye uchaguzi ujao, akieleza kuwa hali si shwari kujifunza kuomba kura ni jambo la msingi: "Taarifa ya Umoja wa Mabunge ya Dunia (IPU) ya mwezi Februari, 2022 kuhusu idadi ya wabunge nchini, inaeleza kuwa wabunge wa kuchaguliwa katika majimbo ni 264, wanawake ni wachache mno."

Taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inasema kuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, madiwani waliochaguliwa ni 3,953, huku wanawake waliochaguliwa wakiwa ni 260.

**Kumekuwapo na taarifa kwenye vyombo vya habari kuhusu baadhi ya trafiki kunaswa kwa tuhuma hizo na zimeendelea kuwapo kana kwamba hawajui ni makosa kujihusisha na vitendo hivyo.**

Kutokana na taarifa hiyo juhudi zinahitajika zaidi kuwainua kama kituo hicho kinavyofanya kwa kuanzisha mafunzo kwa vitendo, ili kusaidia wanawake kupata mbinu mbalimbali za jinsi ya kusimama majukwaani kuomba kura kwa wananchi.

Si jambo geni mbinu na elimu mbalimbali zinatumiwa kuwawezesha wanawake kuingia kwenye ulingo wa kisiasa na kuwa viongozi lakini bado mambo hayatengamaa ndiyo maana baadhi ya wadau wa kutetea haki zao wanabuni mikakati mipya.

Mafunzo hayo ya miezi sita, yaliyoanza mwezi uliopita yataendelea hadi Desemba mwaka huu, yakihusisha wanawake kutoka katika kata za Kipunguni na Majohe.

Kazi ya kusaidia wanawake kuwa viongozi na kuifikia ajenda ya '50/50' inahusisha wengi ndiyo maana Women Fund (WFT), wanawezesha mafunzo hayo ya kuwajenga wanawake ili waweze kusimama bila woga na kujinadi kwa wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2024 na 2025.

Bishagazi anasema kwenye mafunzo hayo, wanaandaa mfano wa mikutano ya kampeni na kuwasimamisha wanawake wenye nia ya kutiania kila mmoja kwa wakati wake anajinadi mbele ya wenzake wanaokuwa katika mafunzo hayo.

Ni vyema masuala kama hayo yakafikishwa vijijini na kinamama wakapata fursa kwani huko ndiko waliko wanawake wengi zaidi na wanaohitaji kubadilishwa kuanzia misimamo, mitizamo na mienendo.

Kinachowakwamisha wanawake ni pamoja na kushindwa kujinadi, wanapoomba kura, lakini pia ni waoga wanapoulizwa maswali na kuyajibu hivyo wakisaidiwa kuondokana na hofu hiyo kutasahihisha kasoro zinazowakwamisha.

Hata mimi naamini kwamba kwa njia hii watajengewa ujasiri na kujiamini na kuwahamasisha zaidi kusimama mbele za watu kutetea haki zao si kwenye uchaguzi.

## Kizimbani kwa mashtaka ya kughushi nyaraka mkimbizi

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Jonson Julius (34), na Moses Aluda wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, kwa mashtaka 11 likiwamo la kughushi nyaraka za kumruhusu Peter Matonya kwenda kuishi Canada kama mkimbizi.

Akisoma hati ya mashtaka jana mahakamani huko, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Sylvia Mitanto mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Francis Mhina, alidai washtakiwa hao wanatuhumiwa kwa kesi ya uhujumu uchumi.

Alidai, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka saba ya kughushi nyaraka mbalimbali, wakituhumiwa kuyatenda kabla ya Aprili 7, 2022 ndani Jiji la Dar es Salaam.

Mitanto, alidai washtakiwa hao kwa makusudi na kwa nia ovu walighushi hati ya kusafiria ya ukimbizi yenye jina la Peter Matonya, kwamba ni halali na imetolewa na Serikali ya Canada wakati wakijua siyo kweli.

Washtakiwa hao pia wanatuhumiwa kughushi nyaraka za

rukhsa ya kuishi Canada kama mkimbizi, nyaraka za kusafiri kwa dharura na kibali cha kuruhusu kuishi na kufanya kazi katika nchi hiyo.

Ilidaiwa Februari 28, 2022 washtakiwa hao walighushi tiketi ya ndege yenye thamani ya Dola za Marekani 850, ya siku hiyo ikionesha kwamba imetolewa na Shirika la Ndege la Canada kwa Matonya kwenda kuishi katika nchi hiyo ilhali wakijua siyo kweli.

Alidai kati ya Februari Mosi hadi Septemba 10, 2022, ndani ya Jiji la Dar es Salaam, washtakiwa hao walijipatia Sh. milioni 13 kutoka kwa Matonya kwa kumdanganya kwamba watamsaidia yeye na wategemezi wake ambao ni Peter William na Magdalena Nyaki, kwenda kuishi Canada wakati wakijua siyo kweli.

Ilidaiwa kwamba katika tarehe hizo ndani ya Jiji la Dar es Salaam, washtakiwa hao pia walijipatia Dola za Marekani 12,000 kutoka kwa Kasereka Joel kwa madai kwamba watamsaidia kupata kibali cha kwenda kuishi Canada.

Mitanto, alidai katika tarehe hizo, washtakiwa hao walitakatisha Dola za Marekani 12,000 na Sh. milioni 13 huku wakijua ni zao la njia ya udanganyifu.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa Mahakama Kuu ndiyo yenye mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kesi iliahirishwa hadi Oktoba 3, 2022 kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa waliopelekwa mahabusu.



Watoto wakijifunza kuchora juzi, ikiwa ni sehemu ya kampeni ya 'Chora Ramani', inayoendeshwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kuibua vipaji vyao ili viendelezwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ya kupinga tozo kunguruma Korti Kuu

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Masjala Kuu ya Dar es Salaam inatarajia leo kusikiliza shauri la kupinga tozo za miamala ya kielektroniki lililofunguliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

LHRC ilifungua shauri hilo namba 42/2022 Septemba Mosi mwaka huu dhidi ya Waziri wa Fedha na Mipango na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) kupinga kanuni za tozo hizo zinazotumika sasa.

LHRC pia imeomba mahakama iweke zuio la muda kuendelea kutumika kwa kanuni za tozo hadi kesi ya msingi itakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Kituo hicho kinaomba kanuni hizo zitenguliwe kwa kuwa zilitungwa bila kufuata utaratibu ulioainishwa ndani ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano kuhusu upitishwaji wa sheria ya tozo kwa njia ya ya kielektroniki.


Kituo hicho kupitia hati yake, kinaomba mahakama hiyo iruhusu LHRC kiwasilishe maombi ya kufanya mapitio ya kimahakama ili kutengua kanuni hizo.

Awali, mawakili wa serikali waliomba mahakama hiyo siku 14 kujibu hoja za LHRC (mleta maombi) ambapo mahakama iliamuru majibu hayo yawasilishwe Septemba 14, mwaka huu.

Tangu kuanza kutumika kwa kanuni hizo, kumeibuka malalamiko kutoka kwa baadhi ya wadau, wakitaka serikali kuachana na tozo hizo na kutafuta vyanzo vingine vya mapato wakiwa na hoja kwamba tozo hizo zinaumiza wananchi.

Hivi karibuni, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilitaka serikali kusikia kilio hicho cha wananchi na kukifanyia kazi kwa kuzingatia maoni yanayotolewa na wananchi dhidi ya tozo hizo zilizoanza katika mwaka huu wa fedha huku Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akisisitiza kuwa wanafanyia kazi suala hilo na watatoa taarifa ya utekelezaji.

## KABWELA



# Jalada kutua Korti Kuu mshtakiwa kukana jina

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu inalipeleka jalada la kesi namba 62/2020 katika Mahakama Kuu ili itoe uamuzi baada ya mshtakiwa Mzawar Katebaro aliyehukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela, kuendelea kulikataa jina hilo.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate, baada ya Wakili wa Serikali, Adolf Lema kuwasilisha kiapo kikionyesha kwamba Katebaro alikubali jina hilo, huku mshtakiwa akiendelea kulikataa na kudai kwamba yeye ni Mzawar Katabaro na siyo Katebaro.

Hakimu Kabate, alisema anataka Mahakama Kuu ipitie mwenendo wa kesi hiyo na itoe uamuzi ambapo awali Kabate alimuuliza mshtakiwa kama alisikia kiapo kilichotolewa na Lema na kama anajua madhara yake.

Katebaro, alimjibu hakimu huyo kwamba anaweza kuthibitisha jina lake kupitia vitambulisho vyake huku Hakimu Kabate alimwagiza karani ampe karatasi ili aandike jina lake kisha kutoa nakala ya hati yake ya kusafiria.

Alidai nakala hiyo inaonyesha jina lake ni Katabaro na siyo Katebaro huku akidai amewasilisha nakala kwa sababu hati halisi ameshindwa kuipata. Mahakama ilipokea nakala hiyo.

Kutokana na mkanganyiko huo, Hakimu Kabate aliagiza mwenendo wa kesi hiyo uchapwe na jalada lipelekwe Mahakama Kuu kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

Pia alisema, wale waliomkamata mshtakiwa huyo waendelee kumshikilia kwa kuwa hawezi kutoa amri yoyote ya kumpeleka mahabusu kutokana na utata uliojitokeza kwenye jina, akihoji "nitampeleka mahabusu kama nani, kama Katebaro au Katabaro?"

Awali, Wakili Lema alidai yeye ndiye aliendesha kesi hiyo hadi hukumu ikatolewa, ambapo Machi 25, 2020 mshtakiwa akiwa na wenzake watatu, walisomewa mashtaka yao na mshtakiwa huyo alikubali jina la Katebaro.

Pia alidai Januari 19, 2021 aliwasomea maelezo ya awali (PH), ambapo mshtakiwa huyo alikubali jina hilo la Katebaro na kwa uthibitisho alitia saini maelezo hayo na Aprili 8, 2021 mshtakiwa alianza kutokuonekana mahakamani.

"Juhudi za kumtafuta zilifanyika kwa kuanza kuwatafuta wadhamini wake na pia hati ya kukamatwa ikatolewa na kesi iliendelea kusikilizwa bila yeye kuwapo na mwisho washtakiwa walipatikana na hatia," alidai Lema.

Wakili huyo alidai kitengo cha mshtakiwa kukataa jina lake ni mawazo baada ya kutokea kwa tukio, hivyo akaomba hukumu iliyotolewa iendelee.

Agosti 31, 2021 mshtakiwa alidai mahakamani kwamba amekaa mahabusu siku 60 katika Kituo cha Polisi Chang'ombe kwa sababu wamemfananisha na mtu mwingine.

Mahakama hiyo ilitoa hukumu hiyo Novemba 8, 2021 baada ya kupatikana na hatia ya wizi wa gari na kukutwa na mali inayodhaniwa kwamba ni ya wizi.

Inadaiwa Desemba 3, 2019 mshtakiwa akiwa Mtaa wa Mwinyitanga ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, aliiba gari aina ya Toyota Porte lenye thamani ya Sh. milioni 12.5.

Pia anadaiwa Januari 12, 2021, akiwa eneo la Manyovu Buhingwe, Kigoma, alikutwa na gari hilo linalodhaniwa kuwa ni la wizi.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wa pili kushoto), akikabidhi vifaa kwa ajili ya Hospitali ya Uhuru wilayani Chamwino mkoani Dodoma jana, (wa tatu kushoto) ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson. NMB ilikabidhi magodoro, vitanda na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 50 kwa ajili ya hospitali hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sababu mtihani darasa la VII kufanyika Septemba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imelieleza Bunge sababu za mtihani wa taifa wa darasa la saba kufanyika mwezi Septemba, ikiwa ni pamoja na kusaidia kutoa matokeo kwa wakati na maandalizi ya ngazi nyingine ya elimu.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Tarime Mjini (CCM), Mwita Michael.

Mbunge huyo alihoji sababu za wanafunzi wa darasa la saba kufanya mtihani huo mwezi Septemba wakati mtaala unaelekeza masomo yakamilike mwisho wa mwaka.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kipanga alisema mtaala wa elimu unaelekeza mwanafunzi kutumia siku 194 za mwaka kwa masomo.

Alisema mtaala wa elimu pamoja na masuala mengine umezingatia muda wa kufanyika kwa mitihani ya ndani na ile ya kitaifa.

"Hivyo, kukamilika kwa ufundishaji na ujifunzaji wa maudhui ya muhtasari kwa darasa la saba hutegemea zaidi mpango kazi wa mwalimu.

"Kwa msingi huo, hadi kufika mwezi wa Septemba, walimu wa darasa la saba hupaswa kuwa wamemaliza kufundisha mada zilizobainishwa katika muhtasari ili kutoa nafasi ya ufanyikaji wa mtihani wa kitaifa," alisema.

Alieleza kuwa ufanyikaji wa mtihani wa darasa la saba mwezi Septemba unasaidia kutoa nafasi kwa usahihishaji na utoaji wa matokeo kwa wakati ili kutoa nafasi kwa wazazi au walezi kufanya maandalizi ya kuwawezesha watoto wao kujiunga na masomo ya ngazi nyingine za elimu ambazo masomo yanaanza Januari mwaka unaofuata.

# 'Mfumo imara utoaji wa taarifa utanusuru misitu'

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

KUWAPO mfumo imara wa kutoa taarifa za uhalifu na uharibifu wa misitu kutasaidia kunusuru maelfu ya hekta za misitu ya hifadhi ambayo imekuwa ikiathiriwa na shughuli za kibinadamu ikiwamo uchimbaji wa madini kiholela, ukataji miti ovyo, uwindaji haramu, kilimo na shughuli zingine.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), Allan Kazimoto, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na wadau kutoka mamlaka mbalimbali waliokutana mjini Morogoro kuhakiki mfumo wa kutoa taarifa za uhalifu na uharibifu katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia na hifadhi za taifa katika milima ya Tao la Mashariki.

Kazimoto alisema asilimia 62.4 ya watu waliohojiwa kwenye hifadhi za misitu ya asili za Kilombero, Mkingu, Milima ya Uluguru pamoja na Hifadhi ya Taifa Udzungwa wamekiri uhalifu unaendelea katika maeneo hayo ukichangiwa na shughuli hizo za kibinadamu.

Alisema kuwa tathmini nyingine inaonyesha asilimia 81.5 ya waliohojiwa walikiri kuwa hakuna mfumo rasmi wa utoaji wa taarifa za uhalifu katika hifadhi hizo, hali inayofanya taarifa kushindwa kufika kwa wakati au wakati mwingine kutofika kabisa kwenye mamlaka husika.

"Tathmini nyingine ilionyesha asilimia 86.2 wanamiliki simu za kiganjani, hivyo watafiti wakaona ni bora kuja na mkakati au mfumo kabambe wa utoaji taarifa za uhalifu kwa mamlaka husika kwa kutumia simu za kiganjani," alisema.

Alishauri mfumo huo kutumika kuboresha maeneo kadhaa yaliyoonekana kutokana na tathmini iliyofanyika na tayari mfumo huo wa kutoa taarifa za uhalifu na uharibifu umeshafanyiwa majaribio katika misitu mitatu ya Hifadhi ya Uluguru, Mkingu na Kilombero na hifadhi moja ya taifa ya Udzungwa.

Mhifadhi kutoka Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) Kanda ya Mashariki, Suleiman Burenga, alikiri uvamizi wa shughuli za kibinadamu umeendelea kuathiri uendelevu wa misitu.

Alishauri utafiti unaofanyika uguse hadi kwenye mamlaka za kisiasa ili mchango wa viongozi usaidie kukabiliana na hatua mbalimbali za kudhibiti uhalifu.

"Muhimu kuwa na mfumo huu ni kupata taarifa za uhakika ili kujua namna ya kukabiliana na uhalifu, ingawa zitakuja taarifa za kweli na za uongo, lakini muhimu ni kuzipokea na kuzifanyia kazi," alisema Burenga.

Mkurugenzi wa Utumiaji Misitu kutoka TAFORI, Dk. Chelestino Balama alisema mbinu zilizokuwa zikitumika awali, hazikuwa na mafanikio makubwa kwa kuwa nyingine zilikosa usiri ama kuzusha taharuki, ndiyo maana mfumo huu wa sasa umezingatia usiri mkubwa katika kufikisha taarifa za uhalifu na uharibifu.

# Ndalichako: Wakopesheni vijana vifaa badala ya fedha

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, ameziagiza halmashauri nchini kuwakopesha vijana vifaa vya kuongeza thamani ya mazao wanayozalisha badala ya fedha taslimu.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki katika ziara yake mkoani hapo kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kitalu nyumba (Greenhouse) inayotekelezwa na vijana katika halmashauri za Manyoni, Ikungi na Manispaa ya Singida.

Alisema uzoefu unaonesha kuwa vijana wanapokopeshwa fedha taslimu wanapotea, kikundi kinavunjika, mradi husika haufanyiki na fedha hazionekani.

"Vijana wanapohitaji vifaa kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao halmashauri badala ya kuwapa fedha taslimu mkopo wa vijana wabainishe ni vifaa gani wanavihitaji ili wanunuliwe watafanya marejesho inakuwa ni sehemu ya mkopo wao," alisema.

Prof. Ndalichako alisema katika mwaka huu wa fedha, serikali itajenga vituo vitano atamizi kwa ajili ya kuendeleza ujuzi kwa vijana ambavyo vitakuwa na vifaa vya uchakataji na usindikaji wa mazao mbalimbali.

Aliongeza kuwa vijana ambao wamepata mafunzo ya uzalishaji na wapo katika hatua ya uzalishaji waombe mkopo kupitia Mfuko wa Maendeleo kwa Vijana unaofadhiliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Mfuko wa Maendeleo ya Vijana mwanzoni kulikuwa na masharti sasa umefanyiwa maboresho hata mtu mmoja anaweza kuomba mkopo akakopeshwa sio lazima kiwe kikundi na kiwango cha mkopo kutoka Sh. milioni 10 hadi kufikia Sh. milioni 50," alisema.

Alisema serikali imeendelea kuwathamini katika kuwawezesha vijana zaidi ya 12,000 katika halmashauri 117 wamenufaika na mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba.

Alisema katika mwaka wa fedha 2022/2023, serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imetenga Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya kutoa mafunzo hayo kwa vijana 2,400 kutoka katika halmashauri 24 nchini.

"Rais Samia anathamini vijana na ndiyo maana amekuwa akitoa maelekezo ya kubuni miradi ambayo itawakwamua vijana kimaisha na kiuchumi kwa kuwapatia ujuzi utakao wasaidia waondokane na changamoto ya ajira kwa kujiajiri na kuajiri wenzao kupitia ujuzi waliopatiwa.

Alisema katika mwaka wa fedha 2022/23, ameamua kuongeza bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 250 hadi Sh. bilioni 990 na pia ametoa ruzuku ya mbolea, akitarajia vijana wengi kuchangamkia fursa hiyo kwa kushiriki katika kilimo biashara.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (kulia), akipata maelezo kwa Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa Kampuni ya Bima ya Sanlam, Ernest Selestine (wa tatu kushoto), alipotembelea mabanda ya maonesho kwenye tamasha la kutoa elimu ya bima kwa vyombo vya moto lililoandaliwa na Benki ya CRDB katika viwanja vya Posta, Kijitonyama jijini Dar es Salaam. Katikati ni Mkuu wa Kitengo cha Bima Benki ya CRDB, Moureen Majaliwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 530/- hutumika kila mwaka kuagiza ngano

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKURUGENZI wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Dk. Anselm Moshi, amesema serikali inatumia Sh. bilioni 530 kila mwaka kuagiza ngano kutoka nje ya nchi.

Hayo aliyasemwa katika mkutano wa wadau wa zao la ngano uliofanyika Wilaya ya Makete mkoani hapo na kwamba lengo la nchi ni kuzalisha zaidi ya tani milioni moja kwa mwaka.

"Tunatumia Sh. bilioni 530 kila mwaka kuagiza ngano kutoka nje, lakini katika nchi hii kuna ardhi nzuri ya kulima ngano, tuna wakulima wenye ujuzi wa kulima ngano, tuna hali ya hewa nzuri hakuna sababu ya kwenda kuagiza Argentina, Ukraine au Asia, tukatumia fedha zetu za kigeni badala ya kuzitumika kujenga barabara nzuri kama hii tuliyokuja nayo hapa," alisema Dk. Moshi.

"Namuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwamba hili linawezekana na kwa kweli nipende kumshukuru mkuu wa mkoa kuja na haya maono ya kwamba tunaweza tukafanya Njombe na hususani Makete tukazalisha ngano kwa wingi sana," alisema.

Dk. Moshi alisema kuanzia mwaka juzi walianza kuzalisha ngano mikoa ya Kaskazini na mbegu iliagizwa kutoka nchini Zambia.

"Kama Makete tutazalisha ngano sisi tutainunua yote inayozalishwa hapa, sisi tumekuja hapa ni wafanyabiashara sio watu wa maneno maneno, nimekuja hapa nijue tunaweza kulima hekari ngapi? Ni kina nani wanalima ili tukae mezani," alisema.

Alisema amesikia kuna kikundi cha vijana kina hekari 320 na nataka kuingia nao mkataba ili wazalishe ngano na kuinunua yote kwa bei ambayo watakubaliana.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alisema kutokana na uhitaji mkubwa wa zao hilo nchini, Wilaya ya Makete itakuwa ya mfano katika mkoa huo kwa uzalishaji wa zao la ngano. Aliagiza kuitisha mkutano wa wenyeviti kutoka vijiji vyote vinavyozalisha zao hilo mwishoni mwa mwezi huu ili kukubaliana namna ya kuanza uzalishaji mapema mwakani katika maeneo yote yanayopaswa kulimwa.

Wakati huo huo, aliwaagiza maofisa kilimo kuainisha majina ya wakulima kiasi cha mashamba na idadi ya wanayotaka kulima ngano ili kurahisisha ongezeko la uhamasishaji wa kilimo cha zao hilo.

Awali, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe, alisema ili kuendeleza zao hilo halmashauri imesajili wakulima 3279 ambao wanazalisha ngano ili kupata takwimu za maeneo yaliyolimwa msimu wa 2021/2022 na matarajio ya maeneo yatakayolimwa 2022/2023.

Makufwe alisema kwa usajili uliofanya ilibainika kuwa ekari 19,774.70 (hekari 8,005.95), zinatarajiwa kulimwa ngano msimu 2022/23 na matarajio ya uzalishaji kuwa tani 18,411.50 kwa malengo hayo mbegu tani 1,385 zinahitajika.

Baadhi ya wakulima akiwamo Alberto Sanga, alisema awali walikuwa wakilima kilimo hicho kwa mazoea na kuuza kwa walanguzi kwa bei wanayotaka wao hali iliyokua inafanya baadhi ya wakulima kuachana na zao hilo.

## 'China Trade Week' kushirikisha kampuni 300 maonesho bidhaa

**Na Frank Monyo**

CHINA Trade Week Tanzania (CTW), imeandaa maonesho makubwa ya bidhaa zaidi ya 300 kutoka kampuni zaidi ya 50 nchini humo yanayotarijiwa kufanyika mkoani Dar es Salaam.

Lengo la maonesho hayo yatakayofanyika Septemba 26 hadi 28, mwaka huu, kuwezesha biashara za kimataifa kati ya Tanzania na China na kuboresha ushirikiano na kufungua fursa. Tanzania inakuwa nchi ya sita kuwa mwenyeji. Akizungumzia maonesho hayo jana, Balozi mdogo wa Tanzania, Falme za Kiarabu zilizopo Dubai, Iddi Seidf Bakari, alisema China imekuwa mshikirika mkubwa wa biashara na Tanzania na kupitia maonesho hayo itatoa fursa kwa wafanyabiasha wa Tanzania kujifunza zaidi na kuimarisha ushirikiano kati yao.

"Katika maonesho hayo zaidi ya kampuni 50 za Kichina zitashiriki katika kuonesha bidhaa mpya kutoka sekta zaidi ya saba zikiwamo bidhaa za kielektroniki, viwanda, afya, mavazi, urembo na ujenzi.

"China imeendelea kuwa mshirika mkuu kwa Afrika na hasa Tanzania na tunakaribisha mipango yote ya biashara ya kimataifa, ushirikiano utakaoendelezwa kutoka CTW Tanzania na msaada wa sekta ya kitaifa ambayo imekuzwa kutokana na ushirikiano huo," alisema Bakari na kuongeza;

"Huku uchumi wa kitaifa ukiendelea kufungua milango yake, Tanzania ipo katika nafasi nzuri ya kusaidia na kuwezesha biashara duniani," alisema.

Alisema CTW Tanzania inajivunia kufanyika maonesho hayo kwa mafanikio makubwa nchi za Kenya, Ethiopia, Ghana, Morocco na Afrika Kusini sambamba na kutoa semina ya sekta za ujenzi wa miundombinu, nishati, kilimo, chakula, sayansi na teknolojia.

Naibu Rais wa Kampuni ya MIE Groups ya Dubai, Zahoor Ahmed, alisema: "Tunajivunia kuunganisha biashara ya kimataifa kupitia onyesho la kwanza la mchanganyiko litakalofanyika nchini Tanzania mwezi Septemba, jijini Dar es Salaam.

Alisema Serikali ya Tanzania imekuwa hodari katika msaada wao kuleta ubunifu na viwanda vya Kichina na kuunda ushirikiano mpya na kuendesha uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika uchumi wa Afrika Mashariki.

# Serikali yaonya ajira bila mkataba

SERIKALI imekumbusha kuwa ni kosa kisheria kumwajiri mfanyakazi bila kumpa mkataba kulingana na matakwa ya Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alitoa angalizo hilo jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariamu Kisangi aliyetaka tamko la serikali dhidi ya waajiri wasiotoa mikataba kwa wafanyakazi wao.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema suala hilo ni haki ya mfanyakazi na mtu yeyote asiyetoa mkataba wa kazi anapaswa kuchukuliwa hatua.

"Nitoe rai kama kuna maeneo ambayo tuna uhakika hawatoi mikataba ya kazi, mtupe taarifa ili tukachukue hatua zinazostahili," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Segerea (CCM), Bonnah Kamoli alitaka kujua mpango wa serikali kuhakikisha madereva wa magari ya abiria na mizigo wanapewa mikataba ya kazi ili kupata mafao na bima za afya.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Katambi alisema serikali imeendelea kusimamia sheria za kazi na kuwahimiza waajiri wote nchini kuwapatia wafanyakazi wao mikataba ya ajira kwa kuwa hilo ni takwa la sheria na ni haki ya wafanyakazi.

"Katika kuhimiza hili serikali ilitoa tamko na maagizo kwa wamiliki wa mabasi na malori tarehe 12 Juni 2022 na tarehe 22 Julai 2022 kwamba ifikapo tarehe 30 Agosti 2022 wafanyakazi madereva wote wawe wamepewa mikataba kwa mujibu wa sheria," alisema.

Aliliambia Bunge kuwa waajiri wengi wametekeleza na baadhi wanaendelea kutoa mikataba kwa wafanyakazi madereva.

Alisema ofisi imejipanga na inaendelea na ukaguzi maalum katika sekta ya usafirishaji na kuchukua hatua stahiki kwa waajiri wanaokiuka takwa hilo la kutoa mikataba kwa wafanyakazi madereva na sekta zingine.

"Serikali kwa kutambua na kulinda haki za wafanyakazi madereva, imeweka utaratibu wa kukaa vikao vya kushauriana na majadiliano na viongozi wa vyama vya wamiliki wa vyombo vya usafirishaji (malori na mabasi) na viongozi wa vyama vya wafanyakazi madereva kwa lengo la kupeana taarifa kuhusu kero zinazowakabili madereva na kuzitafutia ufumbuzi," alisema.



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, akisalimiana na baadhi ya wabunge Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ramani mpya ya sura ya Tanzania Bara yaandaliwa

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatarajia kuandaa ramani mpya nchi nzima inayoonyesha sura ya Tanzania Bara.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Ridhiwani Kikwete alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Angelina Malembeka.

Mbunge huyo alitaka kujua mpango wa kurekebisha ramani ya nchi baada ya baadhi ya maeneo kujazwa mchanga kuongeza ukubwa wa ardhi.

Akijibu swali hilo, Ridhiwani alisema ramani hizo zitaandaliwa kupitia mradi wa kuimarisha miundombinu ya upimaji na ramani utakaotekelezwa kwa mkopo utakaotolewa na Korea Kusini kwa muda wa miaka minne (2022/23 - 2025/26).

Alisema moja ya sababu ya kuhuisha ramani ni kuonyesha uhalisia wa sura ya nchi na kuhakikisha kuwa mabadiliko yanayotokea katika ardhi yanaonyeshwa kwenye ramani mpya.

Ridhiwani alisema ukubwa wa eneo na mipaka ya nchi unajulikana na ipo bayana, hivyo kujazwa mchanga kwenye baadhi ya maeneo hakuongezi wala kupunguza ukubwa wa eneo la nchi.

"Ramani ya nchi inayoonyesha sura ya nchi, huandaliwa ili kuonyesha hali halisi iliyopo ardhini ikijumuisha taarifa za kijiografia za asili ambazo ni pamoja na mito, maziwa, milima na bahari na zisizo za asili zinazojumuisha barabara, reli, mabwawa na miji," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum, Ritta Kabati (CCM), alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi, mipaka ya asili baina ya mikoa na mikoa, wilaya kwa wilaya, kata kwa kata na vijiji kwa vijiji imebadilika.

"Je, serikali ina mpango gani wa kubadilisha mipaka hiyo ili iwe sawa? Lini mradi wa Korea utaanza?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Kikwete alisema kuna baadhi ya mito ya asili imekauka kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kuibua migogoro na kusisitiza kuwa serikali imeshachukua hatua ya kupitia upya ramani ya maeneo hayo.

"Pale tutakapokuwa tumeandaa taratibu zote, mradi huu utaanza," alisema.




**Habari zote: Augusta Njoji DODOMA**

## Mbunge aibana serikali kuhusu mikataba madini

MBUNGE wa Bahi (CCM), Kenneth Nollo, amehoji ni lini serikali itaanza kupeleka mikataba ya madini na nishati ili ijadiliwe bungeni na kisha kuingia makubaliano na wawekezaji.

Nollo aliibua hoja hiyo bungeni jijini hapo jana wakati wa kipindi cha 'Maswali', akisema moja ya maeneo yanayolalamikiwa kwenye nchi zenye utajiri wa mafuta na gesi ni kukosekana kwa utawala bora kwa kutokuwa na uwazi wa mikataba hiyo kwa umma.

"Je, ipi mikakati ya serikali ya kuenzi mikataba katika kufikia lengo la kuwa na uwazi kwenye mikataba kwa umma?

Pia kutokana na mikataba kuja kupitia kamati, je, serikali haioni kuna umuhimu wa kubadilisha utaratibu ili mikataba hiyo ionekane kwa Bunge zima kwa kila kipindi cha mwisho wa mwaka?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geophrey Pinda, alisema uwazi kwenye mikataba upo.

"Kamati za Bunge zimeundwa na Bunge zinapopitia mikataba ni kwa niaba ya Bunge ni kupunguza hali ya kutoa upotofu wa jumla kwenye mikataba," alisema.

Hata hivyo, alisema kuhusu ubadilishaji wa mfumo ni jukumu la Bunge na kumshauri mbunge kutoa hoja ya kubadilishwa kwa mfumo uliopo kwa sasa wa mikataba kuwasilishwa kwenye kamati badala ya bungeni.

Alisema sheria ya mapitio na majadiliano kuhusu masharti hasi katika mikataba ya utajiri asili na maliasili za nchi sura ya 450(5), inatoa wajibu wa Bunge kuwa kwa mujibu wa ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema Bunge katika utekelezaji wa jukumu lake la kuishauri serikali, lina uwezo wa kuitisha mikataba inayohusu masuala ya utajiri na rasilimali za nchi na kuishauri serikali na kutoa azimio la kuondoa masharti hasi katika mikataba.

"Takwa hili la sheria linazingatia misingi iliyowekwa na sheria kwamba mikataba au makubaliano yaliyoingiwa kati ya serikali na wawekezaji yanazingatia haki, usawa na nia njema kwa pande zote na kuzingatia maslahi ya wananchi wa Tanzania," alisema.

Naibu waziri alisema serikali imekuwa ikiwasilisha mikataba kupitia kamati za kudumu za Bunge na kuzitolea maelekezo na ushauri kutoka kwa sekta husika na pale kamati husika inapoona umuhimu wa kufikisha mkataba mbele ya Bunge maelekezo hutolewa na kwa kuzingatia sheria husika.



## Waomba kulipwa haraka fidia kupisha ujenzi mradi

**Na Allan Isack,** BABATI

WAKAZI wa Mtaa wa Maisaka A Mjini Babati mkoani Manyara, wameiomba serikali kuharakisha mchakato wa kuwalipa fidia ili waondoke na kupisha ujenzi wa mradi wa maji.

Pia wameiomba Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati (BAWASA), kuharakisha mchakato wa ulipaji fidia ya kuhama ili wasiendelee kufanya shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo.

Ombi hilo lilitolewa na mmoja wa wakazi wa eneo hilo, John Kimaria, kwa niaba ya wenzake na kusema wamekuwa wakiishi kwa hofu wakidhani ipo siku watahamishwa kwa nguvu katika maeneo yao bila ya kulipwa fidia.

"Sasa hivi mioyo yetu imetulia baada ya Mkuu wa Wilaya kuzungumza na sisi kutuhakikishia haki zetu tutapewa, hivyo tuko tayari kupisha mradi huo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema serikali kupitia BAWASA imejipanga kuwalipa fidia wakazi hao.

Mkuu huyo alisema wakazi hao wanaoishi kwenye eneo hilo, serikali imeliandaa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji na watapatiwa fidia zao baada ya kufanyika tathimini.

"Shughuli ya kufanyiwa tathimini itakuwa ya wazi na hakuna mtu yeyote atakayeonewa au kudhulumiwa hivyo msiwe na hofu ya jambo lolote," alisema Twange.

Meneja Ufundi BAWASA, Honolath Sebastian, alisema wamepitia maeneo yote ambayo yanapaswa kulipwa fidia na yameorodheshwa yakiwamo maeneo ya nyumba za ibada.

"BAWASA tunapenda kuwahakikishia kwamba tutafuata utaratibu wote za kisheria katika kuwahamisha wahusika wote," alisema Sebastian.

Mthamini wa Mkoa wa Manyara, Pius Oswin, aliwatoa hofu wakazi hao na kusema kazi ya kufanya tathmini itaanza muda wowote kuanzia sasa.

# Waishukuru serikali kwa kuwajengea mradi wa maji

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

WAKAZI wa Kijiji cha Losoito wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wameishukuru serikali kwa kuwajengea mradi wa maji.

Wamesema kabla ya ujenzi wa mradi huo walikuwa wakitumia punda kama usafiri wa kwenda kutafuta huduma ya maji umbali mrefu.

Walitoa pongezi hizo jana wakati wa hafla ya uzinduzi wa mradi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, aliwataka wakazi wa kijiji hicho kutunza mradi huo, utakaowanufaisha wakazi zaidi ya 2,000 na mifugo yao.

"Awali wanawake walikuwa wanatumia punda kutembelea umbali mrefu kwenda kufuata huduma maji, lakini kupitia serikali mmeletewa maji karibu na makazi yenu hivyo tunzeni mradi huu," alisema Dk. Serera.

Diwani wa Kata ya Naisinyai, Taiko Laizer, aliishukuru serikali kwa kuwapatia mradi huo, akisema punda waliokuwa wakiwatumia kwenda kuchota maji watakwenda kufanya shughuli nyingine za uzalishaji mali.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Losoito, Samson Swakei, kwa niaba ya wananchi wa eneo hilo, walimkabidhi zawadi ya mbuzi Mkuu wa Wilaya, pamoja na zawadi ya ndama ikiwa ni furaha ya kuletewa maji.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kutufanikishia mradi wetu wa maji, sasa tunaomba ukarabati wa barabara kwa kuwa ni mbovu hata nyie viongozi mmeona ilivyokuwa na kipindi cha mvua haipitiki," alisema Samson.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), wilayani Simanjiro, Joanes Martin, alisema mradi huo, umekamilika kwa kutumia muda wa miezi mitano.

Kiongozi wa Vijana wa Jamii ya Wafugaji Tarafa ya Moipo, Emmanuel Lengitambi, alisema mradi huo, utawanufaisha wananchi 2,204 wa vitongoji viwili vya Losoito na Emishiye kwa huduma ya maji ya uhakika.

"Tunaishukuru serikali kwa kukamilisha mradi huu wa maji baada ya Kampuni ya God Mwanga Charity, kuchimba kisima chenye maji mengi katika kijiji chetu," alisema Lengitambi.

Mkazi wa kijiji hicho, Theresia Parmet, alisema wananchi walikuwa wakitembea umbali mrefu wa kilomita 30, kwa kilomita 15 kwenda Mirerani kufuata maji na kurudi nyumbani kilomita 15.



Balozi wa Rwanda nchini Tanzania, Meja Jenerali Charles Karamba (wa pili kulia), akifanya usafi katika stendi kuu ya mabasi jijini Arusha mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji, Hargeney Chirukulo. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Wanafunzi wapewa cherehani kushona taulo za kike

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WANAFUNZI wa kike katika Shule ya Msingi Ilkiurei Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru, wamepewa cherehani ya kushonea taulo za kike ili kujisitiri wakati wanapokuwa kwenye hedhi.

Cherehani hiyo, yenye thamani ya Sh. 3,000,000 imetolewa na shirika lisilokuwa la kiserikali la KUKUA PAMOJA TANZANIA, kwa ajili ya kushona taulo za kike kwa wanafunzi shuleni hapo.

Lengo la kutolewa kwa mashine hiyo ni kuhakikisha kila msichana anapata taulo za kike anapokuwa shuleni, kujistiri na kuhudhuria masomo kipindi chote bila kipingamizi cha hedhi.

Akizungumza wakati wa kukabidhi cherehani hiyo, Mkurugenzi wa Shirika la UKUE PAMOJA Tanzania, Ayubu Patrick, alisema wamelazimika kutoa msaada huo ili kuwawezesha wasichana wasiokuwa na uwezo wa kupata taulo wakati wa hedhi na wasishindwe kuhudhuria masomo yao.

Alisema kupitia mradi huo utawanufaisha wasichana 20 kwa kuwa wataweza kushona taulo hizo, baadaye wataweza kushona vipindi vitatu mpaka vinne kwa mwezi na kwa mwaka takribani vipindi 48 wakati wa hedhi kwa kushindwa kumudu gharama za taulo za kike.

"Tutakuwa na programu ya kuwafundisha wasichana 20 kushona. Wakijua watakwenda kuwafundisha wengine, kadhalika tutawafundisha elimu ya makuzi na mabadiliko ya kukua kimwili, athari zake pamoja na namna ya kujitunza katika hali za mabadiliko ya makuzi na ujana," alisema Patrick.

Alisema takwimu zinaonyesha bado wasichana wengi wanakabiliwa na tatizo la kushindwa kuhudhuria masomo kwa kukosa vipindi vitatu mpaka vinne kwa mwezi na kwa mwaka takribani vipindi 48 wakati wa hedhi kwa kushindwa kumudu gharama za taulo za kike.

Wasichana hao wamelishukuru shirika hilo kwa kutoa msaada huo, wakisema ni muhimu kwao kwa kuwa baadhi ya wasichana hushindwa kujiamini kipindi cha hedhi kutokana na kukosa uhakika wa kujisitiri.

Jemima James, Mwanafunzi wa Darasa la Nne, alisema wasichana wengi wa shule za msingi wanakabiliwa na tatizo la kushindwa kumudu kununua taulo za kike na baadhi kukosa masomo kipindi cha hedhi husababisha kuzorotesha kitaaluma.

"Kuna wasichana wakiwa kwenye hedhi, inawalazimu kuomba ruhusa na kubaki nyumbani, tukifundishwa kutengeneza sodo, itaturahisishia kuwa na hedhi salama na kusoma kwa amani," alisema Jemima.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ilkiurei, Beatrice Kapinga, alisema wanafunzi wakiwa na uhakika wa kupata taulo hizo shuleni, itaongeza ari ya wasichana kusoma kwa kuwa tatizo hilo halitakuwapo tena.



## HABARI KILIMANJARO

# Waonywa tabia kuomba kuhama vituo vya kazi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utwala Bora, Deogratius Ndejembi, amesema wahitimu wa mafunzo ya uchunguzi wa awali, wachunguzi wakuu na wasaidizi, yaliyotolewa na Taasisi ya Kuzia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) hawaruhusiwi kuhama katika taasisi hiyo hadi ifakapofika miaka mitano na kuendelea.

Lengo la kuzuia kuhama kwa wahitimu hao kwa kipindi hicho ni kuwapo kwa matumizi ya fedha zilizowekezwa kwenye mradi huo kwa kuwa makundi hayo matatu ndiyo pekee yamepatiwa mafunzo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), kulenga shabaha, ukakamavu na uokoaji wa fedha katika miradi ya maendeleo.

Ndejembo aliyasema hayo jana katika Shule ya Polisi Moshi wakati akifunga mafunzo ya awali ya uchunguzi huku akibainisha kuwa kumekuwa na tabia ya kuhamishwa kituo cha kazi baada ya kuidhinishwa kazini.

"Hakuna hata mmoja aliyelazimishwa kuomba kazi hii. Nasema asitokee mtu hata mmoja akaanza kutuma vimemo kwa kuwa anafahamiana nani au wanajua na mtu gani. Wafanye kazi miaka mitano TAKUKURU kabla ya kuhama kwenye taasisi hii ikiwa ni pamoja na miaka miwili kabla ya kuhama kituo cha kazi ili uwekezaji wa mradi huu kuonekana.

"Rais Samia Suluhu Hassan, amejipambanua katika hotuba mbalimbali akipiga vita rushwa. Kadhalika ametoa maelekezo maalumu katika ofisi yetu kuichukia, hivyo kutokana na maelekezo hayo, ameidhinisha zaidi ya Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya mafunzo haya kwa ajili ya kutokomeza rushwa na kuwa na taifa la watu waadilifu," alisema.

Pia alisema Rais ameridhia ajira mpya kwa kundi hilo, hivyo aliwataka kuhakikisha wanalipa deni hili kwa taifa kwa kwenda kufanya kazi kwa bidii, weledi na kwa uadilifu ili kupambana na rushwa.

Alisema kwa sasa nchi imetenga fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo na kuwataka wakasimamie kwenye miradi ya maendeleo zisije zikaliwe na mchwa.

"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) tayari ametoa taarifa na tunaona madudu yaliyotokea. Tunaomba mkasome na mkaanze kazi, ili thamani ya fedha za maendeleo kwenye miradi ikaonekane, hatutegemei kuona mnaenda kuwa tatizo kwenye jamii," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salmu Amudun, alisema kwa sasa rushwa imekuwa tishio kubwa kwa taifa endapo wataacha iendelee.

Alisema taasisi hiyo, ilikuwa na upungufu mkubwa wa ikama, hivyo upatikanaji wa watumishi hao, utasaidia kuendelea kutatua matatizo ya rushwa nchini.

"Wahitimu wote, watapangwa maeneo yenye matatizo wakasaidie kazi ya usimamizi wa miradi ya maendeleo, sitegemei kupewa vimemo nani apelekwe wapi au sehemu gani," alisema.

# Walalamikia kupanda holela nauli

**Na Mary Mosha,** SIHA

WANANCHI Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wameiomba serikali wilayani hapo kuwachukulia hatua za kisheria madereva wanaopandisha nauli kinyemela bila kufuata utaratibu.

Wamesema kitendo hicho, kinawaumiza wananchi hasa wa kipato cha chini.

Mmoja wa wananchi hao, Josiah Munisi, alisema licha ya bei ya mafuta kushuka, wameshangaa kuona nauli hazishuki, hivyo wameiomba serikali kupitia mamlaka husika kushughulikia jamba hilo.

"Ni kweli mafuta yameshuka na ruzuku iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa lengo la kuwasaidia wananchi lakini baadhi ya madereva hawaelewi. Ukifika kituo cha magari wanatangaza bei ya nauli waliyojipangia wao, kabla haujaingia hata kwenye gari.

Tunaomba mamlaka husika kuchukua hatua za kisheria sambamba na kuzungumza ili kufahamu wamelipa kiasi gani cha nauli," alisema Munisi.

Munisi, mkazi wa Ngarenairobi, West Kilimanjaro, alisema nauli kutoka Ngarenairobi hadi Sanya Juu ilikuwa Sh.1,000 kwa sasa imepanda kufikia Sh. 1,500 mpaka Sh. 2,000 kwa kuwa awali ilikuwa Sh. 500.

Vilevile alisema nauli ya Sanya Juu kwenda Lawate awali ilikuwa Sh.500 lakini kwa sasa ni Sh.1500, Bomang'ombe ilikuwa Sh. 1,000 kwa sasa ni Sh.1,500. Kutokana na kupanda huko kinyemela, wanaiomba serikali kuwasaidia kutatua jambo hilo.

Anna Mmari, mkazi wa Majengo Sanya Juu, alisema viongozi wa serikali hawapaswi kukaa ofisini bali wanatakiwa kutembea na kuangalia upandishwaji holela wa bidhaa mbalimbali za vyakula na usafiri ili kuangalia kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini.

Ramadhani Juma, mkazi wa Westi Kilimanjaro, aliliomba Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, kuwasaidia abiria ikawamo kuulizia nauli walizotozwa na kuangalia tiketi za nauli hizo.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA) Mkoa wa Kilimanjaro, Paulo Michael, alisema mamlaka hiyo haijatangaza upandishwaji wa nauli na kinachofanywa na baadhi ya madereva na utingo ni ukiukwaji wa sheria.

"Suala la upandishwaji wa nauli mamlaka haijatangaza, kwa hiyo tunalifuatilia na tukibaini tutachukua hatua kali za kisheri," alisema Michael.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, akizungumza na wanafunzi wenye ulemavu baada ya kukagua ukarabati wa majengo katika Chuo cha Marekebisho na Ufundi Stadi Sabasaba mkoani Singida. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bosi RUWASA ambana mkandarasi utekelezaji miradi ya maji Rombo

**Na Mwandishi Wetu,** ROMBO

MKURUGENZI Mkuu wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Clement Kivegalo, ameiagiza Kampuni ya Best One Ltd, inayotekeleza miradi miwili ya maji wiilayani hapo yenye gharama ya Sh. bilioni 5.3 kukamilisha kwa wakati ili kupunguza adha ya maji kwa wananchi.

Akizungumza jana baada ya kukagua utekelezaji wa miradi hiyo, Kivegalo alisema miradi hiyo inatekelezwa kwa pamoja kati ya RUWASA na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo, hivyo unatakiwa kukamilika kwa wakati, ili wananchi wapate huduma hiyo muhimu.

"Nimekuja hapa na wataalamu wangu kuona utekelezaji wa miradi ya maji ndani ya wilaya hii kutokana na wito uliotolewa na Mbunge wa Rombo, baada ya kuona utekelezaji unasuasua, nimetembelea pia mradi wa Njiro II, unaotekelezwa kwa fedha za mapambano ya ugonjwa wa UVIKO-19, fedha zilitolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Nimefarijika kuona umekamilika kwa kiasi kikubwa na tayari baadhi ya vijiji vimeanza kupata maji na tunataka kasi iongezeke," alisema.

Kwa mujibu wa Kivegalo, kuna tatizo dogo katika utekelezaji wa miradi hiyo ikiwamo ucheleweshaji wa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani na alikutana na wataalamu wake na mkandarasi kujadiliana nao.

"Moja ya miradi hii unaolalamikiwa kuchelewa ulikuwa chini ya Mamlaka ya Maji Rombo na sasa RUWASA. Tutashirikiana kuhakikisha unakamilika kama ambavyo wameomba," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema matatizo katika miradi hiyo, yanatafutiwa ufumbuzi na ameamtaka mkandarasi kuharakisha utekelezaji wa miradi.

Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo, Martin Kinabo, alisema kwa sasa miradi inayotekelezwa katika Wilaya hiyo ni miwili, mradi wa Njoro II, utagusa vijiji 15 utawanufaisha wananchi 24,454 na utagharimu Sh. bilioni 3.4.

Alisema mradi mwingine ni wa Ona utahusisha vijiji 29 na utagharimu Sh. bilioni 2.9 na miradi yote inaendelea vizuri.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Best One Ltd, Juma Mvamba, aliahidi kukamilisha miradi hiyo, kwa wakati endapo atawezeshwa malipo ya awali na mahitaji mengine kama msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani.

"Tunaendelea kutekeleza mradi mmoja, mwingine tayari umekamilika na wananchi wanapata maji na RUWASA wameahidi kutusaidia kukamilisha mradi kwa wakati," alisema.

Hivi karibuni Mbunge wa Rombo, Prof. Adolf Mkenda, akiwa katika ziara jimboni hapo, alilalamika kuchelewa kukamilika mradi mmoja na kutaka RUWASA kuingilia kati ili wananchi wa Rombo wapate maji.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba20, 2022
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI




## Chuo Kikuu cha Ardhi champata 'Samia' wao

## Utaalamu 'akili bandia' unavyowapa raha wafanyabiashara ndani, nje ya Tanzania




SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

### TANZANIA BUSTANI YA KIPEKEE

# Wanyama, wadudu, mimea ya ajabu imejazana visiwani Zanzibar na Bara



UKIZUNGUMZIA Bustani ya Edeni, hisia zinakwenda kwenye maandiko matakatifu kuhusu uumbaji wa binadamu na maagizo ya kutawala na kumiliki viumbe. Ni andiko zaidi, lakini unapofuatilia vivutio vya asilia vinavyoishi Tanzania unaweza kuifananisha na Edeni yenye viumbe vya kipekee visivyoonekana popote duniani.

Mbali na vito vya thamani vya tanzanite huko Mererani uwepo wa mbega wekundu 'Red colubus' Zanzibar na Iringa na maua ya 'Saint paulia' yenye thamani kubwa duniani yanayopatikana Msitu wa Amani Lushoto, unaweza kuona tena uwepo wa bustani ya maajabu.

Utayafikia maajabu hayo kupitia utalii ikolojia unaokupeleka kwenye misitu hasa ya asili kuona viumbe na mimea vivutio. Mathalani ni kwenye mashamba kulikosheheni mimea na miti aina nyingi, lakini ndani ya misitu kulikojaa wanyama mbalimbali, mimea kadhaa, wadudu wengi, ndege aina nyingi na za kipekee, nyoka kibao na viumbe wengine wa kuvutia na kushangaza kama vinyonga, mijusi, kenge na panzi.

Misitu ya asili ina thamani sana kiikolojia hii ni ile ambayo iko kwenye milima au miinuko na huvuta sana mawingu ya mvua kiasi kwamba hali ya hewa ya sehemu hizo huwa na unyevunyevu na ubaridi kwa kiasi fulani ukilinganisha na sehemu nyingine, anasema Dk. Felician Kilahama, Mkurugenzi (mstaafu) wa Idara ya Misitu na Nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii, anapozungumza na Nipashe kuhusu utalii ikolojia.

Anasema kabla ya kustaafu 2012, idara hiyo ilianzisha Misitu ya Hifadhi Mazingira Asilia (Nature Forests Reserves-NFRs tisa, ambayo ni pamoja na Amani na Nilo, katika Milima ya Usambara Mashariki-Muheza), Magamba (Milima ya Usambara magharibu huko Lushoto), Chome (Shengena) katika Milima ya Upare, Uluguru, Morogoro, Kilombero na Uzungwa Scarp katika Wilaya ya Kilombero, Rondo wilayani Lindi na Minziro wilayani Misenye mkoa wa Kagera.

Anasema kwa sasa zipo hifadhi misitu karibu 20 zenye hadhi hiyo ambayo ina maeneo muhimu kwa utalii ikolojia yenye kuvutia watalii wanaopenda kuona hali halisi ya maumbile asilia na jinsi yanavyotoa burudani ya kutosha kuliko maeneo wazi au mbuga za wanyama ambazo vivutio vikuu ni hao wanyama pekee labda ziwepo sehemu chache ambazo bila wanyama watalii wanaweza kuzifurahia.

**VIUMBE KIPEKEE**

"Pamoja na miti na mimea mbalimbali, Tanzania inafahamika kuwa ni taifa lenye viumbe adimu na vingine havipatikani sehemu nyingine duniani. Kwa kitaaluma rasilimali kama hizo hujulikana ni "endemic flora and fauna" yaani mimea na wanyama wasiopatikana popote duniani isipokuwa nchi hiyo vilipo." Anasena mtaalamu huyo wa uhifadhi.

Kwa mfano, katika Milima ya Usambara mashariki kuna mmea wenye biashara kubwa duniani katika nchi zilizoende-

INAENDELEA UK. 18

ELIMU

NA BEATRICE MOSES

# Chuo Kikuu cha Ardhi champata 'Samia' wao

YOLLANDA Kitama ni rais wa serikali ya wanafunzi, akiwaongoza wasomi wa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) cha Dar es Salaam. Msomi huyu ameandika historia ya aina yake kwa vile ndiye mwadada wa kwanza kushika wadhifa huo tangu ARU ilipoanzishwa miaka 48 iliyopita.

Anashika mamlaka katika mtindo unaofafanishwa kwa namna fulani na ilivyotokea kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa Rais wa kwanza mwanamke Tanzania, akiweka historia hiyo Machi 19, 2021 saa 4:00 asubuhi. Ndiye aliyekuwa Makamu wa Rais wa awamu ya tano, iliyoongozwa na John Magufulu, baada ya kifo chake, aliapishwa kushika nafasi hiyo kubwa ya kuwaongoza Watanzania na kazi inaendelea.

Kwa miaka mingi tangu kuanzishwa kwa chuo hicho mwaka 1974, awali kama tawi au chuo kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hadi kupanda hadhi mwaka 2007 na kuwa Chuo Kikuu cha Ardhi, kwa miaka yote hiyo hakikuwahi kuwa na mwanafunzi wa kike aliyewahi kuwa rais wa serikali ya wanafunzi (ARUSO).

Lakini, Yollanda, ameandika enzi mpya, rais huyo anasoma shahada ya Sayansi ya Geographical information Systems and Remote Sensing akiwa mwaka wa tatu.

Anachukua uongozi baada ya mwenye nafasi hiyo aliyekabidhiwa uongozi baada ya uchaguzi uliofanyika Mei mwaka huu kuugua hivyo kulazimika kuahirisha masomo, Yollanda katika kinyang'anyiro hicho aligombea nafasi ya Makamu wa Rais lakini kutokana na tatizo la kuumwa, amekwea ngazi na sasa ndiye rais.

Anashukuru akijinasibu kuwa aliipanga vyema timu yake ya kampeni na alishinda nafasi hiyo, kwa kura na haikuwa vinginevyo.

"Ilipofika Julai, rais aliyekuwa madarakani alipata matatizo ya kiafya hivyo aliahirisha masomo kwa muda, kutokana na katiba ya ARUSO, inamtaka Makamu wa Rais kuapishwa kuwa rais kuziba nafasi iliyo wazi kwa sababu zilizoelezwa na mhusika na pia kama katiba inavyoainisha ," anasema Yolanda na kuongeza kuwa alikula kiapo cha kuwa rais wa taasisi hiyo Agosti 2, 2022.

Mkurugenzi wa Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ardhi, Amina Mdidi, anabainisha kuwa Yollanda alikuwa makamu na kwamba katiba yao pamoja na mambo mengine inaelekeza jinsi ya kuziba nafasi ya rais iliyoachwa wazi kuwa nafasi inachukuliwa na makamu wake na hicho kilichofanyika.

Mkurugenzi Mdidi, anasema hata hivyo, katika chuo hicho pamoja na kwamba huyo ni mwanachuo wa kwanza wa kike kushika nafasi ya urais, kuna nafasi nyingine kadhaa ambazo waligombea na kuzipata wanafunzi wanawake ama waliteuliwa ikiwamo ya uspika, waziri mkuu na makamu wa rais.

Anabainisha kuwa serikali ya wanafunzi ni sehemu muhimu ya chuo kwa sababu wanatumika kama daraja kupitisha mambo kutoka kwa wanafunzi kwenda kwa uongozi wa chuo pia, kutoka kwa uongozi wa ARU kuwafikia wanafunzi.

"Huwezi kuzungumza kwa wakati mmoja na wanafunzi zaidi ya 7,000 lakini kwa sababu kuna viongozi ujumbe hufikishwa kwao nao kwa namna walivyojipanga unawafikia wanafunzi wenzao kwa wakati sahihi," anasema Mdidi.

Ametumia nafasi hiyo pia kuwataka wanafunzi wa kike kujitokeza kushiriki kugombea nafasi yoyote ya uongozi kwenye serikali yao, kwakuwa wanachuo wote wana haki sawa kama wanavyoshiriki kwenye masomo madarasani.

**SAFARI YA YOLLANDA**

Anasema alianza uongozi tangu akiwa anasoma shule ya msingi darasa la tano akiwa na miaka 11 akishika wadhifa wa kuiongoza idara ya afya na mazingira ya Shule ya Msingi Maburi wilayani Serengeti mkoani Mara.

"Nilipofika darasa la sita nikiwa na miaka 12 nilikuwa dada mkuu na niliongoza hadi nilipohitimu la saba na hata kutunukiwa cheti cha uongozi bora," anajinasibu Yollanda.

Rais wa ARUSO, anabainisha kuwa alipoingia sekondari kidato cha kwanza mwaka 2014 Shule ya Wasichana Kowak iliyopo mkoani Mara katika wilaya ya Rorya, alichaguliwa kiranja wa mawasiliano (communications prefect).

Anasema, akiwa kidato cha pili aliwania nafasi ya kiranja wa burudani lakini alishindwa na kuongeza:" Sikujisikia vibaya nilijifunza kitu na nilitulia na kuendelea kujihusisha zaidi burudani, nilishiriki maigizo,ngoma za asili, mashairi na midahalo," anasema.

"Nilipoingia kidato cha tatu nilipewa dhamana ya kuwa mwenyekiti wa klabu ya habari ya shule na kufanikisha malengo yaliyowekwa. Nikiwa Ifunda Girls High School, nilichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Klab ya FEM hadi nlipomaliza kidato cha sita."

"Nilipoingia chuoni moyo wangu ulitamani niwatumikie watu na niendelee kujifunza, kwenye uongozi wangu ninatamani kuendelea huku nje baada ya kumaliza masomo yangu ya chuo kikuu, hivyo nilianza kuwa kiongozi wa darasa wa kujitolea baada tu ya kuingia darasani kwa mara ya kwanza," anas[...]

Anasema, baadaye aliingia kw[...] kinyang'anyiro cha kuwania [...] ya ubunge kati ya wagombea w[...] wawili wasichana na wav[...] watatu hapo alishinda na ak[...] majukumu.

"Niliteuliwa na serikali ya [...] wanafunzi ARUSO iliyoingia ma[...] kani kuwa naibu waziri wa elim[...] hudumu pale kwa muda kisha nik[...] ishiwa wizara ya huduma na ma[...] nikaongeze nguvu katika ku[...] changamoto za wanafunzi," anas[...]

Anataja baadhi ya changa[...] ambazo amewahi kukutana [...] ikiwamo baadhi ya wapinzani [...] kumtengenezea kashfa kipindi [...] ombea nafasi mbalimbali.

Anazungumzia ratiba, aki[...] imekuwa ngumu kwake kutoka[...] majukumu imembidi hata ku[...] baadhi ya vitu ili aweze kumudu [...] kumu yake kikamilifu.

"Natamani kuwafungulia njia m[...] na wasichana wenzangu na ku[...] nyesha kuwa hata wao wana[...] kuwa viongozi na kielelezo che[...] Rais Samia Suluh Hassan," anasema.



Rais wa Chuo cha Ardhi, Yollanda, akichukua wadhifa huo baada ya miaka 48 ya mfumo dume. **PICHA: BEATRICE MOSSES**

TEKNOLOJIA

**NA BEATRICE PHILEMON**

# Utaalamu ‘akili bandia’ unavyowapa raha wafanyabiashara ndani, nje ya Tanzania

## Ni ‘Bizzyn system’, mfumo unaokusemesha, kukumbusha, kukuonya kila hatua usikwame




Mkurugenzi Mkuu, Emmanuel Kimaro. **PICHA: BIZZYN**

MFUMO wa kidijitali wa ‘Bizzyn accounting system’ unawatoa kikamilifu vijana wajasiriamali. Ni baada ya kufanikisha wafanyabiashara wadogo, kati na wakubwa kusimamia biashara zao kikamilifu kwa urahisi wakiwamo wanaofanya shughuli zao Tanzania, Kenya, Malawi, Nigeria na Afrika Kusini.

Unapozungumzia Bizzyn, siyo wengi wanaoufahamu au kuuelewa, lakini kikubwa ni mfumo wa kidijitali unaotumia teknolojia ya akili bandia au (artificial intelligence) kutambua na kushauri kwa usahihi wapi biashara yako inaelekea na kukupa miongozo sahihi ya kufuata ili uweze kufanikiwa au kukua katika biashara na kufikia viwango unavyovitamani.

Mfumo huu unaanzishwa rasmi mwaka 2021 na vijana Watanzania Emmanuel Kimaro, Mkurugenzi Mkuu, Abbas Musa, Ofisa Mkuu Uendeshaji, pamoja na Caroline Mwasigala, Ofisa Mkuu wa Teknolojia. Katika mazungumzo na Nipashe jijini Dar es Salaam, Kimaro anasema: “Tuliamua kuja na mfumo huu baada ya kugundua changamoto iliyokuwa ikiwapata wafanyabiashara wadogo, wakati na wakubwa kushindwa kusimamia biashara zao kikamilifu.”

Katika utafiti wao anasema waligundua wafanyabiashara wengi wanatumia makaratasi kutunza kumbukumbu za mauzo ya kila siku, kushindwa kutuma ankara (invoice), kushindwa kujua faida na hasara ,kufanya mahesabu ya biashara kwa ufanisi yote yakipelekea kuamua kuja na mfumo rahisi na rafiki kutumia.

Aidha, hadi sasa mfumo huu umekuwa mkombozi kwa wafanyabiashara wengi wa ndani na nje ya nchi katika kusimamia na kuendesha biashara zao kwa ufanisi kutoka kuanzishwa kwake na kupitia mfumo huo wameweza kujua matumizi ya mitaji ya biashara zao, wapi wanatumia zaidi pesa na kuwasaidia kusimamia bajeti zao kwa ufasihi.

“Hadi sasa zaidi ya wafanyabiashara 300 wadogo, wa kati na wakubwa waliopo katika sekta ya kilimo, afya, fedha, viwanda, hoteli, utalii, biashara na maduka ya dawa kutoka Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha wamenufaika na mfumo huu katika kusimamia biashara zao, mauzo na malipo.”anasema Kimaro.

Mbali na hilo, umewawezesha wafanyabiashara kujua matumizi ya mitaji ya biashara zao, kufahamu wapi wanatumia zaidi pesa na kuwasaidia kusimamia bajeti zao kwa ufasihi.

Anaongeza, “Tumeamua kuanzisha mfumo huu ili kusaidia wafanyabiashara kusimamia kazi zao na pia, kutunza kumbukumbu za mahesabu ya biashara zao kwa njia ya kidigitali.” Anasema.

Mbali na hilo, kampuni yake ina mpango wa kuwafikia wanafunzi kwenye vyuo mbalimbali ili kutoa elimu ya jinsi ya kuanzisha biashara zao na kuzisimamia kwa mfumo wa ‘Bizzyn accounting system’. anaongeza.

Kadhalika, wanaandaa shindano kwa wanafunzi watakao shinda kupata cheti na mitaji ya kuanzisha biashara ikiwamo kuwapa mafunzo jinsi ya kutumia

mfumo wa Bizzyn accounting system, ili kuendelea zaidi.

> “Mwekezaji huyu amekubali kusimamia kampuni yetu na kuhakikisha tunafikia nchi nyingine za Afrika kusaidia wafanyabishara wadogo, wa kati na wakubwa waweze kutunza kumbukumbu za mahesabu ya biashara zao kwa njia ya kidigitali,” anasema.

### NJE YA MIPAKA

Anasema, ili kufikia wafanyabiashara wengi zaidi katika nchi za Afrika ikiwamo Tanzania, Kimaro anasema, hivi sasa amepata mwekezaji kutoka taasisi ya Adanian Labs Africa kutoka Ireland.

“Mwekezaji huyu amekubali kusimamia kampuni yetu na kuhakikisha tunafikia nchi nyingine za Afrika kusaidia wafanyabishara wadogo, wa kati na wakubwa waweze kutunza kumbukumbu za mahesabu ya biashara zao kwa njia ya kidigitali,” anasema.

Aidha, anasema wamefanikiwa kupata wauzaji wa kazi zao, kutangaza na kutafuta wateja wa huduma zinazotolewa na kampuni ya Bizzyn katika nchi ya Kenya, Malawi, Afrika Kusini, Nigeria na Zambia na kwamba kampuni yake inakaribisha wawekezaji wengi zaidi ili iweze kufikia wafanyabiashara wengi zaidi na kutoa elimu jinsi ya kutumia mfumo wa Bizzyn.

### WANAVYOFANYA KAZI

Mfumo wa Bizzyn, unatumia teknolojia ya juu zaidi katika kurahisisha ufanywaji wa biashara, unamwezesha mwenye kampuni kujua faida na hasara itokanayo na shughuli zake kwa kipindi maalum na kusaidia kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha, anasema Kimaro.

Halikadhalika, unamrahisishia mfanyabiashara kujua idadi sahihi ya huduma, mizigo au bidhaa ambazo zipo kwenye biashara yake, au unampa taarifa mfanyabiashara bidhaa zinapokaribia kuisha na kuwakumbusha kuagiza nyingine mapema.

Vilevile, inawasaidia wafanyabiasha kuuza bidhaa zao na kupokea malipo kwa njia mbalimbali na hii imewawezesha wafanyabiashara wengi kulipwa kwa wakati na wateja wao, anaongeza.

Ofisa Mkuu wa Uendeshaji, Abbas Musa, anasema hivi sasa kampuni ya Bizzyn ina watumiaji ndani na nje ya nchi na watumiaji wakubwa ni wafanyabiashara wadogo na wakati.

“Kwa mfanyabiashara au mjasiliamali anayetaka kutumia tekinolojia hii anaweza kujisajili katika tovuti ya www.bizzyn.com na kuweza kutumia mfumo huu bure kwa mwezi mzima,” anasema.

Anasema, mfumo huu wa Bizzyn unawasaidia pia wafanyabiashara wote kuweza kuandaa mishahara na kuwalipa wafanyakazi wao kwa usasihi zaidi na kwa haraka.

“Tumeamua kuja na mfumo huu ili kuwaweka karibu wanunuzi na wasambazaji wa bidhaa kwa wafanyabiashara katika kujua matumizi katika biashara zao na hii mekuwa rahisi kwa wafanyabiashara wadogo na kati kujua taarifa sahihi za manunuzi pamoja na rekodi ya wasambazaji wa bidhaa zao,” anasema Musa.

“Mfanyabiashara au mjasiriamali anayetumia mfumo huu, Bizzyn inatuma taarifa za mauzo ya kampuni au biashara kwa mwenye kampuni kila siku inapoisha na pia kuwasaidia wenye kampuni na biashara kuweza kuendelea na shughuli zao bila wasi wasi kwa kujua kuwa Bizzyn ipo kwa aijli yao,” anasema Musa.

Anaongeza kuwa, mwenye kampuni atatumiwa ujumbe kwenye simu ya mkononi au kwa njia ya barua pepe au wassap kuhusu mauzo ya siku muda wa biashara ikifungwa jioni.

“Kama kampuni, tunashukuru sana kwa sababu mfumo huu umeweza kuleta mabadiliko makubwa kwa wafanyabiashara wengi ambao umewasaidia kuandaa mishahara na kuwalipa wafanyakazi wao kwa ufasihi zaidi na kwa haraka,” anasema Musa Aidha, anaekeza pia Bizzyn inawasaidia

Kutokana na changamoto iliyokuwa inawakumba wafanyabiashara wadogo na wa kati katika kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha kwa kushindwa kuwa na taarifa sahihi za mahesabu ya biashara zao, kwa kutumia mfumo wa kisasa wa Bizzyn zinatumwa moja kwa moja kwenye taasisi ya mkopo wa biashara.

ELIMU

NA PANKRAS LUOGA, MUHAS

# Wazazi, walezi nyumbani kusiwe uwanja wa kivita

## Tengeni muda ongeeni na watoto



Wazazi na walezi kazi ya kumbeba kwa upendo na kumlea mwanao haiishi, kumbuka kutenga muda uzungumze na wanao au wategemezi. **PICHA: MTANDAO**

Ni kawaida kila unayemsalimia atakujibu kuwa anaendelea vizuri, lakini unapoongeza kwa ukaribu na upendo zaidi, utapata mambo mengi ya ndani yanayomsibu.

Vivyo hivyo, kwa wazazi na walezi ni vyema kuwa na muda wa kutosha wa kuongea kwa ukaribu, upole na upendo na watoto wenu na familia wakiwamo wategemezi ili kujua wanayoyapitia katika maisha ya kila siku.

Hali ya uhusiano wa wazazi na watoto ipoje katika jamii yetu kwa sasa? Ni swali ambalo linahitaji tafakari, hasa kwa vile watu wengi leo ni wazazi na walezi wasio na muda au mpango wa kuongea na watoto wao.

Hata wakiupata, wanakuwa wakali kupitiliza kwa kila kitu watoto wanachokifanya bila kujali kuwa ni kizuri au kibaya. Hii ni kutokana na dhana potofu kuwa kuongea na mtoto kwa upole, heshima na upendo ni kumdekeza hivyo kuwaandaa kushindwa katika maisha yao ya mbeleni.

Kwa maneno mengine inasemekana ni kuwalea watoto kama mayai yanayobembelezwa ili yasivunjike au kupasuka.

Pia hali hii kwa sasa huletwa na kushamiri na kuenea kwa utandawazi hasa katika matumizi ya mitandao ya simu na kompyuta na kubadilika kwa mifumo ya maisha ikiwa ni pamoja na wazazi na walezi kujikita zaidi katika kutafuta pesa na mahitaji mengine ya kuendesha familia wakidhani kuwa wanachofanya ni kuwapa watoto wao maisha bora.

Hali hii inatokana na utamaduni wa kuona kuwa jukumu lao kuu kwa watoto ni kuwapatia mahitaji ya maisha kama shule bora, mavazi na makazi, lakini vyakula pamoja na burudani. Hali hiyo inapelekea wazazi au walezi kutojali muda wa kuongea na watoto wao kwa upole, heshima na upendo ili kujua changamoto wanazozipitia kila siku na vile ambavyo wanahitaji kutoka kwao au wanatamani kuwashauri ili kuzikabili.

Mfano walezi ambao wanajishughulisha na kazi za kuajiriwa maofisini au kujiajiri muda mwingi wametingwa sana na kutafuta hela hivyo huondoka nyumbani alfajiri na mapema na kurejea usiku watoto wakiwa wamelala. Baadhi ya walezi wametingwa na vikao vya maandalizi na sherehe za 'kichen-party, send-off, harusi na sikukuu. Pamoja na sherehe hizo kuna masuala mengine ya kiofisi na mambo ya ajira, biashara, ufugaji na kilimo.

> Pia kujadili kwa pamoja kuhusu faida na hasara ya kila njia ambayo mtoto angependa itumike na mwishoni kukubaliana nini kifanyike katika jambo linalojadiliwa iwe ni kuhusu shule, maisha na malengo mengine.

Hivyo kukosa nafasi au kutumia muda mfupi sana kukaa na watoto wao na wakipata mwanya huongea kwa ukali na haraka haraka kuhusu masuala ya maisha ya ikiwa ni pamoja na maendeleo na changamoto zao.

**ATHARI ZINAZOIBUKA**

Hali hiyo imekuwa na madhara makubwa kwa watoto wao bila kujua, baadhi ya athari hizo kwenye maisha ya watoto ni pamoja na kutojiamini na kushindwa kueleza maendeleo yao, changamoto zinazowakabili na mawazo yao jinsi ya kuzitatua. Halikadhalika, wanachukia kukaa nyumbani hivyo kushinda mitaani kwenye michezo ya kompyuta na kutazama video na tamthilia huko wanapata watu na marafiki wa kuongea nao kwa upendo na upole, kuamua kujihusisha na ulevi wa bangi, pombe na dawa za kulevya na uhalifu.

Chanzo cha yote hayo ni kutaka kuondokana na ukali wa wazazi au walezi pale nyumbani na kutafuta watu wenye muda wa kuongea nao kuhusu maendeleo, changamoto zao na jinsi ya kuzitatua.

Jamii ikumbuke, muda mwingi wazazi na walezi wanakuja wakiwa wakali hivyo watoto kushindwa kueleza mambo yao hasa magumu wanayoyapitia, lakini zaidi ya hayo wazazi na walezi wana mawazo ya jinsi ya kutatua changamoto bila kuwahusisha na kupata mawazo ya watoto ambayo ndiyo wenye matatizo na pengine kuwa na namna bora zaidi ya kuzitatua.

**UFUMBUZI**

Wazazi na walezi watenge muda wa kutosha wa kuongea na watoto kwa ukaribu, upole, heshima na upendo, kwa hiyo ni muhimu kujipa nafasi hiyo ili kuhakikisha watoto wanaoongea mambo yote wanayoyapitia.

Hii itasaidia watoto kujiamini na kuongea mbele za wazazi na wanajamii wengine, ikumbukwe pia hilo ni jukumu muhimu la wazazi, walezi kwa watoto wao na siyo kuongea na watoto kwa muda mfupi tena kwa ukali bila kusikiliza changamoto na mawazo yao, hivyo basi jukumu hili linaweza kufanywa na wahusika wakiwa nyumbani hasa wakati wa jioni baada ya kumaliza shughuli za kila siku.

Kwa mfano, wazazi na walezi wanaweza kumuuliza mtoto kwa upole, heshima na upendo kuhusu maendeleo yake shuleni ikiwa ni pamoja changamoto anazozipitia na kujua mawazo ya jinsi ya kutatua matatizo na magumu yanayomkabili.

Pia kujadili kwa pamoja kuhusu faida na hasara ya kila njia ambayo mtoto angependa itumike na mwishoni kukubaliana nini kifanyike katika jambo linalojadiliwa iwe ni kuhusu shule, maisha na malengo mengine.

Aidha, katika kutekeleza jukumu hili ni muhimu walezi na wazazi wakazingatia kutoa mahitaji muhimu ya watoto wao kama chakula, muda, upendo, heshima na kupewa hamasa juu ya faida za kuweka juhudi stahiki katika kutengeneza na kufanya maandalizi mazuri kwa ajili ya maisha ya baadaye.

Na kuwasisitiza kuwa maisha yajayo yanatengenezwa kuanzia leo. Zaidi ya yote wazazi na walezi wajitahidi kuwa karibu na marafiki wa watoto wao, walimu na watoto wao wenyewe ili kujua maendeleo na mienendo ya watoto shuleni na mitaani.

Kwa ujumla wazazi na walezi lazima watenge muda wa kutosha wa kuongea na watoto wao kwa upendo ili kupata taarifa za ndani za maisha yao, magumu wanayopitia, mapendekezo na kupata njia shirikishi za kuwasaidia.

Ikiwa wazazi na walezi watatenga muda wa kuongea na watoto wao kwa heshima, upendo na upole watapunguza au kumaliza changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na woga, kujiunga na uhalifu utotoni, mimba na ngono utotoni, kutokujiamini na kukosa watu wa kuwaeleza mambo yao na wanaoweza kusikiliza mawazo yao na kuyapatia ufumbuzi.

***Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili.***
***Maoni: 0757-645746***

SAYANSI

**NA DK. FELICIAN KILAHAMA**

MAAJABU WAHADZABE 3

# Walivyosheheni sayansi, utaalamu upo moto bila kibiriti,'bigijii' asilia

## ■Dawa nyingi za magonjwa karibu yote



Mwindaji wa Kihadza akirejea na kitoweo. **PICHA: FELLICIAN KILAHAMA**

WASOMAJI wa Nipashe namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka salama sio kwa kustahili, bali ni kwa mapenzi na rehema pamoja na fadhili zake nyingi.

Tunapomshukuru Mungu kwa kuanza wiki hii, leo tunaendelea na makala ya tatu katika mfululizo wa historia na hali halisi ya maisha katika kabila la Wahadzabe.

Ukiwachunguza wamejaa utaalamu na sayansi ya asili wana ufahamu mwingi na kwa ujumla hawa ni Watanzania, ambao wanajulikana kama 'wawindaji na wakusanyaji' wa zama za sasa wanaoishi kwa kutegemea sana misitu na mapori kama sehemu muhimu mno ya kupata riziki za kila siku.

Ingawa katika makala iliyopita nilieleza kwa ufupi kuhusu aina za vyakula wanavyotumia kwa mwaka mzima, ikiwa ni pamoja na maelezo ya baadhi ya matunda, leo tunaangalia zaidi kuhusu aina muhimu za miti ya matunda ambayo katika mjadala uliopita hazikuainishwa.

Kinachojadiliwa hapa ni aina za miti ambayo nilipozungumza na baadhi ya Wahadzabe wanaitaja kama ni muhimu kwa ustawi wao. Isichukuliwe kutoka kwangu kwamba miti ya matunda mingine haithaminiwi hasha, bali mibuyu ina upekee kwao maana wanasema mbegu na matunda yake husagwa na kutumika kutengeneza uji pia ni chanzo muhimu cha vitamini 'c' kuimarisha mfumo wa kinga mwilini na lishe.

Kufuatana na maelezo waliyoyatoa, miti muhimu ya matunda katika eneo lao ni pamoja miti wanayoitaja kwa majina ya asili kama 'undushibi' -Cordia sinensis na 'tafabe' Salvadora persica.

Kwa uzoefu wao, miti hiyo imejaa matawi mengi ambayo huzalisha matunda mengi kwa wakati mmoja na hasa hali ya hewa ikiwa nzuri wanavuna matunda mengi sana.

Msimu wa matunda kwao ni kati ya Oktoba na Machi na yanapoiva yanakuwa na rangi ya kuvutia na yana utamu wa aina yake hivyo kuwavutia walaji.

Aina nyingine za miti ya matunda yanayotumia ni pamoja na 'hlukwayebe' kitaalamu Grewia villosa, 'nguilabe' au Grewia ectosicarpa; mwingine ni 'embiribi' -Grewia forbesii, 'tl'atanabe' -Grewia pachycalyx; 'kongorobi' Grewia bicolor, 'musakabi'-grewia crenata), 'ts'elai' hyphaene ventricosa na 'hogoyobe' (ficus sycomorus).

Wanasema mti huo una matunda yanayopendwa na nyani kiasi kwamba kunakuwapo changamoto ya kuwazuia nyani wasile.

Isitoshe wanasema yanaharibiwa na wadudu na jitihada za kuwazuia nyani au wadudu mpaka sasa hazijafanikiwa.

Inasadikiwa miaka ya nyuma wadudu hawakuwapo lakini kutokana na ongezeko la joto katika ukanda wa bonde la ufa, kumekuwapo na kiwango kikubwa cha wadudu mbalimbali ambao hawana mazoea nao.

Miti mingine ya matunda ni pamoja na 'mikamasi' (Cordia spp), 'mikole' au 'mikoma' (Grewia spp) au 'miswaki' trees (Salvadora spp). Manufaa mengine kutoka kwenye msitu, licha ya kupata chakula na asali, ni pamoja na wanachokiita 'kaifl'oko'.

**BIGIJII, TIBA**

Ikiwa ni aina ya 'utomvu' unaovunwa kutoka mitini wanayoita 'hangatle' na 'shakwako' na kwa maelezo yao, baada ya muda utomvu waliovuna huganda na hutafunwa kama 'bigijii' kama kiburudisho lakini kwao ni kitu chenye manufaa kiafya.

Matumizi ya miti au mimea ni pamoja na kutibu magonjwa yanayowasumbua kutokana na sababu mbalimbali, hupata dawa, kadri inavyowezekana kutoka katika mazingira ya msitu na kutibu maradhi yanayowashambulia.

Aina ya dawa zinazotumiwa hutofautiana kati ya mti na mti au mimea inayopatikana katika mazingira ya msituni vilevile, hutofautiana kulingana na aina ya ugonjwa. Isitoshe, watoa taarifa walithibitisha kuwa wanao uzoefu wa muda mrefu hivyo wanafahamu aina mbalimbali za miti na mimea ambayo huitumia kujitibu.

Kwa uzoefu wao wa siku nyingi, wanasema ni rahisi kutibu magonjwa ya kawaida mfano, maumivu ya koo au matukio ya kuumwa na nyoka. Mathalani, aina ya dawa zilizotajwa ni pamoja na 'pilisi' (boscia angulifilia), ambayo magome ya mti huo hulowekwa kwenye maji kwa muda, kutikiswa na kutumiwa na kinamama waliojifungua.

Wanasema dawa hiyo hutumiwa kuosha matiti ya mama aliyejifungua ikiwa ni njia ya asili ya kuchochea utokaji na upatikanaji wa maziwa kwa wingi na kumwezesha mtoto kupata chakula cha kutosha.

Miti mingine ya dawa ni pamoja na "pawe" (Sclerocarya birrea), matunda kutoka kwenye mti huu hutumiwa kutengeneza 'losheni' ya kupaka kwenye ngozi; pia 'katchiko' (Strychnospota toum), matunda yake hulowekwa kwenye maji na baadaye kukorogwa mpaka kutoa povu linalotumiwa kufua nguo ni sabuni ya asili.

'Wi'ika" (Thylacium africanum), ni mti unaotibu aliyeumwa na nyoka. Tiba ni kuchukua mizizi yake na mara moja kuitafuna na kuigandamiza sehemu iliyoumwa wanasema ukifanya hivyo bila kuchelewa sumu hupoteza nguvu na majeruhi kuwa salama.

Mti mwingine wa dawa ni 'mukue' (Maeruaper vifola) majani yake hutafunwa na kumezwa polepole ili kutibu maumivu ya koo. Kadhalika, mti wanaouita "mondoko" (Entandrophragma caudatum), hutumika kuponyesha maumivu mwilini kwa kuchemsha magome na kunywa kama chai.

'Kindo' unatajwa kuwa iwapo mtu analo tatizo la kutopata choo vizuri wanaloweka mizizi kwenye maji na baadaye kunywa ili kumaliza tatizo hilo kama kawaida. Mti wa mwisho ulitajwa ni "morongodako' (Zanthoxylum chalybeum), ambao magome yake huchemshwa na kunywewa kutibu kikohozi na maumivu kooni.

**MOTO BILA KIBIRITI**

Kwa miaka mingi Wahadzabe wanatengeneza moto kutokana na miti kwa kuutumia utaalamu wao wa asili bila vibiriti vilivyozoeleka na wengi.

Wakati wa kutengeneza moto aina za miti iitwayo 'tlehako' (Sacleuxii newii) na "Lafako" au "hangatl'e" (Commiphora schimperi) hutumiwa.

Kwanza anayetaka kuwasha moto hutafuta nyasi au majani ya miti yaliyokauka na kuyaweka chini. Juu yake hulazwa panga linalowekewa kipande cha mti tayari kwa kuwasha moto.

Inafanyika hivyo ili wanapopekecha kipande cha mti kwa kutumia kijiti kigumu, na kutokana na msuguano mkali cheche za moto hutokea na kuweza kusababisha majani au nyasi zilizopo chini ya panga kushika moto na hatimaye kuweza kuwaka.

Moto hutumika kuandaa chakula hususani kuchoma nyama au kuoka viazi na mihogo pori ili kuongeza ladha. Kwa miaka mingi Wahadzabe wamekuwa wakitumia njia hii bila kusababisha madhara katika msitu wanamoishi.

Usiache kusoma makala ijayo, itaeleza kwa ujumla maisha yao kama jamii, mifumo na mambo wanayaona kuwa ni hatari kwao mwisho cha kufanyike ili Wahadzabe kuishi kama wananchi wengine.

# Wanyama, wadudu, mimea ya ajabu imejazana visiwani Zanzibar na Bara

INATOKA UK. 13

lea Ulaya na Marekani, unaoitwa "African violet" kibotania hufahamika kama 'Saint paulia'. Huu ni mmea mdogo lakini maua yake yanavutia sana na huwekwa ndani ya nyumba na kustawi vizuri, wakoloni walichukua sampuli yake zamani na kutengeneza biashara kubwa hadi sasa ni moja ya mimea yenye kununuliwa kwa wingi huko Ulaya na Marekani na thamani yake ni mabilioni ya dola za Marekani kwa mwaka. "Ua hilo halipatikani sehemu nyingine duniani isipokuwa Tanzania kwenye Milima ya Usambara Mashariki hivyo ni 'endemic plant' katika Tanzania. Kuna aina ya miti na mimea takribani 1,500 inayopatikana Tanzania pekee si sehemu nyingine duniani. Kati ya hiyo mimea au miti 325 unapatikana ukanda wa Pwani tu na mimea mingine kama 300 hupatikana katika ukanda wa Afrika Mashariki tu (huitwa near endemic plants species)." Anasema Dk. Kilahama.

Wanyama wanaotambaa au 'reptiles' kuna 360 na 85 wanapatikana Tanzania tu; kuna 'amphibians' 206 kati ya hao 86 wanapatikana nchini tu. Kwa mmoja mmoja, wapo Zanzibar ni Zanzibar red colobus monkey au nyani wekundu hao wanaopatikana visiwani pekee. Katika misitu ya Iringa kuna 'Iringa akalat' ambaye ni ndege wa aina yake. Ndani ya msitu wa Rondo kuna 'Rondo dwarf galago'.

Kule Pemba anasema kuna ndege aina yake aitwaye Pemba flying fox, Pemba white-eye bird, Pemba sunbird na Pemba green pigeon.

Dokta Kilahama anataja vivutio katika misitu ya Kilombero na Udzungwa kwamba yupo Udzungwa forest partridge ndege wa aina yake na Udzungwa weavers wote ndege na Udzungwa red-colobus aina ya nyani wakati maajabu mengine yako Kihansi kuna 'Kihansi spray toads' ni churamiti wanaozaa hawatagi mayai kama chura wa kawaida.

Aidha, anasema katika Misitu ya Milima ya Rubeho wilayani Mpwapwa makao makuu Dodoma kuna ndege mzuri anaitwa 'Rubeho akalat' wakati msitu wa Mazumbai, Lushoto una Mazumbai 'warty frog' chura wa aina yake. Katika Misitu ya Usambara Mashariki ambako kuna Amani na Nilo Nature Forest Reserves, kuna ndege waitwao 'Usambara akalat' na 'Usambara partridge' pia kuna aina ya vinyonga wenye pembe moja, mbili na tatu.

"Vilevile, kuna vipepeo wa aina mbalimbali wengi na ni biashara kwa wakazi wa Amani ambao kusafirisha mabua ya vipepeo kwenda nchi za nje na kujipatia kipato. Maeneo ya Amani yanavutia sana watalii ikiwepo utamaduni wa kilimo cha iliki, karafuu na viungo vingine, mashamba ya chai, unapata mwonekano mzuri wa mazingira katika eneo hilo. Hivyo watalii huburudika kwenye maeneo ya misitu lakini pia hata katika mashamba ya wananchi." Anasema Dk. Kilahama.



Ua aina ya St Paulia lenye thamani kubwa duniani na uzuri wa ajabu. Vyote hivyo vinapatikana Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

Misitu ya Uluguru kuna chura wa aina yake aitwaye 'Afrixalus uluguruensis,' kuna nyoka wa aina yake mwenye madoa mekundu ambaye ilisadikiwa kuwa aliwahi kuonekana katika msitu huo zaidi ya miaka 100 iliyopita. Lakini baada ya kufanya msitu kuwa hifadhi asilia alikuja kuonekana tena. Misitu ya Magamba ina ua lenye uzuri wa ajabu la 'Streptocarpus shumensis' na 'Usambara weaver' -ndege.

KUFIKIKA

Anaeleza kuwa ni upatikanaji wa viumbe hivyo muhimu, kwani mara nyingi havikai eneo moja hasa wanyama hivyo kwenye utalii wa aina hii watalii wanapotembelea ni kuwatafuta ndege au vinyonga au nyoka na mnyama adimu.

Anatoa mfano wa Australia kuwa yupo mnyama anayeishi juu ya miti, anayeitwa 'Australian koala'. Wakati akisoma huko wanafunzi na watalii wengine walipelekwa katika misitu ya mikaratusi anayoelezwa kuwa 'koala 'wanapatikana anasema: "Tulizunguka maeneo ya misitu ya mikaratusi kwa saa nyingi tukimtafuka Tulimuona baada ya muda mrefu kupita. Lakini watalii walifurahia kutembea tembea msituni, wakati wanafunzi sita tukaona ni kupoteza muda, maana mnyama ni mdogo mpaka tutumie kiona mbali darubini (binoculars).

"Nilichogundua kwa watalii ni burudani na viburudisho vya hapa na pale na kuona wanyama kama kangaroo wakikimbia na miguu miwili huku amebeba mtoto kwenye mfuko chini ya tumbo lake. Hivyo utalii ikolojia unayo mambo mengi ya kuangalia na ya kuvutia. Niwaalike wasomaji kutembelea Amani Nature Forest Reserve wafurahie mandhari yake. Pia waonje chai yenye ladha murua na viungo kadha wa kadha," anahimiza Dk. Kilahama kufanya utalii huo wa ndani wa kiikolojia.

## WANENAVYO MALENGA

# DUNIA YAMONG'ONYOKA

Dunia yamong'onyoka, jinsi inavyogeuka,
Utu umemalizika, unyama umeinuka,
Yale yanayofanyika, siyo ya kumithirika,
Watu walivyofyatuka, jambo la kusikitika.

Vituko vinainuka, vingine vinafumuka,
Visivyoaminika, ndivyo vinavyofanyika,
Watu wanaotumika, wajinadi kwa Rabuka,
Watu walivyofyatuka, jambo la kusikitika.

Haya yanayosikika, masikio yaumuka,
Watu wanavyoinuka, mtu mzima kuzika,
Tena anafahamika, kuzaa alihusika,
Watu walivyofyatuka, jambo la kusikitika.

Uchawi unatumika, ule usothibitika,
Kwamba baba wamshika, kuua amehusika,
Mahakama ya kupika, kaburini wamuweka,
Watu walivyofyatuka, jambo la kusikitika.

Si ajabu yasikika, watoto wanainuka,
Baba yao wamshika, kwamba amewachawika,
Waamua kumchoka, kuamua kumfyeka,
Watu walivyofyatuka, jambo la kusikitika.

Ya Ruvuma kusikika, mengine tunakumbuka,
Kudai wamerogeka, wazee wao kufyeka,
Hili bora kufutika, kusikia tunachoka,
Watu walivyofyatuka, jambo la kusikitika.

Tuambizane hakika, tufanyayo twapotoka,
Imani tunazoshika, pabaya zatupeleka,
Bora Mungu kumshika, huyo anaaminika,
Watu walivyofyatuka, jambo la kusikitika.

Urithi unahusika, kuleta ya kukereka,
Watoto wanainuka, mali za baba kutaka,
Kama hajaeleweka, aweza akafutika,
Watu walivyofyatuka, jambo la kusikitika.

Bora ikaeleweka, watoto mkayashika,
Mali ni kuwajibika, za kurithi ni baraka,
Hizo zisijefanyika, wazazi mkawachoka,
Watu walivyofyatuka, jambo la kusikitika.

Ni kiama kimefika, mambo yanayofanyika,
Mtu mzima kuzika, hajafa kumfunika!
Masikio yanawaka, habari hizi kufika,
Watu walivyofyatuka, jambo la kusikitika.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

ELIMU

**NA JULIETH MKIRERI**

SIKIENI UJUMBE HUU

# Maktaba si vitabu ila maarifa yanayopatikana ndani yake




Kupenda kusoma kunaanzia utotoni, watoto wanapofunzwa kupenda na kufurahia vitabu. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

MAKTABA ni eneo maalumu kwa ajili ya kujipatia maarifa. Ni sehemu ya kujisomea na kujifunzia mambo mbalimbali kuanzia yaliyoko, yajayo na yaliyopita. Ndiko zinakohifadhiwa nyaraka, picha na kila aina ya 'data' ziwe kielektroniki au kianalojia.

Hapo zamani ilikuwa kawaida kuunda maktaba kwenye mahekalu lakini kiasi miaka ilivyokwenda na maendeleo kuongezeka, zilijengwa kwenye nyumba za watawa wa kiume na wakati huo maandiko yote yaliandikwa kwa mkono.

Wakati maktaba hizo zinaanzishwa walikuwapo watu wachache waliojua kusoma na kuandika zama hizo, lakini hali ilianza kubadilika baada ya kuanza uchapishaji wa magazeti. Maktaba zilipata nguvu mpya na kuonekana zaidi wakati huo kutokana na kazi za uandishi na uchapishaji kuhifadhiwa.

Kwa Tanzania, maktaba zilianzishwa na Mwalimu Julius Nyerere, katika ngazi za vijiji kutokana na kuhitaji watu wawe na maarifa mbalimbali ili kufikia azma hiyo ni lazima kujua kusoma na kuandika.

Hata hivyo, maktaba ambazo zilianzishwa ili kuboresha mazingira ya kusoma na ujifunzaji hazikuendelea kwasababu ziliwekezwa mara moja na hazikuwa endelevu.

Juhudi za kutaka watu kupenda kusoma na kujifunza zinaendelezwa na Shirika la Room to Read, linalotekeleza mradi wa maktaba katika mikoa minne ya Morogoro, Pwani, Tanga na Dar es Salam, kwenye halmashauri 10 na shule 337.

Katika Maadhimisho ya Siku ya Usomaji Duniani inayofanyika Septemba 8, Room to Read, inawakutanisha wadau mbalimbali katika kongamano la kujadili namna mambo mbalimbali ya elimu ikiwamo umuhimu wa maktaba shuleni katika dunia ya sasa ya sayansi na teknolojia.

Mkurugenzi Mkazi wa Room to Read Tanzania, Juvenalius Kuruletera, akizungumza katika maadhimisho hayo anasema, inahitajika mikakati zaidi kuitangaza siku ya usomaji kwa kufanya makongamano na kupaza sauti ili siku hiyo muhimu iweze kufahamika kila mahali na watu wahamasike.

Kuruletera, anasema katika kipindi chote cha miaka 11 tangu kuanza shughuli zake nchini yameleta matokeo chanya kwa walengwa moja likiwa ni kuanzisha maktaba ambazo zimewaleta wengi pamoja.

Anaishukuru serikali kwa ushirikiano na shirika hilo kuhakikisha kile walichokilenga kinafikiwa kwa wakati na walengwa wananufaika hasa kwenye mikoa mradi unapotekelezwa.

Mkurugenzi wa Idara ya Ubunifu na Uandaaji wa vifaa kielimu Fixon Mtelesi, anaeleza kuwa siku ya usomaji duniani imekuwa ikiadhimishwa kila Sepemba 8 na kwamba hayo ni matokeo ya tamko la Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (UNESCO) lililotolewa Oktoba 26, 1966.

Anasema, kuanzishwa kwa siku hiyo ni kukumbusha umuhimu wa usomaji kama kigezo muhimu cha kudumisha utu na haki za binadamu na kwamba.

Siku ya Usomaji huangazia ukweli kwamba kuna mamilioni ya watu ambao hawajui kusoma na kuandika hata ambao wamepata elimu rasmi, lakini siku hiyo hujenga uelewa wa pamoja kwenye jamii kuhusu umuhimu wa kufahamu kusoma na kuandika ambao ndiyo msingi wa wa usomaji na ujifunzaji.

Anaeleza kuwa, kujua kusoma na kuandika pekee hakumtoshelezi mwanafunzi kuwa msomaji mahiri mwenye kupenda kujisomea na hivyo anahitaji kupata fursa ya kujisomea vitabu kwenye maktaba ili kukuza stadi za usomaji.

“Hii inamaanisha kwamba mwanafunzi apate vitabu vya hadithi vinavyovutia kupenda kujisomea, pia kusikiliza hadithi kutoka kwa mwalimu ili kujifunza kuiga usomaji fasaha,” anasema Mtelesi.

“Aidha, maktaba hutoa fursa kwa mwanafunzi kusoma mara kwa mara, tena kufanya hivyo kwa hiari na kujisomea kwa kufurahia na hatimaye kuwa msomaji wa kujitegemea na akiwa hivi anapata uwezo mkubwa wa kusoma kwa ufasaha” anabainisha Mtelesi.

Anaeleza kuwa mbali ya jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na mataifa duniani kukuza usomaji bado kuna idadi kubwa ya watu duniani wasiojua kusoma vizuri na wasiokuwa na tabia ya usomaji.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la UNESCO za mwaka 2022 inakadiriwa kuwa watu million 773 hawana stadi za usomaji hivyo kushindwa kusoma kwa ufasaha.

“Tunaomba wadau mbalimbali wa elimu na serikali kutambua umuhimu wa kushiriki katika kuanzisha, kusimamia na kuendeleza maktaba katika shule za msingi ili kuwajengea wanafunzi ari na tabia ya usomaji,” anasisitiza.

Mtelesi, pia anasema makataba hizo pia zinapaswa kuwa rafiki kwa watoto na zenye vitabu bora zilizopangiliwa katika ngazi kulingana na uwezo wa mwanafunzi, hatua ambayo itafanikisha kuwajengea watoto tabia ya usomaji na hivyo kuwa na taifa lenye wasomi wa kujitegemea, wenye maarifa na ubunifu.

Joachim Kahwa, ni Mkurugenzi wa Mradi wa Usomaji na Maktaba wa Shirika la Room to Read, anasema taasisi hiyo inahamasisha uwepo wa maktaba zenye vitabu vya hadithi vyenye kuvutia vinavyopangiliwa kwa ngazi au hatua.

Kahwa, anasema pia limewekeza katika kutoa mafunzo kwa walimu kazini kwenye maeneo wanapotekeleza mradi huo ili kuwajengea stadi za kufundisha na kuandika kwa wakati pia kusimamia uendeshaji wa maktaba na ufundishaji wa vipindi vya maktaba.

“Kupitia mradi wa Room to Read tumeshuhudia mabadiliko chanya kadhaa ikiwamo watoto kupenda kujisomea shuleni na nyumbani, kuwahi kufika shule ili kwenda kuazima vitabu maktaba kupunguza kelele na utoro na kwa ujumla kufanya vizuri kwenye masomo yao,” anaeleza.

Anabainisha kuwa, shirika hilo limeanzisha maktaba mtandaoni ambayo ina vitabu mbalimbali vyenye lugha tofauti ikiwamo Kiswahili hivyo kumpa mtoto fursa ya kujisomea mahali popote pia, kumwepusha na matumizi mabaya ya muda ikiwamo ya kuangalia runinga kwa muda mrefu.

Ofisa Elimu Wilaya ya Ubungo, Joseph Mabeyo, anaeleza kuwa wilaya hiyo ina shule 66 za msingi za serikali na mradi wa maktaba unatekelezwa katika shule 28 na kwa kuanza 21 zitanufaika.

Aidha, anaongeza kuwa hadi sasa shule saba zimepata fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maktaba ya makontena ambayo itakuwa ni fursa kwa wanafunzi kupata sehemu ya kujisomea na kuazima vitabu.

Mabeyo, anatoa rai kwa wazazi wanapojenga nyumba kutenga chumba mahususi kwa ajili ya watoto wao kujisomea pia anawakumbusha walimu kuweka utaratibu wa kusoma hata ukurasa mmoja wa kitabu kwa siku.

Elieshi Lema, ni mmoja wa wadau wa elimu, anayesema kuwa bila kuwa na maktaba mazingira ya kusoma na kujifunzia hayajakamilika na kwamba ili watoto wabadilike, wanahitaji kusoma vitabu ambavyo wanawafahamu wahusika na kiini cha kujua vitu vingi ni kusoma na endapo kutakuwa na makataba nyingi kwenye shule itasaidia wanafunzi kutumia muda wao mwingi kujifunza.

“Maktaba si vitabu bali maarifa yanayopatikana katika vitabu na lazima iwe na vitabu vinavyolenga kukuza ubunifu” anasema akiungwa mkono na mwalimu wa Shule ya Msingi Zirai mkoa wa Tanga Ahmed Sheshe, anayeongeza kuwa uwapo wa maktaba katika shule yao umeleta matokeo chanya na kufanya ongezeko la wanafunzi tofauti na miaka mingine.

## HABARI PICHANI



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, akikagua bidhaa za magendo zilizokamatwa hivi karibuni katika ghala la Mkinga Horohoro. **PICHA: OSCAR ASENGA**



Wakazi wa Kijiji cha Ikongosi Juu, Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa, wakifurahia hati za hakimiliki za kimila zilizotolewa na Taasisi ya Pelum Tanzania na Landesa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi hivi karibuni. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**




Mwanzilishi wa Taasisi ya Gracious Hands, Devother Kimei (kulia), akikabidhi msaada wa madaftari kwa wanafunzi wenye ulemavu katika Shule ya Sekondari Jangwani mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Wengine ni wanachama wa taasisi hiyo. **PICHA: FATUMA ATHUMANI**



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo nchini (TBA), Daud Kandoro, akizungumza na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliotembelea miradi ya ujenzi mbalimbali katika mji wa serikali, jijini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**


### CHEMSHABONGO NA -00 1 00-


Dondoo: Kulia
3. Binadamu
5. alikuwa Rais mweusi Marekani
6. mwendesha mitambo
10.Mji mkuu wa Mali
14.ng'ata kwa meno
15.sehemu ya kwanza ya Biblia
17.cheti 18.miezi 3 anayokaa mwanamke Muislamu aliyeachika
20.mnyama mjanja katika hadithi
21.aina ya kahawa
Chini:
1. Rabat ni mji mkuu
2. Zamani
3. mpinzani mkuu Afrika Kusini
4. kuwa wa awali kufanya jambo
7. kwa taratibu
8. toka chini na kwenda juu
9. mchezo wa kutumia kipande cha mti baina ya timu mbili
10.karatasi inayotiwa barua
11.omba ruhusa ya kuondoka
12.mboji 13.ndege mwenye mkia mrefu 16.Uitaji wa Waislamu kuswali 19.vumbua



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| MAZINGIRA | WALI |
| WAMASAI | IRAN |
| KIANGAZI | AGUA |
| ALAMINA | MNAA |
| KANISANI | AZMA |
| MAZIWA | ASALI |
| PASAKA | AKILI |
| MPAKA | ADAA |
| MMEA | AGUA |
| KAMA | GARI |
| KALILI | ALA |
| AMANI | NIA |
| ASISI | GIA |





maoni: 0755429240





## Wataalamu wa macho wapiga kambi Mbarali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

TIMU ya wataalamu wa macho kutoka Marekani na Watanzania wamepiga kambi kwa zaidi ya wiki moja katika Wilaya ya Mbarali kwa ajili ya kuwafanyia matibabu wananchi wa wilaya hiyo hasa wenye tatizo la mtoto wa jicho.

Aidha, wataalamu hao walifanya msako wa nyumba kwa nyumba katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo kwa ajili ya kuwabaini watu wenye matatizo hayo ili wawafanyie matibabu.

Katika kambi hiyo, zaidi ya wananchi 280, walifanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho huku wengine zaidi ya 400 wakibainika mtaani kuwa wana tatizo hilo.

Meneja wa Mpango wa Taifa wa Huduma ya Macho kutoka katika Wizara ya Afya, Dk. Bernadetha Shilio, alisema tatizo la mtoto wa jicho linawaathiri zaidi watu wazima wenye umri wa zaidi ya miaka 40.

Alisema, tatizo hilo ni kubwa nchini na kwamba huduma hiyo ilikuwa inatolewa kwa wananchi hao bila malipo yoyote kwa maelezo kuwa gharama zinachukuliwa na taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya Hellen Keller.

"Lengo letu hapa ni kuwafikia wananchi 900 ambao wengine wanajitokeza wenyewe na wengine tunawatafuta mitaani kwa sababu baadhi huwa hawajui kuwa wana tatizo," alisema Dk. Shilio.

Mkurugenzi wa Shirika la Hellen Keller, Dk. Deogratius Ngoma, alisema wataendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea kuupanua mradi huo kwa maelezo kuwa awali ulikuwa unatekelezwa kwa Wilaya ya Mbarali pekee.

Alisema waliamua kufanya kambi hiyo katika Wilaya ya Mbarali baada ya kubaini kuwa kulikuwa na tatizo kubwa zaidi kuliko maeneo mengine ya nchi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alilishukuru shirika hilo kwa kuamua kuwasaidia wananchi hao huku akiwataka wananchi kujitokeza kupima ili kama watabainika kuwa na tatizo hilo wapate matibabu.

# Waliochoma bweni waamuriwa kufukuzwa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANAFUNZI waliochoma bweni katika Shule ya Sekondari Mwakaleli, Rungwe mkoani Mbeya, wameendelea kukaliwa kooni baada ya serikali wilayani hapo kuiagiza bodi ya shule hiyo kuwafukuza shule.

Bweni hilo lijulikanalo kwa jina la Mwantimwa, liliungua Septemba 13, mwaka huu na takriban wanafunzi 12 waliokuwa wanalitumia walinusurika huku samani zote na mali za wanafunzi zikiteketea kwa moto.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishana Msaidizi wa Polisi (ACP) Benjamin Kuzaga, moto huo ulizuka saa 1:40 jioni wakati wanafunzi wakiwa madarasani wakijisomea na kwamba chanzo awali kilikuwa hakijulikani.

Alisema baada ya uchunguzi, walibaini kuwa moto huo uliwashwa na mwanafunzi Jacqueline Charles (14), ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule hiyo na kwamba aliwasha moto huo kwa kutumia kiberiti.

Kuzaga, alisema walibaini hilo baada ya kufanya uchunguzi wa kiintelijensia kwa kushirikiana na uongozi wa shule ndipo ikabainika kuwa wakati anawasha moto huo, kulikuwa na mwanafunzi mwingine ambaye alikuwa anaumwa na amelala ndani ya bweni hilo.

"Moto huo uliteketeza kila kitu kilichokuwamo ndani ya bweni hilo. Tumefuatilia tumebaini kwamba hasara iliyotokana na moto huo ni zaidi ya Sh. milioni 52.5 na wanafunzi walipoteza kila kitu isipokuwa nguo ambazo walivaa," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema, kabla ya tukio hilo, mwanafunzi mwingine, Salom Mohamed (15), aliwahi kujaribu kuchoma bweni hilo lakini moto huo ukadhibitiwa kabla haujaleta madhara na kwamba naye anashikiliwa kwa mahojiano zaidi.

Kamanda Kuzaga alisema, awali mwanafunzi aliyeshuhudia tukio la kuchoma moto huo, alikuwa hatoi ushirikiano kwa sababu alikuwa anahofia na kwamba kila mmoja alikuwa amejawa na taharuki.

Juzi, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Rungwe, ilitembelea shule hiyo kuangalia madhara ya moto huo pamoja na kuwafariji wanafunzi hao kutokana na tukio hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, aliagiza Bodi ya Shule hiyo kuwafukuza wanafunzi hao wanaodhaniwa kuhusika na tukio hilo ili liwe fundisho kwa wanafunzi wengine ambao wana tabia za aina hiyo.

Alisema, tukio hilo limesababisha hasara kubwa na limeharibu historia ya shule hiyo kwa kuwa majengo hayo yalijengwa kabla ya uhuru na kwamba kuyachoma ni kuharibu historia.

Dk. Anney, alisema mbali na kufukuzwa shule pia wanafunzi hao watafikishwa mahakamani na kwamba watatakiwa kulijenga upya bweni hilo ili liendelee kutumiwa na wanafunzi ambao kwa sasa wanalala kwenye baadhi ya madarasa.

"Haiwezekani ukapata wendawazimu wako huko uje uchome bweni halafu tukuache. Hata kama hakutumwa na mzazi wake hili bweni itabidi alipe," alisema Anney.

Baadhi ya wazazi wa wanafunzi wanaosoma kwenye shule hiyo walipatwa na taharuki baada ya kusikia taarifa ya bweni hilo kuungua na walikuwa wanahofia usalama wa watoto wao.

Mmoja wa wazazi hao, Martha Nzowa, alisema walitumiwa taarifa na Mkuu wa Shule hiyo, hivyo wakaamua kwenda kuangalia madhara yaliyotokea na kwamba walikuta watoto wako salama ila vitu vyao vimeteketea.

Aliiomba serikali na wadau mbalimbali kuwasaidia watoto wao vifaa ili waendelee na masomo na akaiomba serikali isiwarudishe watoto hao nyumbani kwa maelezo kuwa wengine wanaelekea kwenye mitihani.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, akijaribu kutumia mashine za kupimia macho ambazo wataalamu wa macho kutoka Marekani walipiga kambi wilayani humo kwa ajili ya kuwafanyia upasuaji wa mtoto wa jicho. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima 120,000 wasajiliwa mfumo kidijitali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imesajili zaidi ya wakulima 120,000 kwenye mfumo wa kidijitali ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuboresha huduma za ugani kwa wakulima hao.

Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Michael Sanga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa tathmini ya uandikishaji wa wakulima pamoja na usajili wa wakulima.

Alisema, wakulima hao wanasajiliwa kwa ajili ya kunufaika na mbolea za ruzuku zinazotolewa na serikali kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023 ambazo zimeanza kutolewa.

Sanga alisema, mpaka sasa mkoa wa Mbeya ndio unaoongoza nchini kwa usajili wa wakulima kwenye mfumo na kwamba kuna matatizo madogo madogo ambayo yanafanya kazi hiyo isifanikiwe kwa asilimia 100 na kwamba wanaendelea kukabiliana nayo.

Alisema moja ya matatizo ambayo huwa yanaibuka ni tatizo la mtandao kwa kuwa serikali iliingia mkataba na moja ya mitandao mikubwa ya simu kwa ajili ya kuratibu kazi hiyo lakini matatizo mengi yanaibuka.

"Tunaendelea kuwaandikisha wakulima hawa katika maeneo yote ya mkoa wetu, tunawasajili wakulima hawa ili wanufaike na mbolea ya ruzuku ambayo inatolewa na serikali," alisema Sanga. Alisema kazi ya kuwasajili wakulima linaendelea kwa viongozi wa serikali za mitaa na kwamba viongozi wa TFRA, wanafuatilia kwa ukaribu ili kuhakikisha majina yote yanaingizwa kwenye mfumo.

Kabla ya kuanza kuwasajili, alisema wakulima hao walianza kwanza kuwasajili mawakala wa usambazaji wa mbolea na kwamba zoezi hilo lilishakamilika na kwa sasa wanaendelea kuhamasisha wakulima kujiandikisha

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliagiza matatizo yote yaliyoibuka kwenye uandikishaji wa wakulima yanatatuliwa mapema kwa kuwa msimu wa kilimo haujaanza ili wakulima waendane na msimu.

Aliitaka TFRA, kuwashirikisha wakurugenzi wa halmashauri na maofisa kilimo ili wahamasishe uandikishaji wa wakulima katika maeneo yao na kuhakikisha kazi hiyo inakwenda vizuri.

Vilevile, aliitaka mamlaka hiyo kuweka mawakala wilayani ambao watakuwa wanawasajili wakulima ili kuhakikisha zoezi hilo linafanyika kwa mafanikio zaidi.

"Nawapongeza kwa kuongoza kusajili wakulima nchini lakini mimi binafsi nawashauri muongeze juhudi, mkoa wetu ni miongoni mwa mikoa ambayo inazalisha sana mazao ya kilimo kwahiyo lazima tuwe makini kwenye uandikishaji," alisema Homera.

Baadhi ya viongozi wa serikali na wa dini walioshiriki kwenye kikao hicho cha tathimini walishauri zoezi hilo liwe endelevu na liwekewe mikakati mizuri ili wakulima wote waandikishwe.

Mmoja wa viongozi wa dini, Prof. Donard Mwanjoka alisema zoezi hilo lina kasoro ndogo ambazo zinaweza zikakwamisha zoezi hilo ikiwamo wakulima kutakiwa kujiandikisha kwenye maeneo ambayo mashamba yao yapo tofauti na wanakoishi.



# Wajasiriamali waipa 5 serikali kwa usikivu malalamiko tozo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAJASIRIAMALI mkoani Dodoma, wameipongeza serikali kwa kusikia kilio cha wananchi dhidi ya ongezeko la tozo za kielektroniki katika miamala ya mitandao ya simu na benki.

Septemba 12, mwaka huu Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, akiwa wilayani Tarime, alisema kuwa amepokea maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, na Chama Cha Mapinduzi (CCM), kushughulikia malalamiko ya wananchi yaliyojitokeza kuhusu gharama za tozo hizo ili kuleta unafuu.

Katika hotuba yake Nchemba, alisema wataalamu wa wizara yake wanayafanyia kazi maelekezo mbalimbali yaliyotolewa pamoja na maoni ya wananchi kuhusu jambo hilo.

Alisema, baada ya muda mfupi serikali itakuja na majawabu ya kufanya marekebisho kadhaa ili kuleta unafuu kwa wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu wa Wajasiriamali Mkoa wa Dodoma, Christopher Dioniz, alipongeza serikali kwa kusikia kilio hicho cha wananchi.

Alisema, makato ya tozo katika miamala ya simu na benki ilikuwa kikwazo kikubwa kwenye bishara zao pale wanapotuma na kupokea fedha.

“Wajasiriamali tunafanya miamala mara nyingi sana katika shughuli zetu za kila siku tunatuma fedha kwa ajili ya kuagiza bidhaa mbalimbali, hivyo makato ya tozo hizi ilikuwa mwiba mkali kwetu,”alisema Dioniz.

Alisema endapo serikali itafanikiwa kupunguza tozo hizo kama ambavyo imeahidi wajasirimali itawasaidia kuendesha shughuli zao bila malalamiko.

“Makato yaliyopo hivi sasa yanachangia kwa kiasi kikubwa hata wakati mwingine kukata mitaji ya wafanyabiashara kwani kiasi kikubwa cha fedha kikikatwa kama tozo hali ambayo inatulazimu kufanya kazi kwa hasara,”alisema.

Kadhalika, alisema hivi sasa wanalazimika kutembea na fedha nyingi mkononi hali ambayo ni hatari kwa usalama wa Maisha yao.

“Ile hali ya zamani ya watu kutembea na fedha taslimu au kuficha ndani ya nyumba chini ya godoro inataka kurejea tena kutokana na hili ongezeko la tozo la miamala ya simu na benki,”alisema.

Hivyo aliiomba serikali kubuni vyanzo vingine vya mapato ambavyo vitakuwa endelevu na visivyo athiri maisha ya kila siku ya wananchi wanyonge.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (katikati), akikata utepe kwa ajili ya uzinduzi wa vifaa vya kuchonga barabara vilivyonunuliwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma jana, wengine ni Mbunge wa jimbo hilo, Anthony Mavunde (wa pili kulia), Naibu Meya wa Jiji, Jamali Ngaliya (kulia nyuma), na Mkurugenzi wa Jiji, Joseph Mafuru (wa tatu kushoto). **PICHA PETER MKWAVILA**

# H’shauri yaagizwa kutumia mitambo utatuzi migogoro

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kutumia mitambo ya kisasa kutatua kero ya migogoro ya mipaka ya viwanja kwa wananchi.

Alisema, wakazi wengi Jijini Dodoma bado wamekuwa wakiingia kwenye migogoro na Halmashauri ya Jiji kutokana na kutotambua mipaka ya barabara na viwanja vyao.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo kwenye uzinduzi wa mitambo mipya ya kuchonga barabara iliyonunuliwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.8

Alisema, kununuliwa kwa mitambo hiyo ni imani yake kuwa itaimarisha miundombinu iliyopo katika Jiji hilo na kupunguza kero ya migogoro ya mipaka baina ya wananchi na Jiji hilo.

“Bado kuna mitaa mingi iliyopo ndani ya kata nyingi za Jiji hili, hakuna barabara zilizochongwa, hivyo mitambo hiyo sasa ikatumike kufungua barabara ili kuondoa migogoro ya wananchi ambao wameshindwa kutambua mipaka yao hadi sasa,”alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema kuwa halmashauri yake sasa inaenda kuongeza mapato zaidi kupitia mitambo hiyo.

Mafuru, alisema pamoja na kuongeza mapato halmashauri sasa inaenda kufungua barabara za mitaa katika kata nyingi zilizopo ambazo zimekuwa na migogoro kutokana na ukosefu wa alama za mipaka yake.

“Baadhi ya kata hizo ni Ndachi, Mnadani, Michese, Lugala, Ng’ong’ona, Mkonze, Makutopora, Vyeyula, Zuzu, Mbwanga, Iyumbu na kata zingine zilizopo ndani ya Jiji ambazo kuna kilio kikubwa cha kukosa barabara za mitaa,”alisema Shekimweri.

Mbunge wa Dodoma, Athony Mavunde, alisema kuwapo kwa mitambo hiyo kutaleta mapinduzi makubwa ya kulifanya Jiji la Dodoma kujengeka kutokana na kuwekwa kwa mipaka kiurahisi.

Alisema, kuwapo kwa mipaka ya barabara kwenye mitaa mbalimbali katika Jiji la Dodoma kutawasaidia wananchi wa maeneo mengi kuendelea na shughuli mbalimbali za ujenzi na matumizi mengineyo.

## Upatikanaji majisafi, salama kwapunguza magonjwa mlipuko

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

IMEELEZWA kwamba, kufanyika kwa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira, kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaopata huduma ya majisafi na salama pamoja na wananchi kunawa mikono kwa maji tiririka kumetajwa kuwa chanzo cha kupungua kwa magonjwa ya mlipuko.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Saitore Laizer, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji awamu ya Tatu (WSDP III), unaogharimu Dola za Marekani bilioni 6.5.

Alisema, tangu kuanza kwa programu hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza magonjwa ya mlipuko, kuongeza usafi katika maeneo ya umma na kuimarisha afya ya Watanzania.

Alisema, vituo vipya vya afya 1,534 vimefikiwa na huduma ya maji ikiwamo vyumba vya kujifungulia kinamama kuwa na maji jambo ambalo litasaidia kupunguza maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa kujifungua na hivyo kupunguza vifo vya watoto wachanga.

Alisema kuwa, katika mpango wa tatu wa programu ya maji wanategemea kuimarika kwa afya ya jamii kwamba kila kaya ifikapo mwaka 2025 iwe na choo bora.

“Tunategemea vituo vipya 3,500 kufikiwa na huduma ya maji hasa vijijini, kuongeza usafi katika maeneo ya umma, magulio, masoko, tuko tayari kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa tatu,” alisema.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa James Mdoe, alisema wamekuwa wadau muhimu katika programu hiyo kwa kujenga vyoo bora, vifaa vya kunawia mikono kwa shule za msingi na sekondari.

Alisema kuwa, katika utekelezaji wa programu hiyo awamu ya pili waliweza kuhudumia shule za msingi 3,046, shule za sekondari 716.

Profesa Mdoe, alisema katika awamu ya tatu wamepanga kuzifikia shule za msingi 2,500 na sekondari 1,400, pia kujenga vyoo bora, upatikanaji maji na vifaa bora vya kunawia mikono.

Mkuu wa Kitengo cha Uratibu Wizara ya Maji, Remigius Mazigwa, alisema kuwa maabara nyingi za maji zimepata ithibati.

Alisema, utekelezaji wa mpango wa pili ulikuwa na matatizo ikiwamo kupungua kwa rasilimali maji kutokana na mito mingi kukauka kulikochangiwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Mwakilishi wa wadau wa maendeleo kutoka Benki ya Dunia (WB), Ruth Walker, aliipongeza serikali kwa jitihada ilizofanya kuhakikisha matatizo ya upatikanaji wa majisafi na salama unapatiwa ufumbuzi.

Alisema WB, iko tayari kuendeleza ushirikiano huo ili kuhakikisha matatizo ya upatikanaji wa majisafi na salama unapatiwa ufumbuzi.

## Bilioni 92/- kujenga mji wa kisasa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar inatarajia kujenga mji mpya wa kisasa ambao utagharimu Sh. bilioni 92 na tayari imeshatenga fedha hizo kwa ajili ya mradi huo.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alibainisha hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi alipotoa ufafanuzi kuhusu mpango huo wa ujenzi wa mji mpya wa serikali.

Alisema lengo la serikali ni kuwa na maeneo yake ambayo yatatumika kwa ajili ya majengo ya ofisi za serikali, hatua ambayo alisema itaongeza ufanisi wa kazi na uwajibikaji.

Waziri huyo alisema juhudi hizo zimeanza kuchukuliwa ambapo majengo mengi ya ofisi za serikali yaliyoko Mji Mkongwe 'yamehama hatua kwa hatua' huku ofisi mpya za serikali zikijengwa katika maeneo tofauti ikiwamo Tunguu na Mazizini.

Alisema hatua hizo pia zimechukuliwa kwa upande wa Kisiwa cha Pemba ambapo ujenzi wa ofisi za serikali umefanyika huko Gombani.

"Tumeanza mpango wa ujenzi wa ofisi za serikali Gombani ambapo jumla ya wizara nne zimekuwa zikitumia majengo yaliyopo huko," alisema.

**Alisema lengo la serikali ni kuwa na maeneo yake ambayo yatatumika kwa ajili ya majengo ya ofisi za serikali, hatua ambayo alisema itaongeza ufanisi wa kazi na uwajibikaji**

# Waziri afafanua tozo uagizaji bidhaa za nje

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Salum Mkuya, amesema mfanyabiashara anapoagiza biadhaa kutoka nje ya nchi, anawajibika kuwasilisha maelezo sahihi ya bidhaa zake katika mfumo wa TANCIS wa Mamlaka ya Mapato (TRA).

Alibainisha hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakihi, aliyetaka kujua kauli ya serikali kuhusu malalamiko ya wafanyabiashara ya utozwaji wa kodi katika uagizaji huo wa bidhaa.

Alisema maelezo hayo yanapaswa kuonyesha aina ya bidhaa aliyoingiza nchini pamoja na thamani halisi ya bidhaa hizo katika utaratibu wa CIF (Cost, Insurance and Freight).

Alisema aina ya bidhaa na thamani yake ndiyo inayotumika kutoa kodi sahihi inayopaswa kulipwa serikalini kwa bidhaa zinapoingia nchini.

Alisema kuwa kwa baadhi ya bidhaa kumewekwa bei maalum ambayo inatumika kutoza ushuru baada ya kutumia bei halisi iliyo katika soko.

"Hii ni katika kudhibiti bei ya bidhaa hizo kwa mtumiaji wa mwisho (mwananchi) na pia kupambana na ukwepaji wa kodi," alisema.

Waziri huyo alisema bidhaa ambazo zimewekwa bei maalum wakati wa uingizaji nchini ni mchele, sukari, unga wa ngano, mafuta ya kupikia na saruji.

Alisema kwa bidhaa hizo thamani inayotumika kutoza kodi za forodha na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ni ile iliyowekwa na serikali baada ya thamani halisi ya kununulia bidhaa nje ya nchi.

Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa jedwali la pili la sheria ya VAT ya mwaka 1998, bidhaa za mchele na unga wa ngano ni bidhaa zilizosamehewa kodi hiyo, hivyo hazitozwi kodi hiyo wakati wa uingizaji nchini na wakati zinapouzwa katika soko la ndani.



Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakifuatilia kikao cha baraza hilo kinachoendelea Chukwani Zanzibar jana.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ACT- Wazalendo yapewa mbinu kujijenga

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka wanachama wa chama hicho kutokata tamaa na badala yake waendelee kushikamana katika jitihada za kukijenga chama chao.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alitoa kauli hiyo jana katika Jimbo la Mpendae mjini Unguja alipozungumza na viongozi na wanachama wa jimbo hilo akiwa kwenye ziara yake ya ujenzi wa chama.

Aliwahimiza wanachama hao kudumisha umoja na mshikamano, akisisitiza ni silaha muhimu katika kuendeleza jitihada za kufikia malengo ya chama hicho hatua kwa hatua.

Aliwataka wanachama, hasa vijana, kutumia maarifa na juhudi katika kuendeleza jitihada za kujenga chama hicho kwa kuwajibika ipasavyo katika masuala na majukumu mbalimbali ya kukijenga chama hicho.

Othman alisema suala la umoja ndiyo njia pekee ya kufanya chama hicho kusonga mbele na kwamba ni vyema kuwaunga mkono wale wote wanaojitolea kusukuma mbele jitihada za kujenga chama badala ya kuwavunja moyo.

Alisema kuwa moja ya malengo ya chama hicho ni kuhakikisha Zanzibar inaondosha kero mbalimbali zinazojitokeza wakati wa uchaguzi kwa kuwa na uchaguzi huru na haki ambao utasaidia kujenga mustakabali mpya wa Zanzibar.

Aliwataka wanachama kuwa wakweli wenye dhamira na lengo moja kwa kuwa huo ndio mwongozo wa chama hicho katika kufikia utekelezaji wa masuala mbalimbali ya ujenzi wa chama na taifa.

Akizungumzia Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Othman alisema chama hicho kinaendelea kuwajibika ndani ya serikali kwa kutekeleza majukumu yake kiliyopewa kwa ufanisi mkubwa kwa dhamira ya kusaidia ujenzi wa nchi.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, aliwataka vijana kuungana na kuwa kitu kimoja kuendelea kukiunga mkono chama hicho ili kitimize malengo ya kusaidia ujenzi wa Zanzibar mpya.



# Huduma za upasuaji kwa wajawazito zaboreshwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MGANGA Mkuu Manispaa ya Shinyanga, Dk. Elisha Robert, amesema huduma za wajawazito katika kituo cha Kambarage, zimeboreshwa ili wajifungue salama na kuondoa au kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Akizungumza na Nipashe mjini hapo, alisema serikali imeamua kuboresha huduma kutokana na kuwapo idadi kubwa ya wajawazito wanaohitaji kuhudumiwa.

"Ndani ya mwezi mmoja wajawazito ambao hujifungua kwenye kituo hiki cha afya Kambarage hufika hadi 340, na baada ya kuboresha huduma hii ya upasuaji vifo vya uzazi vimepungua kutoka vifo 24 mwaka 2020 na mwaka 2021 hadi 11, mwaka 2022 hadi sasa tuna vifo sita tu tukitarajia kuvimaliza kabisa kutokana na uboreshaji huu," alisema Dk. Robert.

Aidha, alitoa wito kwa wajawazito kujenga tabia ya kuhudhuria kliniki mara kwa mara kupata taarifa ya maendeleo ya mtoto na kujifungulia kwenye vituo vya afya ili kusiwapo kabisa vifo vya uzazi, kutokana na huduma za afya kuboreshwa na vifaa tiba kuwapo vya kutosha.

Katika hatua nyingine, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha na kuboresha huduma za afya nchini ili kuimarisha afya za wananchi, ikiwamo ujenzi wa kituo kipya cha afya Ihapa Kata ya Oldshinyanga kilichorahisisha upatikanaji wa huduma za afya.

Mmoja wa wakazi wa Manispaa ya Shinyanga, Therezia Gaspal, aliishukuru serikali kwa kuboresha huduma za afya hasa za uzazi na kuwaondolea mateso wanawake.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (katikati), akizindua vitabu vitatu vya mikakati ya kuboresha elimu katika Manispaa ya Shinyanga mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko na Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Getrude Gisema. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Hatimaye Itilima kufurahia majisafi na salama

**Na Happy Severine,** ITILIMA

ZAIDI ya wananchi 8,000 wa Kata za Budalabujiga na Mwalushu wilayani Itilima, mkoani Simiyu, wataanza kunufaika na majisafi na salama baada ya miradi ya visima viwili virefu kukamilika.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Itilima, Fredy Hussein, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema mradi mmoja unatekelezwa katika kata ya Budalabujiga na una thamani ya Sh. milioni 335, huku wa Mwalushu utagharimu Sh. milioni 339.

Vile vile, zaidi ya wananchi 3,471 watahudumiwa na mradi huo utakapokamilika Septemba, mwaka huu.

Holo Martin, mkazi wa Kata ya Budalabujiga, alishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kutatua adha ya maji katika kata hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda, akizungumza wakati wa uwekaji jiwe la msingi aliipongeza RUWASA kwa utekelezaji mzuri huku akionesha kuridhishwa na kazi hiyo.

Alisema mchango mkubwa wa serikali katika kuwaletea wananchi miradi ya maendeleo unalenga kuboresha huduma zao na kwa mwaka mmoja Wilaya ya Itilima pekee imepewa zaidi ya Shilingi bilioni tano.

Aliwataka wananchi hao kutunza miradi hiyo ili iwasaidie kwa kipindi kirefu.

**Holo Martin, mkazi wa Kata ya Budalabujiga, alishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kutatua adha ya maji katika kata hiyo.**

# Wataka majengo ya shule kuzingatia wenye ulemavu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWENYEKITI wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Wilaya ya Kahama, Marco Nkanjiwa, amewataka wananchi na viongozi wanaojenga miundombinu ya shule kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, alisema kundi hilo linahitaji kupata elimu nzuri lakini linakumbana na changamoto nyingi, ikiwamo za miundombinu isiyo rafiki.

Nkanjiwa alisema ni muhimu jamii kutambua uwapo wa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali na kuzingatia ujenzi wa miundombinu utakaowasaidia wapate huduma zote muhimu kama wengine.

Alisema kukosekana kwa miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu shuleni kunasababisha kundi hilo kukosa masomo na kutimiza ndoto zao na wengine kuona wanadhalilika wanapobebwa na wanafunzi wenzao kuingia darasani au kuacha masomo yao.

Kwa mujibu wa Nkanjiwa, vyumba vya madarasa vilivyojengwa miaka ya nyuma havina miundobinu rafiki kwa wenye ulemavu, ikilinganishwa na madarasa yaliyojengwa hivi karibuni, jambo ambalo linapaswa kuboreshwa ili elimu iwe shirikishi. Alitaja baadhi ya shule zenye miundombinu rafiki kuwa ni shule za msingi Majengo, Kahama na Bulige, pia Shule ya Sekondari Mama Samia na shule za sekondari mpya zilizojengwa na fedha za UVIKO-19 na kuwataka wananchi wanapoanzisha ujenzi kuzingatia makundi hayo.

"Utoro kwa wanafunzi wenye ulemavu husababishwa na ukosefu wa miundombinu rafiki juu yao, madarasa na vyoo wanavyotumia hayana mazingira mazuri na badala yake akijitahidi kwenda shuleni wanaambulia kupata magonjwa ya mlipuko wanapotumia vyoo," alisema Nkanjiwa.

Ofisa Elimu wa Shule za Msingi Manispaa ya Kahama, Hamida Kaganda, alisema kila wanapoanzisha ujenzi wa vyumba vya madarasa huwa wanazingatia mazingira rafiki ya wanafunzi wenye ulemavu na kuhakikisha wote wanahitimu elimu bila kupata tatizo.

Alisema shule zote zilizopo kuna jumla ya madarasa 273 yenye miundombinu rafiki ya wanafunzi wenye ulemavu na kwamba ni muhimu wazazi na walezi wanapoanzisha ujenzi wanawashirikisha kuhakikisha wanatengeneza mazingira hayo lengo likiwa kutimiza ndoto zao.

## HABARI KIMATAIFA

# Rais Samia ashiriki mazishi ya Malkia

**LONDON,** Uingereza

VIONGOZI wa ulimwenguni akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan wamekusanyika kwenye kanisa la Westminster Abbey mjini London kushiriki ibada ya mazishi ya Malkia Elizabeth II aliyeaga dunia wiki mbili zilizopita.

Rais Samia, William Ruto wa Kenya na Joe Biden wa Marekani ni miongoni mwa wakuu wa nchi walioshiriki ibada hiyo ya mazishi ya kitaifa ya Malkia Elizabeth yaliyofanyika jana katika Kasri la Windsor London, Uingereza.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na DW, Jeneza la Malkia Elizabeth II liliondoka katika ukumbi wa bunge wa Westminster likiwa limebebwa na askari kuelekea Westminster Abbey.

Jeneza hilo liliwekwa katika ukumbi huo tangu Jumatano ya wiki iliyopita na kutoa fursa kwa maelfu ya waombolezaji kutoa heshima zao za mwisho kwa Malkia huyo.

**Mazishi hayo pia yalionyeshwa moja kwa moja na mataifa takriban 200 ulimwenguni kote.**

Nchini Ujerumani bendera kwenye majengo ya umma zilipepea nusu mlingoti ikiashiria kuungana na Waingereza katika wakati huo mgumu wa mazishi ya kitaifa ya Malkia wao yaliyofanyika London.

Marais, wafalme, mawaziri wakuu wa mataifa mbalimbali pamoja na watu takriban milioni moja walikuwa kandokando ya barabara za mji wa London kwa ajili ya kutoa heshima zao za mwisho kwa Malkia huyo ambaye alikalia kiti cha enzi kwa miaka 70.

Mazishi hayo pia yalionyeshwa moja kwa moja na mataifa takriban 200 ulimwenguni kote, huku maofisa wa polisi wakionekana katika opereshení muhimu ya kuimarisha hali ya usalama.

Kabla ya mazishi ya kiongozi huyo aliohudumu kwa kipindi kirefu zaidi, Mfalme Charles III alitoa ujumbe wa shukrani kwa watu nchini Uingereza na dunia kwa ujumla wake akisema yeye na mkewe Camilla wamefarijika kutokana na idadi kubwa ya watu ambao wamejitokeza kwa ajili ya kutoa heshima zao za mwisho kwa Malkia.

"Wakati tunapojiandaa kutoa heshima zetu za mwisho, nachukua fursa hii kusema ahsante kwa watu wote wasioweza kuhesabika ambao wamekuwa faraja na msaada kwa familia yangu na mimi mwenyewe katika kipindi hiki cha majonzi," alisema.

Katika mazishi, jeneza la Malkia Elizabeth lilibebwa kutoka ukumbi wa Westminster, kuelekea Westminster Abbey, kwenye gari ambalo lilitumika kubeba majeneza ya viongozi wengine wa taifa hilo akiwamo Edward VII, George V na George VI, pamoja na aliyekuwa waziri mkuu wa zamani wa taifa hilo Winston Churchill.

Katika ibada iliyofanyika Gothic Medieval Abbey sehemu ambayo Malkia Elizabeth alifunga ndoa na mume wake mwanamfalme Philip mwaka 1947 na kutawazwa mwaka 1953 ilihudhuriwa na watu takriban 2000 wakiwa ni pamoja na viongozi wa dunia, na wahudumu wa afya.

Mamlaka ya mji wa London ilisema maeneo yote ya umma ambayo jeneza la Malkia lilipita yalifurika watu kwa ajili ya kutoa heshima zao za mwisho. **DW**

# Azimio yawakingia kifua makamishna wanne IEBC

**NAIROBI,** Kenya

UONGOZI wa Muungano wa Azimio la Umoja One Kenya umemwonya Rais William Ruto kuhusu mpango unaodaiwa wa kuwatimua makamishna wanne wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) waliojitenga na matokeo ya uchaguzi wa urais wa Agosti 9.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na TKN, kinara mwenza wa Azimio Kalonzo Musyoka alidai Rais Ruto na kikosi chake cha Kenya Kwanza wanania ya kumwondoa naibu mwenyekiti wa IEBC Juliana Cherera na makamishna wenzake Justus Nyang'aya, Irene Masit na Francis Wanderi.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo wa Chama cha Wiper, muungano wa Azimio utafanya kila juhudi kuwalinda makamishna hao, na kwamba Kenya Kwanza wanastahili kuacha kuwawinda.

"Tunakemea vikali hatua hii ya kuwawinda na kuwataka Rais na mawakala wake kuwaacha makamishna hao, kwa upande wetu tunajitolea kuwalinda maofisa hao dhidi ya juhudi zozote za kukiuka haki zao," alisema Kalonzo.

Aidha, inaelezwa kuwa mustakabali wa makamishna hao wanne haujulikani baada ya Chama cha Farmers chenye ukaribu na muungano wa Kenya Kwanza kuwasilisha ombi bungeni kikitaka wanne hao kutimuliwa ofisini.

Chama hicho kinachoongozwa na Irungu Nyakera kiliwatuhumu wanne hao kwa matumizi mabaya ya ofisi yao.

Katika hati ya kiapo iliyowasilishwa bungeni, Farmers Party kinadai kuwa Cherera na wenzake hawafai kushikilia ofisi hizo kwa kuwa walilenga kuhujumu uamuzi wa Wakenya. **KTN**



Askari wakibeba jeneza lililokuwa na mwili wa Malkia Elizabeth II, kuelekea Westminster, mjini London kwa mazishi. **PICHA: MTANDAO**

# Zelenksy, mapambano yataendelea

**IZIUM,** Ukraine

RAIS wa Ukraine, Volodymir Zelenksy, amesisitiza kwamba mapambano yataendelea ili kuyakomboa maeneo yaliyotekwa na Russia, huku ikiripotiwa kuwa wanajeshi wake wamesonga mbele hadi katika ufukwe wa mashariki wa mto Oskil.



Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa jana na DW, wanajeshi wa Ukraine walitishia vikosi vya Russia vinavyoshikilia eneo la Donbas, huku ikibainishwa kuwa zaidi ya miili 400 inafukuliwa kutoka kwenye makaburi nje ya mji wa Izium.

Inaelezwa kuwa katika msitu kwenye eneo lililokombolewa hivi karibuni la Izium, wataalamu wa kupima maiti wa Ukraine wanafukua miili iliyozikwa kwenye makaburi ya halaiki wakati majeshi ya Russia yalipokuwa yameshikilia maeneo hayo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa miili kadhaa tayari imeopolewa na kuhamishwa hadi katika chumba cha kuhifadhia maiti kwa uchunguzi zaidi, huku matokeo ya tathmini ya awali yakiashiria kuwa maiti nyingi zinaonyesha dalili za mateso.

Pia wataalamu wa uchunguzi wa maiti akiwamo Andreiy Sergienko waliomba msaada wa maofisa wa zimamoto kufukua mabaki ya maiti za binadamu.

"Kazi yangu ni kufukua miili kabla wataalamu wa uchunguzi kubaini kilichotokea, baadaye tunaziweka maiti kwenye mifuko na kuzisafirisha hadi katika vyumba vya kuhifadhia maiti," alisema na kuongeza;

"Hiki ni kipindi kigumu cha kutisha katika maisha yangu, na ni kwa mara ya kwanza kupitia uzoefu huu katika miaka yangu mitano ya kufanya kazi, kisaikolojia nadhani tutahitaji msaada siku za usoni kwasababu picha hizi zitakuwa katika fikra zetu milele," alisema Andreiy.

Aliongeza kuwa makaburi hayo hayana majina isipokuwa namba tu, na kwamba jumla ya watu 418 walizikwa katika eneo hilo.

Aidha, kutokana na idadi ya maiti zinazofukuliwa baadhi ya wataalamu wanatoa tathmini zao ambazo zinanakiliwa na maofisa wa polisi, ikielezwa kuwa kumetawala kimya cha kutisha msituni, huku zikisikika sauti za nzi wanaofuata maiti. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATHIAS CONSTANTINE RWEGASIRA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA COROLLA** yenye usajili namba **T863 AYL,** CHASSIS NAMBA: **AE1000305767,** ENGINE NAMBA: **5AH387275.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **KW/RB/4220/2022**

---

FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 676 OF 2022
In the matter of the Estate of the late.........
NEHEMIA THOMAS KIBWANA
And
In the matter of Application for letters of Administration by............
ELIZABETH RAYMOND NKONDOKAYA

**GENERAL CITATION**
(Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above name deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 3RD day of OCTOBER 2022

**Dated at DAR ES SALAAM this 15th day of SEPTEMBER 2022**

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DIODORIUS B. DIDIMUS** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 711 CBY.** Chassis namba **MD625AF42J1K73763.** Engine namba **DF4KJ1X72445.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Control No: **9910834327715.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LEO PLASTICS LTD** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **MC 744 AHX.** Chassis namba **KEFKE7T0302586.** Engine namba **LC157FMIJE298133.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/370630/2022.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA BARAZA LA ARDHI TABORA
Maombi ya Ardhi namba 27 ya mwaka 2022
Muombaji
Fungwe Mbasa kwa niaba ya Marehemu Fugwe Shija
Dhidi ya
Mahona Manweki Ntuzu kwa niaba ya Marehemu Manweki Ntuzu –Mjibu Maombi

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi unaarifiwa kuwa shauri husika hapo juu litatajwa katika Baraza la ardhi Tabora tarehe 2/11/2022 saa 3;oo asubuhi, mbele ya Mheshimiwa Jaji X .A. Bahati.
Nb; unatakiwa kuhudhulia Mahakamani tarehe tajwa bila ya kukosa
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na kupigwa chapa ya Mahakama leo tarehe 15/9/2022

Naibu Msajili
Mahakama kuu Tanzania Tabora

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA BARAZA LA ARDHI TABORA
Maombi ya Ardhi namba 27 ya mwaka 2022
Muombaji
Fungwe Mbasa kwa niaba ya Marehemu Fugwe Shija
Dhidi ya
Goi Manweki Ntuzu –Mjibu Maombi

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi unaarifiwa kuwa shauri husika hapo juu litatajwa katika Baraza la ardhi Tabora tarehe 2/11/2022 saa 3;oo asubuhi, mbele ya Mheshimiwa Jaji X .A. Bahati.
Nb; unatakiwa kuhudhulia mahakamani tarehe tajwa bila ya kukosa
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama tarehe leo 15/9/2022

Naibu Msajili
Mahakama kuu Tanzania Tabora

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA RUNGWE
KITUO CHA KIWIRA
SHAURI LA NDOA NA: 25/2022
EMANUEL MBONEA................MDAI
DHIDI YA
MAGDALENA UGALIMO.............MDAIWA

**HATI YA KUITWA SHAURINI**

Mdaiwa **MAGDALENA UGALIMO** popote ulipo unaamriwa uhudhurie Mahakamani tarehe 30/09/2022 saa tatu asubuhi bila kukosa. Ieleweke kuwa usipohudhuria siku hiyo shauri hilo linaweza kusikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa pasipo uwepo wako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 31/08/2022.

Ibrahim Nganico Nganiko
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO KIWIRA

---

FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 800 OF 2022
In the matter of the Estate of the late.........
MONICA GAITAN SIGALLA
And
In the matter of Application for letters of Administration by......
IVENOFU AMANYILE MAHALI

**GENERAL CITATION**
(Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above name deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20th day of Oct 2022

**Dated at DAR ES SALAAM this 16th day of Sept 2022**

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RAJABU LUPIMO MADALALI** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA PIKIPIKI AINA YA SANLG YENYE NAMBA ZA USAJILI **T. 933** BUZ, CHASSIS NAMBA **LBRSPJB59B9009244**, ENGINE NAMBA: **SL157FMI11933501** RED IN COLOUR. KWAYEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. POLISI TAARIFA: **NYR/RB/349/2021** AU APIGE SIMU NAMBA:**0743824387.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
Anuani ya simu:"WARAKA" Ofisi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W)
S.L.P. 5058
Simu 212009 TANGA
Telefax 2124576
(Makao makuu)

Simu 027-2642622-(Tanga) 09/9/2022
YAH:SHAURI NAMBA.35 LA 2021
ALIASGAR AKBARALI BADRI.................MDAI
DHIDI YA
ABDALLAH THARIA................WADAIWA

**KWA: ABDALLAH THARIA – POPOTE ULIPO**

**ALIASGAR AKBARALI BADRI,** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga. Shauri husika limepangwa kutajwa tar 22/9/2022 saa Tatu kamili asubuhi (3:00). Hivyo basi, unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tar ya Tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba(W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na Hukumu kutolewa dhidi yako.
AMRI hii imetolewa na kutiwa Saini Muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 9/9/20202

MWENYEKITI
BARAZA La ARDHI NA NYUMBA ( W)
TANGA

---

## NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED
## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

M/MWANZO MWANZA MJINI - SHAURI LA TALAKA Na. 103/2021
GIDION SILAS MKUSU _______MDAI
DHIDI YA
CHRISTINA LISAS SANGO _____MDAIWA

M/MWANZO ILEMELA - SHAURI LA TALAKA Na. 01/2014
LEVINA UPENDO MFUTAKAMBA _______MDAI
DHIDI YA
LIMBU BAGASA ___MDAIWA

M/MWANZO BUPANDWA – SHAURI LA MADAI Na. 32/2021
DANIEL DEUS MHAYA _______MDAI
DHIDI YA
EMMANUEL MAGANIKO_______MDAIWA

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA, MAHAKAMA YA MWANZO MWANZA MJINI, MAHAKAMA YA MWANZO MKUYUNI NA MAHAKAMA YA MWANZO SENGEREMA, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI NYUMBA NA BOMA LA NYUMBA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA 3 | MTAA WA TEMEKE MHANDU, NYAMAGANA - MWANZA | 24/10/2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | NYUMBA Na 2740 BLOCK C | MTAA WA BUSWELU , WILAYA YA ILEMELA MKOA WA MWANZA. | 21/10/2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | SHAMBA EKARI MOJA | ZABAGA - KAHUNDA, WILAYA YA SENGEREMA – MWANZA. | 28/10/2022 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI KWA MALI INAYOHAMISHIKA.
2. MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155**

---

## TANGAZO KUPOTELEWA YARAKA UMILIKI WA KIWANJA

**Modester Kwangu Elias** msimamizi wa mirathi ya Marehemu Kulindwa Shimba
Anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 164 Kitalu "Y1" kilichopo Ibinzamata Manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Modester Kwangu Elias kwa simu namba **0627598379**
**Rbnamba;SHI/SHI/RB/371574/2022**

Jacob F. Mwinuka
AFISA ARDHI
MANISPAA YA SHINYANGA

**Nakala;** Club ya waandishi wa habari, Shinyanga.

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA
Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA
Usimamizi wa mirathi Na.51/2022
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MBARUKU MOHAMEDI MKOMBE
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AZIZA ABDALA SWALEHE

**TANGAZO**
(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 Mwezi 09 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 15 Mwezi 09 Mwaka 2022

HAKIMU

---


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

BURUDANI

# Wizkid aweka rekodi Paris

**PARIS,** Ufaransa

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Wizkid ameweka rekodi ya aina yake kwa kuujaza ukumbi wa Accor Arena uliopo jijini Paris nchini Ufaransa ambao unaingiza watu 20,300.

Wizkid alifanya onyesho la aina yake katika ukumbi huo mwishoni mwa wiki na mastaa kadhaa wakubwa duniani walihudhuria.

Shoo ya Wizkid imeingia kwenye rekodi ya kuwa kubwa sana kati ya zile alizowahi kuzifanya sehemu yoyote duniani kadi sasa.

Na pia Wizkid ameingia kwenye orodha ya wasanii nane kutoka barani Afrika ambao wamewahi kuujaza ukumbi huo wa Accor Arena.

Wasanii hao ni Koffi Olomide, Papa Wemba, Werrason, JP Mpiana, Youssou Ndour, Fally Ipupa na Burna Boy.



# Zuchu ataka ligi na wanaume

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa kike wa Bongo Fleva kutoka familia ya Wasafi Classic Baby (WCB), Zuhura Othman 'Zuchu' amewatangazia vita wasanii wa kiume.

Katika ujumbe wake wakati akielezea juu ya ngoma zake mbili mpya ambazo anatarajia kuziachia siku za hivi karibuni, amesema hakuna msanii wa kike ambaye anaweza kuingia kwenye ligi na yeye.

Zuchu aliposti ujumbe kwenye instagram uliosomeka: "Niwashukuru wazazi wangu ni kwa ajili yenu na uwezo wa Mwenyezi Mungu tu.

"Kwa uandishi wangu yafaa kuwekwa kwenye ligi na wanaume, wadada wenzangu nitawaonea tu.

"Naweza kuwaandikia hata wanaume, jambo la msimu ninaachia nyimbo mbili mwezi huu."



# HARMONIZE KUWEKEZA KWENYE MIWA



**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Rajab Abdul Kahali 'Harmonize" ameonekana kwenye mashamba ya miwa huku akiwaasa wasanii wenzake wawekeze shambani maana ndiko kwenye fedha.

Kupitia video yake fupi aliyoiposti kwenye mtandao wa instagram, ameeleza kuwa kuna maisha baada ya kutumia fedha kwenye klabu, kwani inapatikana zaidi shambani.

Katika video hiyo, Harmonize ameonekana akiendesha trekta lililobeba miwa huku akipakia miwa hiyo kwenye magari ya kubebea.

Hata hivyo, hakutaja eneo ambalo shamba hilo la miwa liliko, licha ya kuwasisitiza wasanii wenzake kuwekeza.

Harmonize kwa sasa ameteka mitandao ya kijamii kutokana na penzi lake na msanii wa Bongo Muvi, Kajala Masanja.

# SAKHO SASA AONYWA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA na mchezaji wa zamani wa Simba, Talib Hilal, amemuonya kiungo wa timu hiyo, Pape Sakho kuacha tabia yake ya kucheza na jukwaa zaidi kuliko kuisaidia timu.

Talib ambaye kwa sasa maskani yake ni nchini Oman, ameisifu Simba kwa kufanikiwa kusonga mbele kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika,pia akisifu upambanaji wa wachezaji.

Simba imetinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo, baada ya kuiondosha Nyasa Big Bullets ya Malawi kwa jumla ya mabao 4-0, ikishinda ugenini mabao 2-0 Septemba 10, na juzi ikipata ushindi kama huo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Nimeangalia mapambano yote mawili, kusema kweli Simba imebadilika, ukweli ni kwamba falsafa iko vilevile ya pasi nyingi, lakini kilichobadilika au kuongezeka ni kujituma na upambanaji wa wachezaji, umenifurahisha sana, wachezaji unaona kabisa wanataka kwenda kufunga mabao, siyo wanacheza kwa kujifurahisha, au kucheza na jukwaa," alisema Talib.

Hata hivyo, alimuonya kiungo raia wa Senagal, Sakho kuwa amekuwa akicheza zaidi na jukwaa kuliko kuisaidia timu, kitu ambacho kinasababisha wakati mwingine mashambulizi ya kushtukiza kuelekea golini kwao.

"Nadhani anatakiwa aambiwe aache kucheza zaidi na jukwaa, ana mambo mengi ambayo hayana msingi, kuna wakati anatakiwa aachie mpira kwa wenzake, lakini anataka kufanya vitu ambavyo vinasababisha anyang'anywe na timu inashambuliwa kwa kushtukiza bila sababu yoyote ya msingi," alisema kocha huyo aliyeipeleka Simba hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2003.

Wakati huo huo, mfadhili wa zamani wa klabu hiyo, Azim Dewji amewataka viongozi kumuachia timu kocha Juma Mgunda kwa sasa, ili kutoivuruga atakapokuja kocha mwingine.

Dewji alisema, pamoja na hayo, Simba imekuwa na bahati mbaya ya kuchukuliwa makocha wake kila wanapokuwa wakiifundisha.

"Mimi naamini Mgunda anaweza kutupeleka mbele, nawaomba aendelee, haina haja ya kutafuta mwalimu kutoka nje kwa sasa, maana hawa walimu wengine kwa sababu Simba ina jina kubwa Afrika kwa sasa, akija tu akikaa kidogo mwaka mmoja wanamchukua, kwa hiyo wamuache.

"Hili linaleta matatizo sana, mimi nilikuwa nagombana na viongozi kwa nini wanatimua makocha, lakini wakaniambia sisi tukimchukua kocha tu inakuwa kosa, wanakuja watu wanatoa pesa nyingi wanamchukua na nikathibitisha hilo, kwa hiyo, kwa kuondoa hayo kwa sasa wamuache, tumecheza mechi nne chini yake tena ngumu na zote tumeshinda," alisema Dewji.




Mshambuliaji wa Simba, Pape Sakho akimiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Nyasa Big Bullets kwenye mechi ya awali mkondo wa pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na wenyeji kushinda mabao 2-0 juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Malindi haitaki kupoa Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Malindi SC, imesema mipango yao ni kuhakikisha michezo yao yote ya nyumbani wanapata alama tatu kwenye Ligi Kuu ya Zanzibar inayoendelea.

Kauli hiyo ya Malindi imekuja baada ya juzi kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wapinzani wao wa miaka mingi, Mlandege FC katika mchezo wa mzunguko wa tatu wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), kwenye mchezo uliochezwa katika Dimba la Amaan majira ya saa moja usiku.

Bao pekee la Malindi katika mchezo huo, lilipachikwa nyavuni na Mohamed Mussa dakika ya 46.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ali Kisaka, alisema kupata ushindi katika mchezo huo ni moja ya mipango yao kwa msimu huu kuhakikisha michezo yao ya nyumbani wanavuna alama zote tatu.

Alisema kipaumbele cha kwanza kwa timu yao ni kuangalia michezo ya nyumbani, pia hata ya ugenini watahakikisha hawakosi alama.

Alisema katika michezo mitatu waliyocheza, wameshinda miwili na kutoka sare moja, hivyo wanataka kuhakikisha mchezo ulio mbele yao wanashinda ili kurejesha hamasa ya mashabiki wa timu hiyo kama ilivyo kuwa miaka iliyopita.

Naye Kocha Mkuu wa timu ya Mlandege FC, Mohammed Abdallah 'Bares', alisema kupoteza mchezo huo dhidi ya Malindi SC kumetokana na makosa madogo yaliyofanywa na wachezaji.

Alisema muda wote kikosi chake kilicheza vizuri hususan dakika 45 za mwanzo, lakini makosa madogo waliyoyafanya dakika ya kwanza tu ya kipindi cha pili ndiyo yaliyotoa mwanya kwa wapinzani wao hao kuwaadhibu.

Katika mzunguko wa nne Mlandege itashuka dimbani kuvaana na Maafande wa Mafunzo, wakati Malindi watakuwa ugenini kupepetana na Kundemba FC.

Matokeo mengine ya mzunguko huo wa tatu hapo jana, timu ya Dulla Boys na Jamhuri zimeshindwa kutambiana kwa kutoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Amaan majira ya saa 10 alasiri wakati katika Dimba la Finya huko Pemba, Black Sailor walikubali kuangukia pua kwa kuchapwa bao 1-0 na Chipukizi FC.

# Mwambusi aahidi kuipambania Ihefu

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Ihefu FC, Juma Mwambusi, ambaye amekabiziwa mikoba ya kuinoa timu hiyo hivi karibuni, amesema moja ya mikakati yake ni kuhakikisha anaipambania timu hiyo ili ifanye vizuri kwenye Ligi Kuu.

Ihefu, inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Bara kutokana na kupoteza michezo yote mitatu iliyocheza tangu kuanza kwa msimu huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwambusi alisema anamuomba Mungu ili malengo yake yafanikiwe ya timu hiyo kufanya vizuri na kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

"Jukumu la kocha yeyote anapopewa kazi ni kuhakikisha anaifanikisha timu kufanya vizuri kwenye ligi na ndivyo ilivyo kwangu na makocha niliowakuta.

"Namuomba Mungu niweze kufikia malengo yangu nipambane ili nipate matokeo mazuri. Ligi ni ngumu hivyo tunahitaji kupambana kupata matokeo mazuri, ushindani umekuwa mkubwa mno, nimeshazungumza na wachezaji kuhusu kujitoa kuipambania timu," alisema Mwambusi.

# Amani Queens vinara Ligi Daraja la Kwanza

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Amani Queens ya Lindi inaongoza Ligi Daraja la Kwanza wanawake inayoendelea nchini, ikiwa inazishirikisha jumla ya timu sita.

Kwa mujibu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), timu hiyo imejikusanyia jumla ya pointi 12, ikiwa imecheza mechi nne, ikishinda zote, mabao tisa ya kufunga, ikiruhusu mawili.

Wakati timu hiyo ikiongoza, timu ya Mapinduzi Queens ya Njombe inashika nafasi ya pili kwa kuwa na pointi tisa, ikiwa imecheza mechi nne, ikishinda mitatu na kupoteza mmoja, mabao 11 ya kufunga na kufungwa matatu.

Mkwawa Queens, yenye maskani yake Iringa nayo ina pointi tisa, ikicheza mechi nne, kushinda tatu, kupoteza moja, mabao 11 na kufungwa matano na inakamata nafasi ya tatu kwenye msimamo huo.

Timu ya Allan Queens ya Dodoma ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi tatu ikifuatiwa Lengo Queens ya Arusha yenye pointi tatu, wakati inayoburuza mkia ni Ukerewe Queens baada ya kupoteza mechi zake zote nne ilizocheza, ikifunga mabao matatu tu, na kufungwa 16.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SALIBA KUJIFUNGA ARSENAL

MLINZI wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 21, William Saliba amedokeza kuwa atasaini mkataba mpya na Arsenal ikiwa klabu hiyo itampa masharti mapya. ***(Sky Sports)***

### ZERBI KUMRITHI ALLEGRI

KLABU ya Juventus ilikuwa inatarajia kumteua, Roberto de Zerbi iwapo watamtimua Max Allegri. ***(Times)***

### MADRID KUMPOTEZEA MBAPPE

REAL Madrid wamepunguza nia yao ya kumnunua fowadi wa Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 23, na hawatamfuatilia tena nyota huyo wa PSG ikiwa hana nia ya kusajiliwa na timu hiyo. ***(Marca)***

### FRANK ANA FURAHA

THOMAS Frank amesema "anafuraha sana" kusalia katika klabu ya Brentford baada ya kuhusishwa na kazi ya ukocha kule Leicester. ***(Sky Sports)***

### FREUND KUULA CHELSEA

CHELSEA wanajiandaa kumteua, Christoph Freund, kama mkurugenzi wao mpya wa michezo baada ya kukubaliana na Red Bull Salzburg. ***(Fabrizio Romano)***

### GLOUKH AWANIWA CELTIC

KLABU ya Celtic inavutiwa na mshambuliaji wa Maccabi Tel Aviv na Israel mwenye umri wa miaka 18, Oscar Gloukh na wanaweza kutuma ofa ya pauni milioni nane Januari. ***(Record)***

### HUDSON-ODOI ANA NAFASI

WINGA wa Chelsea na England, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 21, amesema kuwa ameambiwa na mmiliki wa klabu hiyo, Todd Boehly bado ana nafasi pale Stamford Bridge, licha ya kupelekwa kwa mkopo Bayer Leverkusen. ***(Mail)***

### GAKPO AMEVUMILIA

MCHEZAJI anayelengwa na Manchester United, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23, amevumilia mwanzo "mgumu" wa msimu baada ya winga huyo wa Uholanzi kuhusishwa na kuondoka katika klabu hiyo, amesema mkurugenzi wa michezo wa PSV, Marcel Brands. ***(ED)***

### ZAGADOU KUTUA WEST HAM

MCHEZAJI anayelengwa na klabu ya West Ham, Dan-Axel Zagadou mwenye umri wa miaka 23, anatarajiwa kujiunga na Stuttgart baada ya beki huyo wa Ufaransa kuondoka Borussia Dortmund majira ya joto. ***(Kicker)***

### ARAUJO KAKATAA OFA

MLINZI wa Uruguay, Ronald Araujo mwenye umri wa miaka 23, alikataa ofa kutoka kwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England kabla ya kusaini mkataba wake mpya na Barcelona hadi 2026. ***(Sport)***

### DYCHE, JONES NA CARDIFF

SEAN Dyche na Nathan Jones ni miongoni mwa waliopendekezwa mapema kuwa makocha wa Cardiff baada ya Steve Morison kutimuliwa Jumapili. ***(Wales Online)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RODRYGO AGWAYA NAFASI YA BENZEMA REAL MADRID

●●● Haiwezekani kuichukua, lakini najaribu na ninadhani naendelea vizuri, ninafanya mambo...

**MADRID, Hispania**

MCHEZAJI wa Real Madrid, Rodrygo anaona kuchukua nafasi ya Karim Benzema, "haiwezekani" huku akijinasibu kujitoa kwa hali na mali katika timu hiyo ili aweze kuziba pengo lake wakati huu akiwa majeruhi.

Rodyrgo aliifungia Madrid bao la kwanza katika ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Atletico Madrid, Juzi Jumapili, huku vijana hao wa Carlo Ancelotti, wakiendeleza rekodi yao ya ushindi wa asilimia 100 kwenye LaLiga na kuwa kileleni kuelekea mapumziko ya mechi za kimataifa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, alishirikiana vema na Aurelien Tchouameni na kupachika wavuni bao dakika ya 18, kabla ya Federico Valverde kufanya ubao kusomeka 2-0 kabla ya mapumziko.

Atletico walipambana na kupata bao katika dakika za lala salama kupitia Mario Hermoso, lakini halikutosha kuwapa pointi.

Wakati nahodha wa Real Madrid, Benzema, akitarajiwa kurejea uwanjani baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa, Ancelotti amekuwa akimtegemea Rodrygo kuongoza safu ya ushambuliaji.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amechangia mabao matano katika mechi nane za mwisho za LaLiga na alipoulizwa katika mahojiano baada ya mechi kuhusu kubeba jukumu la Benzema alisema;

"Haiwezekani kuchukua nafasi ya Benzema, lakini najaribu na ninadhani naendelea vizuri. Lazima niseme kwamba ninafanya mambo tofauti kwake, tumebadilisha mtindo wa uchezaji."

Rodrygo na Madrid wameshinda mechi zao zote tisa msimu huu katika mashindano yote, na ndio timu pekee katika ligi tano bora za Ulaya yenye rekodi nzuri.

Na inakuwa mara ya tatu kwa Madrid kushinda mechi tisa za kwanza katika kampeni moja baada ya msimu wa 1961-62 na 1968-69 walipshinda mechi 11 za ufunguzi.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 346,

MECHI KALI

SHEFFIELD WED
VERSUS
BURTON

1 | 1.55
X | 4.01
2 | 4.89

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MOURINHO MAMBO MAGUMU SERIE A



**ROME, Italia**

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho alipewa kadi nyekundu kutokana na kuonyesha hasira zaidi baada ya timu yake kukataliwa penalti katika dakika ya 55 huku ikipoteza kwenye mchezo wao wa nyumbani dhidi ya Atalanta kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Kocha huyo alikuwa na hasira zilizopitiliza, Nicolo Zaniolo alifanyiwa faulo na kusukumwa eneo la hatari na Caleb Okolo na wakati wa marudio ya video yalipoonyeshwa ilionekana kuwa wachezaji wote wawili walikuwa wakivutana jezi na mwamuzi, Daniele Chiffi akapuuza.

Na ndipo Mourinho akaungana na wachezaji wake kupinga uamuzi huo, akikimbia uwanjani na kupiga kelele na kumnyooshea kidole Chiffi, kabla ya mwamuzi kuonyesha kadi nyekundu.

Bao pekee kwenye mchezo huo lilifungwa na Scalvin wa Atalanta, dakika ya 35 na ndilo lilidumu hadi kumalizika kwa mchezo huo.

Roma, sasa wamepoteza mechi mbili kati ya tatu zilizopita za Serie A, idadi kubwa ya vipigo kama walivyopata katika mechi 21 zilizopita ambapo walishinda mechi 11 wakatoka sare nane, na wanashika nafasi ya sita katika msimamo baada ya mechi saba za raundi hii.

# Allegri hana hofu ya kufukuzwa Juventus

**TURIN, Italia**

KOCHA Massimiliano Allegri wa Juventus ameonyesha kutokuogopeshwa na uwezekano wa kupoteza kibarua chake ndani ya klabu hiyo licha ya matokeo mabaya timu hiyo inayopata kwa sasa.

Kocha huyo amewataka watu kutokuhofia kuhusiana na kipigo cha timu yake ilichokumbana nacho katika mchezo wa ligi ya mabingwa Ulaya na huku ikiwa haina matokeo mazuri kwenye Ligi baada ya juzi Jumapili kuambulia sare.



Ikumbukwe Juventus haina alama yoyote kwenye michuano hiyo ya Ulaya baada ya kupoteza michezo yote miwili ya kwanza.

Na pamoja na ugumu wote wanaopitia Juventus, Allegri anaamini yeye ndo mtu pekee wa kuivusha klabu hiyo katika wakati mgumu iliokua nao kwa sasa.

"Ndio kabisa, tuna ugumu kidogo japo kuna wachezaji wachache wanakosekana," alisema Allegri wakati alipoulizwa kama anaweza kubadili hali ya hewa ndani ya klabu hiyo kwa sasa.

"Lazima tufanye kazi wote na ni wajibu wa wote, kwa sasa ninachoangalia ni kuivusha klabu kwenye wakati mugumu."

## HABARI MICHEZO

,249,820

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

# MJAPANI, SAIDO DIMBANI GEITA GOLD IKIIVAA SINGIDA BIG STARS

**Na Hadija Mngwai**

KIUNGO mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Saido Ntibazonkiza pamoja na Mjapani Shinobu Sakai, wanatarajiwa kuanza kuitumikia Geita Gold FC katika mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Singida Big Star kesho.

Ntibazonkiza alijiunga na Geita Gold msimu huu ambapo alishindwa kuitumikia timu hiyo katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kutokana na usajili wake Caf kutokamilika.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa Geita Gold, Abdallah Mpambayage, alisema nyota huyo raia wa Burundi, Saido na Sakai kutoka Japan, wanatarajiwa kuanza kuitumikia timu hiyo dhidi ya Singida Big Star kesho.

"Nyota wetu wa kimataifa wote wapo sawa, usajili wao upo vizuri na wanatarajiwa kuanza kutumika katika mchezo wetu unaofuata dhidi ya Singida Big Star.

"Awali hawakuweza kucheza mechi za kimataifa kutokana na usajili wao kutokamilika Caf, lakini kwenye ligi wataanza kutumika mchezo ujao," alisema Mpambayage.

Mchezo huo dhidi ya Singida Big Star ulikuwa uchezwe wiki iliyopita, lakini ukasogezwa mbele hadi kesho ili kuipa nafasi Geita Gold kutekeleza vema majukumu yaliyokuwa yakiwakabili ya kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, kwa sasa Geita Gold imetupwa nje kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho kwa faida ya bao la ugenini baada ya mechi ya kwanza ugenini kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Hilal Alsahil SC ya Sudan kabla ya mchezo wa marudiano kuwachapa Wasudani hao mabao 2-1, hivyo kufanya matokeo ya jumla kuwa 2-2.



Mchezaji wa Klabu ya Gofu Lugalo, Gilman Kasiga, akipiga mpira katika mashindano yaliyofanyika hivi karibuni. **MPIGAPICHA WETU**

# Kasiga wa Gofu Lugalo kuwania uenyekiti TGU

**Na Mwandishi Wetu**

UCHAGUZI Mkuu wa Chama cha Gofu Tanzania (TGU), umepamba moto baada ya mchezaji maarufu wa Klabu ya Lugalo, Gilman Kasiga, kuchukua fomu kuwania nafasi ya uenyekiti.

TGU imepanga kuchagua viongozi wake Oktoba 6, mwaka huu katika uchaguzi uliopangwa kufanyika katika Klabu ya Gymkhana ya mkoani Morogoro ambapo Oktoba 5 itakuwa siku ya mchujo wa wagombea.

Pia mchezaji wa timu ya gofu ya Arusha Gymkhana, Pridence Kamugisha, naye amechukua fomu ya kugombea nafasi ya makamu mwenyekiti.

Akizungumza baada ya kuchukua fomu ya kugombea uongozi, Kasiga alisema sababu kubwa ya kuwania nafasi hiyo ni kuleta maendeleo makubwa ya mchezo huo hapa nchini akiainisha maeneo makuu matatu.

Kasiga alitaja eneo la kwanza ni kuendeleza mchezo wa gofu kwa vijana ili kuwa na 'mastaa' wajao baada ya kizazi kilichopo kuacha kucheza na pili kuwazesha watu wazima kujiunga na mchezo ikiwa sehemu ya kuimarisha mtandao miongoni mwao.

"Lengo la tatu ni kuimarisha wachezaji wa gofu wa kulipwa ambao kimsingi ndio makocha wa wachezaji wa sasa, vijana na watu wazima," alisema.

Alisema uongozi wake utazingatia misingi yote ya utawala bora ikiwa pamoja na uadilifu, uwazi, nidhamu na masuala mbalimbali ambayo yatawavutia wadau ikiwa ni pamoja na kampuni kudhamini mashindano mbalimbali.

Kisiga alisema wanatarajia kuwa na mafunzo mbalimbali ya ufundi kwa wachezaji kwa lengo la kuboresha zaidi viwango vya wachezaji huku akifafanua kuwa kutakuwa na mipango ya maendeleo ya muda mfupi, kati na mrefu ili kufikia kiwango cha juu kabisa cha maendeleo.

"Pia tutauleta mchezo wa gofu kwa jamii yote ya Watanzania na kuondoa dhana ya mchezo kuwa ni wa watu wenye kipato cha hali ya juu (matajiri), jambo ambalo limewafanya wachezaji chipukizi wenye vipaji kuogopa kucheza, vijana wenye rika la kushindana na watu wazima kushindwa kuingia," alisema Kasiga.



| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/09/22 | 20:30 | Bastia Borgo vs Le Mans | 2.78 | 3.13 | 2.46 |
| 02. 23/09/22 | 20:30 | Saint Brieuc vs Orleans | 2.48 | 3.15 | 2.75 |
| 03. 23/09/22 | 20:30 | Villefranche Sur Saone vs Bourg Peronnas | 2.35 | 3.14 | 2.94 |
| 04. 23/09/22 | 20:30 | Paris 13 Atletico vs Avranches | 2.63 | 3.08 | 2.63 |
| 05. 23/09/22 | 20:30 | FC Versailles 78 vs Nancy | 2.32 | 3.14 | 2.99 |
| 06. 23/09/22 | 20:30 | Sedan vs Le Puy | 2.34 | 3.15 | 2.95 |
| 07. 23/09/22 | 21:00 | Ireland U21 vs Israel U21 | 2.27 | 3.14 | 2.94 |
| 08. 23/09/22 | 21:45 | Italy vs England | 2.62 | 3.17 | 2.68 |
| 09. 23/09/22 | 21:45 | Finland vs Romania | 2.29 | 3.24 | 3.09 |
| 10. 23/09/22 | 21:45 | Alloa Athletic vs Airdrieonians | 2.43 | 3.63 | 2.43 |
| 11. 23/09/22 | 22:00 | Dordrecht vs Maastricht | 2.33 | 3.53 | 2.68 |
| 12. 23/09/22 | 22:00 | Morocco vs Chile | 2.70 | 3.27 | 2.60 |
| 13. 23/09/22 | 22:00 | The New Saints vs Dundee FC | 2.64 | 3.57 | 2.27 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 20/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 2079 | Shanghai Shenhua vs Meizhou Kejia | 2.61 | 3.15 | 2.51 |
| 12:30 | 5017 | Changchun Yatai vs Wuhan Three Towns FC | 4.12 | 3.78 | 1.69 |
| 13:00 | 3336 | Roasso Kumamoto vs Grulla Morioka | 1.49 | 3.87 | 5.88 |
| 14:30 | 1593 | Dalian Aerbing vs Hebei Zhongji | 1.09 | 7.82 | 19.56 |
| 14:30 | 3959 | Henan Jianye vs Shanghai SIPG | 4.11 | 3.42 | 1.77 |
| 14:30 | 5769 | Wuhan Zall vs Shenzhen | 2.14 | 3.34 | 3.00 |
| 16:00 | 1258 | Huracan Reserve vs Boca Jrs | 2.85 | 3.29 | 2.24 |
| 16:00 | 1368 | Millwall U23 vs Charlton U23 | 2.18 | 3.62 | 2.74 |
| 16:45 | 1623 | Arman Gohar Sirjan vs Khosheh Talaei | 1.91 | 2.90 | 4.70 |
| 17:00 | 1990 | Buqaa Amman vs Kfarsoum | 2.22 | 3.20 | 3.15 |
| 17:00 | 3793 | Rudar Velenje vs NK Nafta | 3.34 | 3.39 | 1.98 |
| 17:15 | 4732 | Shams Azar Qazvin vs Shahrdari Hamedan | 2.11 | 2.65 | 4.30 |
| 18:00 | 1295 | TSV Rain/Lech vs Augsburg II | 2.76 | 3.30 | 2.30 |
| 20:00 | 5385 | SC Kalsdorf vs SV Allerheiligen | 2.45 | 3.50 | 2.47 |
| 21:00 | 1233 | Leyton Orient vs Sutton United | 2.11 | 3.24 | 3.14 |
| 21:00 | 1311 | Tranmere vs Bolton | 2.75 | 3.24 | 2.34 |
| 21:00 | 1636 | Crewe vs Leeds United U23 | 2.10 | 3.68 | 2.84 |
| 21:00 | 2797 | Carlisle vs Fleetwood Town | 2.85 | 3.29 | 2.25 |
| 21:00 | 3029 | Swindon Town vs Plymouth | 2.70 | 3.34 | 2.33 |
| 21:00 | 3231 | Barnsley vs Newcastle U23 | 1.81 | 3.82 | 3.48 |
| 21:00 | 3671 | Shrewsbury vs Port Vale | 2.24 | 3.19 | 2.94 |
| 21:00 | 4354 | Lincoln vs Doncaster | 1.54 | 3.94 | 5.12 |
| 21:00 | 4395 | Northampton vs Cambridge Utd | 2.50 | 3.24 | 2.55 |
| 21:00 | 4555 | Stevenage vs Wycombe | 2.60 | 3.24 | 2.46 |
| 21:00 | 4763 | Morecambe vs Hartlepool | 1.99 | 3.39 | 3.29 |
| 21:00 | 5175 | Rochdale vs Liverpool U23 | 2.16 | 3.64 | 2.75 |
| 21:00 | 5474 | Cheltenham vs Walsall | 1.95 | 3.39 | 3.44 |
| 21:00 | 5656 | Sheffield Wed vs Burton | 1.55 | 4.01 | 4.89 |
| 21:30 | 2927 | Peterborough vs Tottenham U23 | 2.00 | 3.69 | 3.05 |
| 21:30 | 3253 | Grimsby vs Mansfield | 2.59 | 3.28 | 2.45 |
| 21:30 | 4546 | Stockport vs Wolverhampton U23 | 2.75 | 3.59 | 2.18 |
| 21:30 | 4963 | Salford City vs Accrington | 2.35 | 3.29 | 2.70 |
| 21:45 | 1707 | Enfield Town vs Canvey Island | 2.28 | 3.43 | 2.70 |
| 21:45 | 2080 | Harrow Borough vs Hendon | 2.23 | 3.64 | 2.65 |
| 21:45 | 2094 | Herne Bay vs AFC Hornchurch | 3.94 | 3.75 | 1.73 |
| 21:45 | 2330 | Corinthian Casuals vs Folkestone Invicta | 2.85 | 3.34 | 2.22 |
| 21:45 | 2478 | Haringey Borough vs Billericay Town | 1.99 | 3.53 | 3.19 |
| 21:45 | 2814 | East Fife vs Stenhousemuir | 2.22 | 3.24 | 2.94 |
| 21:45 | 3003 | Guiseley vs Matlock Town | 2.85 | 3.25 | 2.26 |
| 21:45 | 3031 | Bishop Stortford vs Bowers Pitsea | 1.29 | 4.89 | 8.22 |
| 21:45 | 3494 | Newport vs Forest Green | 2.55 | 3.24 | 2.50 |
| 21:45 | 3812 | AFC Wimbledon vs Crawley Town | 1.95 | 3.33 | 3.48 |
| 21:45 | 3930 | Wingate and Finchley vs Horsham | 2.47 | 3.45 | 2.47 |
| 21:45 | 4507 | Ipswich vs Arsenal U23 | 1.64 | 3.93 | 4.23 |
| 21:45 | 5002 | Potters Bar Town vs Brightlingsea Regent | 1.98 | 3.54 | 3.20 |
| 21:45 | 5286 | Warrington Rylands 1906 FC vs Marske United FC | 2.75 | 3.54 | 2.20 |
| 21:45 | 5664 | Stranraer vs Dumbarton | 3.09 | 3.24 | 2.14 |
| 22:00 | 1609 | CA Fenix vs Defensor Sporting | 3.18 | 3.13 | 2.14 |
| 23:00 | 4875 | FC Aguablanca vs Barranquilla FC | 2.02 | 3.10 | 3.53 |
| 23:45 | 2896 | SOL De America vs Resistencia FC | 2.23 | 3.09 | 3.05 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumanne Septemba 20, 2022

Nipashe




Rodrygo agwaya nafasi ya Benzema UKURASA 29

SURA ZA KAZI...



Nyota hatari wa Simba, kutoka kushoto ni Pape Sakho, Moses Phiri na kiungo mpishi wa mabao, Clatous Chama wakishangilia baada ya kufanya yao. **MPIGAPICHA WETU**

# Simba: Hesabu zetu sasa kwa de Agosto

**Na Saada Akida**

## ●●● Mgunda akoleza moto amtaja Dejan huku akimwelezea Phiri kuwa...

BAADA ya kufanikiwa kuitoa Nyasa Big Bullets ya Malawi kwenye raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa jumla ya mabao 4-0 kwa kushinda 2-0 ugenini na nyumbani, miamba ya soka nchini, Simba imesema sasa hesabu zao wanazigeuzia kwenye mechi ya raundi ya kwanza dhidi ya Primeiro de Agosto ya Angola.

**Simba itaanzia ugenini katika mechi ya raundi ya kwanza itakayopigwa kati ya Oktoba 7-9, mwaka huu kwa kuwavaa Waangola hao ambao wameitoa Red Arrows ya Zambia kwa jumla ya mabao 2-1 baada ya kushinda 1-0 ugenini na juzi nyumbani kutoka sare ya bao 1-1.**

Akizungumza na gazeti hili, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema sasa wanakwenda kujipanga kwa ajili ya mchezo huo dhidi ya Primeiro de Agosto ili kuhakikisha wanapambana kutafuta matokeo mazuri na kuweza kufikia malengo yao ya kuendelea kusonga mbele hadi kufika robo fainali.

Mgunda alisema tayari ameona makosa waliyofanya katika mchezo huo, hivyo anakwenda kuyafanyia kazi kabla ya mechi hiyo ya raundi ya kwanza ili kuendelea kufanya vizuri.

"Kuna mazuri yamefanyika na tunaenda kuboresha kuwa bora zaidi," alisema.

Akizungumzia mchezo dhidi ya Nyasa Big Bullets, Mgunda alisema: "Tuliishika mechi, tulijua kwamba watashambulia kwa sababu hawakuwa na chakupoteza, hivyo tulikuwa makini katika safu ya ulinzi, lakini tulishambulia pia".

Kuhusu mshambuliaji Dejan Georgijević Mgunda alisema ni mchezaji mzuri na muda wote atatumika, kwa sababu ana uwezo mkubwa na kinachohitaji ni kumpa nafasi ya kuzoea mazingira.

Pia alimpongeza Moses Phiri kwa kuwa na mwendelezo mzuri wa kufunga kila mechi jambo ambalo linamfanya kuamini kwamba nyota huyo anavitu vya ziada vya kuweza kusaidia timu.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohammed Mchengerwa, amewapongeza wachezaji wa Simba kwa matokeo ya juzi na kuwataka kupambana kwa ajili ya kutangaza soka la Tanzania kwa mataifa mengine.

Mchengerwa ambaye alikuwa miongoni mwa wageni waalikwa katika mchezo huo wa Simba dhidi ya Nyasa Big Bullets uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, baada ya mechi kumalizika alikwenda vyumba vya kubadilishia nguo na kuwapongeza kwa ushindi huku akiwataka kupambana katika hatua inayofuata.

"Tukiri wote waliokuwapo uwanjani hatukutamani mchezo uishe kwa sababu ya namna mpira ulivyokuwa ukichezwa, nawaomba sana wachezaji huu mwanzo twende nao hadi mwisho.

"Hatuna sababu ya kushindwa tunataka timu zetu zinazocheza kimataifa zifanye vizuri na kuvuka katika hatua hii na kuzidi kusonga mbele, soka letu lipige hatua kwa sababu mechi hizi zinatazamwa na mataifa mbalimbali," alisema Mchengerwa.

## Yanga yaiendea 'chimbo' Al Hilal CAF

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha hawafanyi makosa kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Klabu ya Yanga imesema tayari imeanza kufanyia kazi kiufundi mchezo wao ujao dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

Yanga imefanikiwa kutinga hatua hiyo baada ya ushindi mnono wa mabao 9-0 dhidi ya Zalan FC ya Sudan Kusini kwa kushinda ugenini 4-0 na nyumbani 5-0, mechi zote zikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Hivyo katika raundi ya Kwanza sasa itakayoanza kutimua vumbi kati ya Oktoba 7-9, mwaka huu, Yanga itaanzia nyumbani dhidi ya Al Hilal iliyoitoa St. George ya Ethiopia kwa faida ya bao la ugenini kutokana na kufungwa 2-1 ugenini kabla ya juzi ikiwa nyumbani Sudan kushinda 1-0.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wanaingia katika chimbo kwa ajili ya kuendelea kutafuta michezo ya wapinzani wao Al Hilal na kuangalia ubora wao ili kuufanyia kazi.

Alisema wakati wanawafuatilia wapinzani wao, wana kazi kubwa ya kufanyia kazi mapungufu yao kwa washambuliaji kuwa makini katika nafasi wanazotengeneza.

"Ni kweli hatukucheza vizuri na shida ni umakini wa washambuliaji wetu, tuna kazi kubwa kwa benchi la ufundi katika kuendelea kuwakumbusha wachezaji kuwa makini katika kuzitumia nafasi kupata mabao," alisema Kaze.

Alisema katika hatua wanayokwenda kucheza ni ngumu kwa sababu ya ubora wa wapinzani wao Al Hilal ambao wamekuwa na uzoefu mkubwa katika mashindano hayo.

Kwa upande wa Daktari wa Yanga, Shecky Mngazija, alisema hali ya mshambuliaji Fiston Mayele na kiungo Feisal Salum 'Fei Toto' bado wako chini ya uangalizi baada ya kuumia katika mchezo uliopita dhidi ya Zalan FC.

"Wachezaji hao bado hawajaanza mazoezi na wako chini ya uangalizi wa jopo la madaktari wa timu," alisema Mngazija.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >